RICHMOND PUBLIC SCHOOLS

rvaschools.net

# ALAMA
# KANUNI YA MAADILI YA UWAJIBIKAJI YA WANAFUNZI



Ustahimilivu.Fahari.Mafanikio.

**2022-23**

# Yaliyomo

**UTANGULIZI** ..... **5**

Kanuni ya Maadili ya Uwajibikaji ya Wanafunzi ni Nini (SCORE)? ..... 5
Kwa Nani, Lini na Wapi Kanuni hii Inatumika? ..... 5

**MAJUKUMU YA WASHIKADAU** ..... **6**

Majukumu na Kuhusika kwa Wazazi, Walezi na/au Familia ..... 6
Majukumu ya Wafanyakazi wa Shule ..... 6
Jukumu la Washiriki wa Jamii ..... 7
Haki na Majukumu ya Wanafunzi ..... 7
Ukaguzi na Upokonyaji ..... 7

**MAJIBU KWA TABIA YA WANAFUNZI** ..... **8**

Ni nani Humwarifu Mzazi/Mlezi? ..... 8
Ni Nani Anayependekeza Kuondoshwa kwa Muda Mrefu au Kufukuzwa? ..... 8

**VIWANGO VYA HATUA NA MAJIBU** ..... **9**

**MAJIBU YA KIWANGO CHA SHULE ZA MSINGI KWA TABIA ZA WANAFUNZI** ..... **10**

**MAJIBU YA KIWANGO CHA SHULE ZA UPILI KWA TABIA ZA WANAFUNZI** ..... **13**

**TABIA ZA WANAFUNZI** ..... **16**

Kategoria A: Tabia ambazo Zinazuia Maendeleo ya Kielimu (BAP) ya mwanafunzi au wanafunzi wengine ..... 16
Kategoria B: Tabia zinazohusiana na Shughuli za Shule (BSO) zinatatiza shughuli za kila siku za taratibu za shule ..... 16
Kategoria C: Tabia za Mahusiano (RB) zinaunda uhusiano mbaya kati ya wanachama 2 au zaidi wa jamii ya shule (Hakuna madhara ya kimwili yaliyofanyika) ..... 19
Kategoria D: Tabia zinazosababisha Wasiwasi wa Usalama (BSC) zinaunda hali zisizo salama kwa wanafunzi, wafanyakazi, na/au wageni wa shule ..... 20
Kategoria E: Tabia ambazo Zinahatarisha Mtu au Watu Wengine (BESO), tabia hizi zinahatarisha afya, usalama, au ustawi wa mwanafunzi au watu wengine katika jamii ya shule ..... 23

**KUONDOSHWA KWA MUDA, KUFUKUZWA, NA RUFAA** ..... **25**

Kuondoshwa Kwa Muda Mfupi (siku 10 au chini) ..... 25
Kuondoshwa kwa Zaidi ya Siku Kumi au Kufukuzwa ..... 26
Kufukuzwa ..... 26
Taratibu za Kusikilizwa mbele ya Msimamizi au Mwakilishi wake ..... 27
Rufaa za Kuondoshwa kwa Muda Mrefu na Kufukuzwa ..... 27
Idadi ya Wanafunzi ..... 28
Taratibu za Kuondolewa ..... 28
Silaha/Dawa za Kulevya/Bidhaa Zinazodhibitiwa/Majeraha Mabaya ya Kimwili ..... 30
Mengineyo ..... 30
Usikilizaji Ulioharakishwa ..... 30

Ufafanuzi wa Maneno ... 30
**TAARIFA ZA SHUGHULI ZINAZODAIWA ZA UTOVU WA NIDHAMU ... 31**
Maelezo ya Rufaa ... 31
**KUKUZA TABIA NZURI YA WANAFUNZI KWENYE MABASI YA SHULE ... 32**
Matokeo ya Tabia Zisizofaa katika Basi la Shule ... 32
**TITLE IX ... 34**
Title IX ni nini? ... 34
Inamaanisha nini? ... 34
Kwa nini Title IX ni muhimu? ... 34
**KUFAFANUA "NJIA YA RPS" YA KUREJESHA MAADILI ... 35**
**SERA YA MAHUDHURIO YA WANAFUNZI ... 35**
Kwa nini Mahudhurio ni Muhimu? ... 35
Ni Katika Hali Gani Wanafunzi wa Zamani Wanahudhuria Shule? ... 36
Kutokuwepo Ukiwa na Ruhusa ni nini? ... 36
Ni Lini Wanafunzi Wanazingatiwa Wapo Ijapokuwa Sio Shuleni? ... 36
Kuchelewa/Kuondoka Shuleni Bila Ruhusa ... 36
Majukumu ya Wazazi ... 37
Kazi ya Kurudia Inaweza Kuombwa? ... 37
Jukumu la Shule ni Nini Wakati Mwanafunzi hayupo? ... 37
Sera ya Ruhusa ya Kutohudhuria ... 37
**TARATIBU ZA MATUMIZI YANAYOKUBALIKA YA INTANETI YA SHULE ZA UMMA ZA RICHMOND ... 38**
Matumizi ya Intaneti kwa Ajili ya Mafunzo ya Shule za Umma za Richmond ... 38
Taratibu za Matumizi Yanayokubalika ya Intaneti ya Shule za Umma za Richmond ... 38
Matumizi Yanayokubalika ... 38
Mali ya Kisheria ... 38
Matumizi Yasiyokubalika ... 39
**KAMUSI ... 40**
**NAMBARI ZINAZOPIGWA MARA KWA MARA ... 44**
**WANACHAMA WA BODI YA SHULE ... 44**
**MAJUKUMU YA WAZAZI NA KUHUSIKA NA UKUBALIFU WA UKAGUZI WA KANUNI YA MAADILI YA UWAJIBIKAJI YA WANAFUNZI ... 47**

RPS RICHMOND PUBLIC SCHOOLS

Wapenda Wanafunzi, Familia, na Wafanyakazi wa RPS,

Karibu kwa mwaka wa masomo wa 2022-2023! Tunafuraha sana kuwakaribisha shuleni tena.

Shule za Umma za Richmond (RPS) zimejitolea kutoa mazingira salama na yenye upendo ambayo yanahakikisha wanafunzi wote wanahisi wamekaribishwa na wanaungwa mkono na zana wanazohitaji ili kufanikiwa.

Washikadau mbalimbali walishirikiana ili kukagua Kanuni ya Maadili ya Uwajibikaji wa Wanafunzi (SCORE) ya mwaka wa masomo wa 2022-2023; kazi yetu inalingana pia na *Mwongozo wa Kielelezo cha Serikali cha Kanuni ya Maadili Mema na ya Kuzuia ya Sera ya Tabia za Wanafunzi na Mibadala ya Kuondoshwa Shuleni*.

Lengo la SCORE ni kuendelea kuweka kigezo cha juu kwa wanafunzi wetu huku tukifahamu kwamba kwa kufanya hivyo lazima tutumie njia ambazo zinafahamu kiwewe na za kurejesha maadili. Hii inamaanisha kwamba ijapokuwa tunamaanisha kwamba wafanyakazi wa shule wanapaswa kushughulikia ipasavyo tabia ambazo zinaathiri vibaya mazingira ya shule, tunaamini pia kwamba tunaweza kuwasaidia wanafunzi kujifunza kutoka kwa makosa yao na kuwasaidia kufanya maamuzi bora baadaye. RPS zitakuwa divisheni ya shule zenye lengo la makusudi la kuunda na kudumisha mahusiano, na moja ambazo zinapunguza matokeo ya kinidhamu kwa kuyabadilisha na chaguo ambazo zinawaweka wanafunzi shuleni, wakiwa wameunganishwa na jamii ya shule yao.

Kama familia za RPS, una jukumu muhimu la kuunga mkono juhudi zetu, na ushiriki wako ni muhimu kwa kitengo cha shule na mtoto wako. Wazazi na watoa huduma, tafadhali mpitie SCORE pamoja na watoto wenu ili mhakikisha kuwa wanaelewa matarajio ya RPS na wako tayari kwa mwaka wa masomo wenye ufanisi. Ukipitia, tafadhali tia sana na urejeshe fomu (iliyo ukurasa wa mwisho) kwa shule ya mtoto wako kabla ya Ijumaa, 30 Septemba 2022.

Asante kwa msaada wako unaoendelea tunaposhughulika kuhakikisha kwamba shule zote ZA RPS zina mazingira salama na jumuishi ambapo wanafunzi wanahisi wamekaribishwa, wanaheshimiwa, na wanapendwa.

Shukrani nyingi,

**Jason Kamras**
Msimamizi

Richmond Public Schools | 301 North 9th Street | Richmond, VA | www.rvaschools.net



# UTANGULIZI

## Kanuni ya Maadili ya Uwajibikaji ya Wanafunzi ni Nini (SCORE)?


Kanuni ya Maadili ya Uwajibikaji ya Wanafunzi (SCORE) ni mwongozo ambao unafafanua tabia inayofaa na isiyofaa. SCORE hushughulikia pia matokeo na hatua za kinidhamu ambazo zinaweza kuamuliwa kuwa zinafaa. Mwongozo huu umeundwa ili kuhimiza uraia mwema na kukuza tabia nzuri ambayo itasababisha ustawi wa jumla ya wanafunzi. SCORE uhakikisha kwamba familia, wanafunzi na wafanyakazi wa shule wanafahamu haki na majukumu yako kuhusiana na tabia ya mwanafunzi. Huweka pia viwango vya taratibu zinazotumiwa katika kushughulikia makosa mahsusi ya kinidhamu. Lengo la SCORE ni kuhakikisha kila mwanafunzi anaweza kufikia elimu bora katika mazingira ambayo ni mazuri kwa mafunzo na kusoma.

## Kwa Nani, Lini na Wapi Kanuni hii Inatumika?

Wanafunzi wanasimamiwa na Kanuni hii nyakati zote wakiwa chini ya mamlaka ya divisheni ya shule ikiwemo, lakini haijakomea kwa nyakati kama vile: (1) kwenye rasilimali ya shule, ambayo inajumuisha mali yoyote isiyohamishika inayomilikiwa au kukodishwa kwa Bodi ya Shule, au kuendeshwa na au kwa niaba ya Bodi ya Shule; (2) kusubiri basi la shule katika vituo villivyoteuliwa vya basi; (3) kutumia njia rahisi zaidi ya kwenda na kutoka shuleni, ikiwemo kwenda na kutoka kituo kilichoteuliwa cha basi la shule; (4) kwenye basi la shule; au (5) kushiriki, au kuhudhuria shughuli zinazodhaminiwa na shule/ zinazohusiana na shule, kama vile safari za kimasomo, makongamano na/au matukio ya riadha.

Wanafunzi wanasimamiwa pia na Kanuni hii wakishiriki katika shughuli fulani za baadhi ya shule, hata kama wako nje ya rasilimali ya shule. Hata kama mwanafunzi anakiuka SCORE kwa shughuli zinazofanyika nje ya wakati na maeneo yaliyoangaziwa hapo juu, huenda bado mwanafunzi huyo akapata matokeo yanayofaa yaliyowekwa na divisheni ya shule ikiwa hatua hizi zinahatarisha usalama wa wanafunzi na watu wengine wazima.

# MAJUKUMU YA WASHIKADAU







Washikadau wote wanaweza kutekeleza jukumu muhimu katika kuwasaidia wanafunzi wetu kufuata SCORE. Makundi ikiwemo wazazi, walezi, na familia za kitivo na wafanyakazi wa Shule za Umma za Richmond, na washiriki wa jamii wana majukumu muhimu kama wakuzaji, mifano ya kuigwa, na washauri. Maelezo yaliyo hapa chini yanaelezea jukumu la kila kundi katika kuwasaidia wanafunzi wetu katika kufanya maamuzi mazuri ya kitabia.

## Majukumu na Kuhusika kwa Wazazi, Walezi na/au Familia

Msaada wa wazazi/walezi na familia wa SCORE husaidia kukuza mazingira ya elimu ambayo yanalenga haki za kila mwanafunzi na kukuza mazingira salama na kakamavu ya kielimu ambayo inawapa wanafunzi wote nafasi ya kufikia uwezo wao.

Shule za Umma za Richmond zinawahimiza wazazi/walezi na familia kukagua SCORE na rasilimali za ziada zilizoorodheshwa katika Idara ya Elimu ya Virginia ya Mwongozo wa Wazazi wa Kuelewa Sera na Kanuni katika Shule za Virginia ambao unazungumzia hasa yafuatayo: a) kuhakikisha mazingira salama ya masomo b) majukumu na haki za wazazi c) mchakato na taratibu za kinidhamu d) mapendekezo ya wazazi. Mwongozo wa Wazazi wa Kuelewa Sera na Kanuni katika Shule za Virginia upo hapa www.doe.virginia.gov/support/student_conduct/parents_guide_student_discipline_policies.pdf.

Kwa kuongezea majukumu ya wazazi yaliyoangaziwa katika Mwongozo wa Wazazi wa Kuelewa Sera na Kanuni katika Shule za Virginia, wazazi/walezi wa Shule za Umma za Richmond wanawajibika kuhakikisha wanafunzi wanapata kazi zote zilizokosekana wakati wa kuondoshwa shuleni. Kulingana na Sera ya Bodi ya Shule ya 8-3.13, mwanafunzi ambaye ameondoshwa shuleni, iwe kwa muda mfupi au kwa muda mrefu, atapokea na kukamilisha kazi zote za elimu (kazi za darasani na za nyumbani) wakati wa kipindi hicho cha kuondoshwa shuleni. Lazima wanafunzi wawasilishe kazi iliyokamilishwa kwa mwalimu wao wa darasani baada ya kurudi shuleni. Ni wajibu wa mzazi/mlezi kuwasiliana na shule, kufanya mipango ya kuchukua kazi shuleni, na kurudisha kazi iliyokamilishwa shuleni.

## Majukumu ya Wafanyakazi wa Shule

Kitivo na wafanyakazi wanawajibika kuunda na kudumisha mazingira salama na yenye upendo ya shule ambayo inafaa mafunzo na elimu. Kama matokeo yake, walimu na wafanyakazi wengine wanapaswa kufanya kazi kwa pamoja na usimamizi ili kukuza, kutekeleza na kuwasiliana taratibu kwa wanafunzi na familia kwa njia ambayo ni rahisi kuelewa na hata pia kuwasaidia wanafunzi katika kufanya maamuzi yanayofaa ya kitabia.

Kitivo na wafanyakazi wanawajibika pia kufuata mfumo wa rufaa ulioangaziwa katika SCORE. Walimu wanapaswa kutumia muundo wa kusimamia darasa ambao unalingana na hatua zilizoangaziwa katika SCORE. Ijapokuwa kwa ujumla walimu wanawajika kushughulikia tabia nyingi za wanafunzi darasani, ikihitajika, walimu wanatarajiwa kuwaelekeza wanafunzi kwa msimamizi ili kupokea hatua zinazofaa. Mwalimu mkuu wa shule na/au mwakilishi wake anawajibika kushughulikia tabia ya mwanafunzi baada ya kupokea rufaa ya mwalimu/mfanyakazi. Huku walimu au wasimamizi wa shule wakishughulikia hatua nyingi za kinidhamu za wanafunzi, makosa makali, au ya kurudiwa, wanahitaji kuhusika kwa ofisi kuu ya usimamizi kupitia Msimamizi, Afisa wa Kusikiliza Kesi za Kinidhamu, na/au Bodi ya Shule.

Kitivo na wafanyakazi watazingatia hatua zifuatazo wakibainisha hatua / matokeo yanayofaa zaidi ya kinidhamu. a) hali na ukali wa ukiukaji b) umri wa mwanafunzi c) rekodi ya awali ya nidhamu d) hali nyingine yoyote muhimu. Msimamizi au mwakilishi wake anaweza kuona inafaa kuwabadilisha wanafunzi kutoka kwa maeneo yao ya shule hadi shule nyingine mbadala kwa muda fulani uliowekwa.

## Jukumu la Washiriki wa Jamii

Washiriki wa jamii wana jukumu muhimu la kuwasaidia wanafunzi kufuata SCORE kwa kushughulikia mahitaji kadhaa muhimu. Shule za Umma za Richmond zina washirika wa kimkakati na mashirika mbalimbali ndani ya Jiji la Richmond ili kutoa msaada wa ziada kwa wanafunzi ambao unashughulikia afya yao ya kimwili, kijamii, kihisia na kiakili. Kwa hivyo, washiriki wa jamii wanawajibika kutoa huduma zilizokubaliwa na msaada kwa wanafunzi ili kuwasaidia katika kufuata SCORE na kuboresha mafanikio yao ya kielimu.

## Haki na Majukumu ya Wanafunzi

Wanafunzi wana haki na majukumu ya:

- Kuhudhuria shule na kupokea elimu bora. Ni wajibu wa mwanafunzi kuhudhuria shule na madarasa aliyopewa kila siku. Kutokuwepo kunapaswa kuripotiwa kwa shule, kwa simu, kila siku. Baada ya kurudi shuleni, wanafunzi wanahitajika kupatia shule barua iliyoandikwa kutoka kwa mzazi/mlezi ambayo inafafanua sababu ya kutokuwepo.
- Kufahamishwa kuhusu kanuni zote za shule na hatua/matokeo yaliyowekwa yanayohusishwa na tabia nyingine zisizofaa. Ni wajibu wa wanafunzi kujua na kufuata kanuni zote za shule, na kukubali matokeo ya tabia zao. Wanafunzi wanapaswa kuelewa SCORE.
- Kuhakikisha maelekezo ya SCORE yamefuatwa.
- Kufahamishwa jinsi gredi zinavyohesabiwa na kupatikana.
- Kutumia maeneo na nyenzo za shule kwa njia inayofaa kila wakati.
- Kuheshimu mawazo, imani na vitambulisho vya wengine. Dhana hazipaswi kuwakera au kuwaumiza wengine.
- Kujadili au kutafuta ushauri kuhusiana na ukosefu wa maendeleo ya kielimu.
- Kuheshimu, na kuheshimiwa, na wanafunzi wengine na wafanyakazi wa shule.
- Kushiriki katika shughuli na vilabu vya shule ambavyo wameruhusiwa. Wanafunzi hawapaswi kubaguliwa katika shughuli kwa sababu ya jinsia (isipokuwa kama inavyoruhusiwa chini ya Title IX), rangi, mbari, dini, utaifa, mwelekeo wa kingono, utambulisho wa kijinsia au hali ya kijinsia. Ni wajibu wa wanafunzi kufuata kanuni za shughuli na vilabu vya wanafunzi. Wanafunzi wanapaswa kushirikiana na kuonyesha moyo wa shule.
- Kufuata sheria za mavazi ya shule.
- Kutodhulumiwa, kuitwa majina, kunyanyaswa na kuepuka kushiriki katika tabia kama hizo. Ni wajibu wa wanafunzi kuripoti tabia ya aina hii kwa wafanyakazi wa shule.

***Kumbuka:*** *Ijapokuwa wanafunzi wana haki zilizotajwa hapa juu, haki nyingine zinaweza kubatilishwa katika tukio la ukiukaji wa SCORE?*

## Ukaguzi na Upokonyaji

Ili kulinda afya, usalama, na ustawi wa wanafunzi na wahudumu wa shule, mamlaka ya shule inaweza kuwakagua wanafunzi, makabati ya wanafunzi, madawati ya wanafunzi, na magari yanayoendeshwa shuleni na wanafunzi na/au magari yaliyoegeshwa katika rasilimali ya shule. Wahudumu walioidhinishwa wa shule wanaweza kuwapokonya wanafunzi nyenzo zozote haramu, zisizoidhinishwa, au za magendo ambazo zitagunduliwa katika ukaguzi huo, kulingana na sheria husika.

Makabati na vituo vingine vya kuhifadhia vinavyopatikana kwa wanafunzi ili kutumiwa kwa muda kuhifadhi vitu vyao vya kibinafsi vinasalia kuwa chini ya usimamizi wa wanafunzi na usimamizi wa shule. Usimamizi wa shule una haki ya kukagua makabati, madawati, na vituo vingine vya kuhifadhia kwa vitu ambavyo vinakiuka sheria, sera na masharti ya shule, au ambavyo vinaweza kudhuru shule, wanafunzi wake au watu wengine. Makabati na vituo vingine vya kuhifadhia vinaweza kukaguliwa mara kwa mara kwa sababu yoyote ile, ambao unaweza kutekelezwa wakati wowote ule. Ukaguzi unaweza pia kutekelezwa bila ilani, bila ridhaa ya mwanafunzi, na bila kibali cha utafutaji. Maeneo ya hifadhi ya mtandao wa kompyuta, diski yoyote na/au hifadhi yoyote ya nje, na rekodi za ufikiaji wa Intaneti ya shule zitashughulikiwa kama makabati ya shule. Kwa hivyo, vitu vilivyotajwa hapo vinaweza kukaguliwa kulingana na sera hii.

Huenda usimamizi wa shule ukakagua pia mali ya kibinafsi wakati kuna sababu nzuri ya kuamini kwamba mwanafunzi anamiliki kitu ambacho kinakiuka sheria, na/au sera na masharti ya shule. Mali ya mwanafunzi inajumuisha, lakini haijakomea kwa, vitu ambavyo vinahusishwa na mwanafunzi, vinavyobebwa na mwanafunzi, au kuhifadhiwa na mwanafunzi katika maeneo yaliyotolewa na shule kwa ajili ya mwanafunzi, na yanaweza kujumuisha lakini hayajakomea kwa:, mifuko, mifuko ya vitabu, mifuko ya mkononi, daftari na vitabu.

Usimamizi wa shule pia una haki ya kukagua mali yoyote ya mwanafunzi ikiwa kuna sababu nzuri ya kuamini kwamba mwanafunzi anamiliki kitu ambacho kinakiuka sheria, na/au sera na masharti ya shule. Ukaguzi wa kuvua nguo unaweza kutekelezwa ikihitajika ili kuepuka tishio linalokaribia la kifo au majeraha mabaya ya kimwili kwa mtu yeyote yule.

Ukaguzi wa kuvua nguo, ukihitajika, unaweza kutekeleza tu na afisa wa utekelezaji sheria aliyeapishwa wa jinsia moja kama mtu anayekaguliwa na ukaguzi huo utatekelezwa katika uwepo wa shahidi wa jinsia hiyo moja. Afisa huyo wa kutekeleza sheria aliyeapishwa atashauriana na mwalimu mkuu wa shule na Ofisi ya Usalama na Ulinzi kabla ya kutekeleza ukaguzi huo. Shule za Umma za Richmond hazitahusika katika ukaguzi wa kuvua nguo wa mtu yeyote.

Ofisi ya Usalama na Ulinzi ya Shule za Umma za Richmond imeidhinishwa kutumia vigundua vyuma kusaidia katika ukaguzi kulingana na sheria husika na kanuni za usimamizi. Vigundua vyuma vinaweza pia kutumika bila mpangilio wowote ili kuzuia umiliki wa silaha na vitu vingine haramu na/au hatari.

Ofisi ya Usalama na Ulinzi ya Shule za Umma za Richmond imeidhinishwa pia kutumia, kwa kushirikiana na Idara ya Polisi ya Jiji la Richmond, mbwa wa kusaidia katika kutafuta dawa haramu. Ukaguzi wote unaofanywa na mbwa utatekelezwa kulingana na sheria husika na kanuni za usimamizi za Shule za Umma za Richmond. Ukaguzi unaofanywa na mbwa unaweza kutekelezwa wakati wasimamizi wa shule wanashuku kwamba mwanafunzi anamiliki dawa haramu. Ukaguzi unaofanywa na mbwa unaweza pia kutekelezwa bila mpangilio wowote ili kuzuia umiliki na/au usambazaji wa dawa haramu.

Kamera za usalama zinatumika katika vituo vya shule na kwenye mabasi ya shule ili kukuza usalama na kuhimiza utaratibu unaofaa shuleni, kwenye mali ya shule, katika hafla za shule, na kwenye mabasi ya shule. Mtu yeyote anayeingia katika kituo cha shule, kwenye rasilimali ya shule, katika hafla ya shule, au kupanda basi anaweza kurekodiwa.

Matarajio ya mwanafunzi ya faragha na uhuru wa kutokaguliwa na kupokonywa vitu vyake lazima usawazishwe dhidi ya majukumu ya divisheni ya shule ya kulinda afya, usalama na ustawi wa watu wote katika jamii ya shule, na jukumu lake la kudumisha mazingira salama ya kusoma kwa wanafunzi wote. Ikiwa nyenzo haramu zitapatikana wakati wa ukaguzi, maafisa wa kutekeleza sheria wataarifiwa. Ikiwa nyenzo zisizoidhinishwa au za magendo zitagunduliwa, usimamizi unapaswa kufuata maelekezo yaliyoangaziwa katika viwango vya hatua na majibu.

# MAJIBU KWA TABIA YA WANAFUNZI

SCORE hii inaangazia tabia ambazo zinadhuru mazingira salama na ya upendo ya shule. Tabia hizi zinahitaji walimu na wasimamizi kuchukua hatua zinazofaa ambazo zinapaswa kujumuisha hatua na/au matokeo. Kwa ujumla SCORE hufafanua aina nyingi za tabia zisizofaa, lakini haipaswi kuchukuliwa kama orodha kamili au kama kikomo cha mamlaka ya Bodi ya Shule au maafisa wa shule cha kushughulikia aina nyingi za tabia ambazo zinatatiza utendakazi sahihi wa shule.

## Ni nani Humwarifu Mzazi/Mlezi?

Kwa kila ukiukaji wa SCORE, mwalimu mkuu au mwakilishi wa mwalimu mkuu (mfanyakazi wa RPS) atawaarifu wazazi/walezi wa mwanafunzi' na anaweza kuomba mkutano na wazazi/walezi anapoona mkutano huo unafaa. Neno "mkutano" linajumuisha, lakini halijakomea kwa, mikutano isiyo rasmi na rasmi na mwanafunzi na/au mazungumzo ya simu na wazazi/walezi kuhusu tabia ya mwanafunzi. Mwanafunzi ambaye ameondoshwa shuleni mara tatu au zaidi wakati wa mwaka wa shule wa masomo hatachukuliwa tena hadi mkutano na mwalimu mkuu na wazazi/walezi ufanyike. Isitoshe, ikiwa mwanafunzi ni mwanafunzi aliye na ulemavu na hatua yoyote ya kinidhamu inaweza kusababisha mabadiliko ya kielimu kwa mwanafunzi (sio kimwili), mwalimu mkuu au mwakilishi wake lazima aelekeze mwanafunzi yeyote anayekiuka SCORE kwa timu ya IEP kwa Ukaguzi wa Kuamua Uhusiano wa Tabia na Ulemavu.

*Aya iliyo hapo juu inatumika tu kwa wanafunzi ambao wako chini ya umri wa miaka kumi na minane (18) na/au wanafunzi zaidi ya umri wa miaka 18 ambao wazazi/walezi walitoa hati za kisheria zilizoonyesha kwamba mzazi/mlezi (1) alidumisha udhibiti wa elimu ya mwanafunzi baada ya mwanafunzi kufika umri wa miaka 18 au (2) mzazi/mlezi ana ridhaa ya mwanafunzi mtu mzima ya kupata na/au kupokea maelezo kuhusu rekodi ya nidhamu ya mwanafunzi.*

## Ni Nani Anayependekeza Kuondoshwa kwa Muda Mrefu au Kufukuzwa?

Msimamizi ana mamlaka, aidha kutoka kwa mapendekezo ya mwalimu mkuu au kwa uamuzi wake, kulazimisha au kupendekeza kwa Bodi ya Shule kuondoshwa kwa muda au kufukuzwa kwa mwanafunzi kwa muda wowote ule, inapohitajika na SCORE. Huenda pia msimamizi akapendekeza kuondoshwa kwa muda au kufukuzwa wakati, katika maoni yake, hali za ukiukaji zinafaa matokeo makali zaidi kuliko yaliyosemekana katika SCORE au kulazimishwa na mwalimu mkuu au watu wengine, haijalishi kama ukiukaji huo ni wa kwanza au ni ukiukaji wa kurudia. Kwa maelezo kuhusu kuwatia nidhamu wanafunzi wanaolindwa na Sheria ya Kuboresha Elimu ya Watu walio na Ulemavu ya 2004 (IDEIA) na Sehemu ya 504 ya Sheria ya Urekebishaji Tabia ya 1973 tafadhali rejelea sehemu nyingine za hati hii.

***Kumbuka:*** *Bodi ya Shule ina mamlaka ya mwisho kuhusu masuala yote ya kinidhamu.*

# VIWANGO VYA HATUA NA MAJIBU

## KIWANGO CHA 1

*Majibu ya Kiwango cha 1 yamekusudiwa kuzuia matatizo zaidi ya kitabia huku yakimweka mwanafunzi shuleni.*

- Onyo
- Barua iliyoandikwa ya kutafakari au barua ya kuomba msamaha
- Kupoteza fadhila
- Kubadilishwa mahali pa kukaa
- Simu/barua/mkutano na mzazi/mlezi
- Mkutano wa mwalimu na wanafunzi
- Ushauri
- Laha ya Kufuatilia Maendeleo
- Kufunza upya au Kukuza Tabia Inayohitajika
- Mkutano wa mwalimu na/au usimamizi
- Huduma kwa Jamii (inayofaa ili kurekebisha tabia)
- Kutambua/Kuzawadia Tabia Inayofaa
- Mfumo wa Kuingia na Kutoka
- Kuadhibiwa darasani
- Kuadhibiwa katika mazingira mengine ya darasa
- Kuimarisha tabia zinazofaa
- Mkataba wa tabia darasani/ Fomu ya Kufuatilia Tabia
- Kuelekezwa kwa Mshauri
- Kuelekezwa kwa Afisa wa Kushirikisha Wazazi
- Usimamizi kuchukua vitu haramu
- Urejeshaji
- Utatuzi wa Mzozo/Makundi ya Jamii

## KIWANGO CHA 2

*Majibu na hatua za usimamizi katika kiwango hiki zimeundwa kuzuia matatizo zaidi ya kitabia na kumweka mwanafunzi shuleni. Kulingana na ubaya wa tabia, huenda ikifaa kumwondoa mwanafunzi darasani kwa muda mfupi.*

- Kuwasiliana na Mzazi/Mlezi
- Mfumo wa Kuingia na Kutoka
- Upatanishi wa wanarika
- Kupoteza fadhila
- Kusafisha kampasi/Huduma kwa Jamii
- Kuchukuliwa kwa Vitu
- Mabadiliko ya Ratiba/Darasa
- Kuelekezwa kwa SBIT
- Mkataba wa kitabia (uliotengenezwa na kutiwa saini na mwanafunzi, mzazi/mlezi, na maafisa wa shule)
- Kuelekezwa kwa Huduma za Msaada wa Shule
- Mkutano wa Mwanafunzi
- Mkutano wa Msimamizi/Mwalimu/Mzazi (unajumuisha kufunza upya au tabia inayotarajiwa)
- Mkutano wa Mwalimu na/au Usimamizi
- Kuelekezwa kwa Afisa wa Kushirikisha Familia
- Rasilimali za Jamii
- Kuelekezwa kwa Mshauri
- Mkataba wa tabia wa Shule/Msimamizi
- Kuelekezwa kwa Mtaalamu wa Tabia (shule ya msingi)
- Msaada wa Shuleni na hatua za kinidhamu
- Upatanishi au utatuzi wa mzozo
- Kuelekezwa kwa timu ya Mpango wa Elimu ya Kibinafsi (IEP) (Kwa mwanafunzi wa sasa aliye na IEP)
- Urejeshaji
- Siku Iliyoongezwa ya Shule
- Makundi ya Jamii/Makundi ya Msaada

## KIWANGO CHA 3

*Kulingana na ubaya, hali sugu ya tabia na/au wasiwasi wa kiusalama, tabia za Kiwango cha 3 zinaweza kusababisha mwanafunzi kuondolewa shuleni kwa muda mfupi.*

- Mkataba wa Mzazi/Mwalimu/Msimamizi
- Kupendekeza Mabadiliko ya Ratiba/Darasa
- Kuelekezwa kwa Mtaalamu wa Tabia
- Kuelekezwa/Kupendekezwa kwa Tathmini ya Tabia/Mpango wa Kuingilia Kati Tabia
- Kuelekezwa kwa Huduma za Msaada wa Shule
- Makundi ya Msaada
- Mkutano wa Msimamizi/Mwalimu/Mzazi/Mlezi
- Msaada wa shuleni na hatua za kinidhamu
- Huduma kwa Jamii
- Kuelekezwa kwa kamati ya child find
- Rasilimali za Jamii
- Kuelekezwa kwa Mshauri
- Urejeshaji
- Kuondoshwa shuleni kwa muda mfupi (siku moja hadi tatu kwa wanafunzi wa shule ya msingi/siku moja hadi tano kwa wanafunzi wa shule ya upili) na kuelekezwa kwa kundi la kurekebisha tabia au mkutano baada ya kurudi
- Kuelekezwa kwa watekelezaji sheria ikihitajika
- Kubatilishwa kwa fadhila

## KIWANGO CHA 4

*Tabia nyingine za Kiwango cha 4 zinahitaji ripoti kwa msimamizi au mwakilishi wa msimamizi kama ilivyoangaziwa katika Kanuni ya Virginia § 22.1-279.3:1. Huenda sera ya shule ya ndani ikahitaji ripoti ya ziada. Kuelekezwa kwa msimamizi au mwakilishi wa msimamizi hakusababisha kuondoshwa kwa muda mrefu, kubadilishwa kwa mpango au kufukuzwa moja kwa moja. Baada ya ukaguzi wa tukio kulingana na muktadha, msimamizi au mwakilishi wake anaweza kumrudisha mwanafunzi katika mazingira kamili na msaada wa ziada na/au majibu ya kutekelezwa.*

- Kupendekeza Mabadiliko ya Ratiba/Darasa
- Urejeshaji
- Kuelekezwa kwa Afisa wa Kushirikisha Familia
- Kuelekezwa kwa Mtaalamu wa Tabia
- Kubadilishwa Shule
- Kuelekezwa kwa kamati ya child find
- Tathmini ya tishio kama ilivyoashiriwa na tabia
- Mkataba wa Tabia ya Mzazi-Msimamizi-Mwalimu-Mwanafunzi
- Kubatilishwa kwa fadhila kwa muda mrefu
- Kuelekezwa kwa shule au mpango mbadala ya masomo
- Rasilimali za jamii
- Kuelekezwa kwa watekelezaji sheria ikihitajika
- Kuelekezwa/Kupendekezwa kwa Tathmini ya Tabia/Mpango wa Kuingilia Kati Tabia
- Kuondoshwa shuleni kwa muda mfupi (kwa wanafunzi wa chekechea hadi gredi ya tatu, siku moja hadi tatu, siku nne hadi kumi kwa wanafunzi wa gredi ya nne hadi sita, au siku tano hadi kumi kwa wanafunzi wa gredi ya kumi na mbili)
- Kuondoshwa kwa muda mrefu (siku 11-45) kama ilivyobainishwa na sera ya ndani au na kanuni (siku 11-45 kama ilivyofafanuliwa katika §22.1-276.01)

## KIWANGO CHA 5

*Majibu ya kiwango cha 5 ni ya tabia zile ambazo zinahitaji kuelekezwa kwa msimamizi au mwakilishi wake. Kwa wanafunzi wa chekechea hadi gredi ya tatu, kuondoshwa kokote kwa zaidi ya siku tatu lazima kuelekezwe kwa msimamizi au mwakilishi wake. Kuelekezwa kwa msimamizi au mteuliwa wake hakuwezi kusababisha kufukuzwa, mpango mbadala, kubadilishwa shule, au kuondoshwa kwa muda mrefu moja kwa moja.*

- Kuelekezwa kwa kamati ya child find
- Kubadilishwa Shule
- Mpango Mbadala
- Tathmini ya tishio kama ilivyoashiriwa na tabia
- Kuelekezwa kwa Msimamizi au Mwakilishi wake
- Kuelekezwa kwa rasilimali za jamii (k.m. TDT, FAPT)
- Kuelekezwa kwa watekelezaji sheria ikihitajika
- Mapendekezo ya kufukuzwa
- Kiungo cha Kuondoshwa kwa muda mrefu: (Siku 11-45 kama ilivyofafanuliwa katika §22.1-276.01)
- Rudisha mwanafunzi katika mazingira ya shule na misaada na hatua zinazofaa

Kumbuka: Wanafunzi wa shule ya chekechea - gredi ya 3, viwango vya 2-5 haviwezi kuzidi siku 3 mtawalia kwa kila tukio isipokuwa hali maalum ziwepo, angalia ukurasa wa 27 kwa ufafanuzi zaidi. Mipango ya hatua zitatengenezwa, kupitiwa, na/au kurekebishwa, kwa Viwango vya 3, 4 na 5. Kanuni za Kurejesha Maadili zitatekelezwa kama itakavyoamuliwa na mipango ya kuingilia kati itatengenezwa, kupitiwa, na/au kurekebishwa, kwa wanafunzi ambao wameelekezwa kwa ofisi mara tano (5) au zaidi kwa hatua za kinidhamu katika mwaka wa masomo AU majibizano matatu (3) au zaidi ya kimwili katika mwaka wa masomo. Kanuni za Kurejesha Maadili zinaweza kuwa sehemu ya njia kamili ya shule ya makosa. Kanuni za Kurejesha Maadili zinahusisha kuingilia kati kwa makusudi kwa sehemu ya usimamizi wa shule au timu za usaidizi wa wanafunzi ili kutatua madhara yaliyofanyika. Hii itatuwezesha kufuatilia utiifu na kuhakikisha msaada unatolewa kwa wakosaji wanaorudia na wale ambao ni wajeuri. Katika kubainisha ni matokeo gani ya nidhamu yanayofaa zaidi, yafuatayo yatazingatiwa: a) hali na ubaya wa ukiukaji b) umri wa mwanafunzi na rekodi za awali za kinidhamu c) hali nyingine yoyote muhimu. Kuondoshwa shuleni lazima kuhusishe hatua ya mafunzo na/au kukagua tabia inayotarajiwa ya shule (k.m. Kuondoshwa shuleni kwa siku tatu na kupata ushauri).

# MAJIBU YA KIWANGO CHA SHULE ZA MSINGI KWA TABIA ZA WANAFUNZI

| SBAR | Kategoria A: Tabia ambazo zinazuia maendeleo ya kielimu (BAP) ya mwanafunzi au wanafunzi wengine | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BAP1 | Kutatiza masomo darasani (kuongea, kupiga kelele, tabia isiyofaa darasani, kutokuwa kwenye kiti chako, kumiliki vitu ambavyo vinakengeusha fikira) | X | X | | | | |
| BAP2 | Kutatiza masomo nje ya darasa (kupiga kelele, kukatiza darasa, n.k.) | X | X | | | | |
| BAP3 | Ukosefu wa uaminifu katika elimu (udanganyifu, wizi wa maandishi) | X | | | | | |
| BAP4 | Kuchelewa darasani bila ruhusa | X | | | | | |
| BAP5 | Kuchelewa shuleni bila ruhusa | X | | | | | |

| SBAR | Kategoria B: Tabia zinazohusiana na Shughuli za Shule (BSO) zinatatiza shughuli za kila siku za taratibu za shule | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BSO1 | Kubadilisha hati au rekodi rasmi | X | X | | | | |
| BSO2 | Kutoa taarifa za uongo kwa wafanyakazi | X | X | | | | |
| BSO3 | Kukataa kutii maombi ya wafanyakazi kwa njia ambayo inatatiza shughuli za shule | X | X | X | | | |
| BSO4 | Kushindwa kuwa mahali unapopaswa kuwa | X | X | | | | |
| BSO5 | Kushindwa kuhudhuria mazingira uliyopewa ya kutiwa nidhamu (kizuizi, kuondoshwa kwa muda shuleni, shule ya Jumamosi) | X | X | | | | |
| BSO6 | Kuwaleta watu wasiodhinishwa shuleni au kuwaruhusu watu wasioidhinishwa kuingia katika majengo ya shule | X | X | X | | | |
| BSO7 | Ukiukaji wa Sheria za Mavazi | X | X | | | | |
| BSO8 | Uchezaji Kamari (michezo ya bahati nasibu ya kupata pesa au faida) | X | X | | | | |
| BSO9 | Kumiliki vitu ambavyo havifai shule (mifano ni vifaa vya kuchezea, vitabu, elektroniki) | X | X | | | | |
| BSO10 | Umiliki wa bidhaa zilizoibiwa | X | X | | | | |
| BSO11 | Matumizi yasiyoidhinishwa ya elektroniki za shule au vifaa vingine | X | X | | | | |
| BSO12 | Ukiukaji wa Matumizi Yanayokubalika ya Teknolojia/sera ya intaneti | X | X | | | | |
| BSO13 | Ukiukaji wa sera ya bodi ya shule kuhusu umiliki au matumizi ya vifaa vinavyobebeka vya mawasiliano | X | X | | | | |
| BSO14 | Uharibifu, michoro ya grafiti, au uharibifu mwingine wa mali ya shule au ya kibinafsi | X | X | X | | | |

| SBAR | Kategoria C: Tabia za Mahusiano (RB) zinaunda uhusiano mbaya kati ya wanachama wawili au zaidi wa jamii ya shule (Hakuna madhara ya kimwili yaliyofanyika.) | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| RB1 | Uonevu bila majeraha ya kimwili (Angalia Kiungo:Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) | X | X | | | | |
| RB2 | Maonevu ya mtandaoni (Angalia Kiungo:Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) | X | X | X | | | |
| RB3 | Kuchapisha, kusambaza, kuonyesha, au kushiriki nyenzo au vitabu ambavyo ni vya kukashifu, ikiwemo kutumia njia za kielektroniki kuchapisha nyenzo kama hizo | X | X | | | | |
| RB4 | Kusema au kuandika aidha moja kwa moja au kupitia mawasiliano ya kielektroniki maoni, vidokezo, mapendekezo yanayoamsha hamu ya ngono, au maoni mengine ya kingono. | X | X | | | | |
| RB5 | Kuiba pesa au mali bila kutumia nguvu za kimwili | X | X | | | | |
| RB6 | Kumwongelesha mtu mwingine kwa njia isiyo na adamu na heshima | X | X | | | | |
| RB7 | Kukejeli, kudhihaki, kushiriki katika makabiliano ya maneno, kuchochea vita kwa maneno | X | X | | | | |
| RB8 | Kutumia lugha au ishara chafu au ya matusi (kuapa, semi za chuki, ishara za magenge) | X | X | X | | | |

| SBAR | **Kategoria C: Tabia za Mahusiano (RB) zinaunda uhusiano mbaya kati ya wanachama wawili au zaidi wa jamii ya shule (Hakuna madhara ya kimwili yaliyofanyika).** | **Kiwango cha 1** | **Kiwango cha 2** | **Kiwango cha 3** | **Kiwango cha 4** | **Kiwango cha 5** | **Arifu Watekelezaji wa Sheria** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| RB9 | Kutumia matusi kwa msingi wa mbari, jamii, rangi, asili ya kitaifa, hali ya uraia/uhamiaji, uzani, jinsia, utambulisho wa kijinsia, hali ya kijinsia, mapendeleo ya kingono au ulemavu halisi au unaokisiwa. | X | X | | | | |
| RB10 | Kushindwa kujibu maswali au maombi ya wafanyakazi | X | X | | | | |
| RB11 | Mgusano usiotakikana au usiofaa wa kimwili | X | X | X | | | |

| SBAR | **Kategoria D: Tabia zinazosababisha Wasiwasi wa Usalama (BSC) zinaunda hali zisizo salama kwa wanafunzi, wafanyakazi, na/au wageni wa shule** | **Kiwango cha 1** | **Kiwango cha 2** | **Kiwango cha 3** | **Kiwango cha 4** | **Kiwango cha 5** | **Arifu Watekelezaji wa Sheria** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BSC1 | Pombe: Kumiliki au kunywa pombe (lazima uripoti kwa Ofisi ya Usikilizaji) | X | X | X | | | * |
| BSC2 | Pombe: Kusambaza pombe kwa wanafunzi wengine (lazima uripoti kwa Ofisi ya Usikilizaji) | | X | X | X | | * |
| BSC3 | Dawa za kulevya: Kumiliki vifaa vya dawa za kulevya (lazima uripoti kwa Ofisi ya Usikilizaji) | X | X | X | | | * |
| BSC4 | Dawa za kulevya: Kukiuka sera ya dawa zisizoagizwa na daktari (Za kwenye kaunta) ya bodi ya shule | X | X | X | | | |
| BSC5 | Tumbaku: Kumiliki/Kutumia bidhaa za tumbaku, sigara za elektroniki, vifaa vya kuvuta sigara, bidhaa zinazoiga tumbaku | X | X | X | | | |
| BSC6 | Tabia ya Maonevu bila maumivu ya kimwili ambayo inaendelea baada ya kuingilia kati (Angalia Kiungo:Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) Maonevu ambayo yanasababisha majeraha ya kimwili yanapaswa kuainishwa kama Shambulio. | | | X | X | | |
| BSC7 | Maonevu ya mtandaoni ambayo yanaendelea baada ya kuingilia kati (Angalia Kiungo: Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) Maonevu ya mtandaoni ambayo yanasababisha tishio kwa usalama wa wanafunzi na wafanyakazi yanapaswa kushughulikiwa kwa kiwango cha juu cha kuingilia kati na matokeo. | | | X | X | X | |
| BSC8 | Unyanyasaji: Kurudia kumkera au kumshambulia mwanafunzi au kundi la wanafunzi au wafanyakazi kwa kuunda mazingira ya kutisha au mabaya ya elimu au ya kazi. | X | X | X | | | |
| BSC9 | Basi: Kumvuruga dereva wa basi | X | X | | | | |
| BSC10 | Basi: Kuhatarisha usalama wa wengine kwenye basi | X | X | | | | |
| BSC11 | King'ora cha moto: Kuwasha king'ora cha msiba pasi sababu | | X | X | | | |
| BSC12 | Inayohusiana na Moto: Kumiliki vitu ambavyo vinaweza kuwasha au kusababisha moto au kiwango kikubwa cha moshi | X | X | | | | |
| BSC13 | Kushiriki katika tabia ya uzembe ambayo inasababisha hatari ya majeraha kwako au kwa wengine | X | X | X | | | |
| BSC14 | Vita ambavyo havisababishi majeraha kama ilivyobainishwa na usimamizi wa shule | X | X | | | | |
| BSC15 | Kuchochea au kusababisha usumbufu mkubwa kwa shughuli za shule au usalama wa wafanyakazi na/au wanafunzi | X | X | X | | | |
| BSC16 | Kurusha vitu ambavyo vina uwezo wa kusababisha usumbufu, majeraha, au uharibifu wa rasilimali | X | X | | | | |
| BSC17 | Kumsukuma au kumgonga mwanafunzi bila majeraha yoyote yanayoonekana | X | X | | | | |
| BSC18 | Kuonyeshana sehemu za mwili, tabia chafu au utovu wa adabu kwa umma | X | X | X | | | |
| BSC19 | Mgusano wa kimwili wa kingono - kugusa sehemu za mwili, kuchuna, kukunja nguo, | X | X | X | | | |
| BSC21 | Kunyemelea kama ilivyofafanulia katika Sehemu ya Sheria za Virginia ya18.2-60.3 | | | X | X | | X |
| BSC22 | Kuiba pesa au mali kwa kutumia nguvu za kimwili (Hakuna silaha zilizotumika) | | X | X | X | | |
| BSC24 | Kuondoka majengo ya shule bila ruhusa | X | X | | | | |
| BSC25 | Kuingia bila ruhusa | X | X | | | | |
| BSC26 | Kumiliki vifaa/vitu hatari ambavyo vinaweza kutumiwa kuwaumiza wengine | | X | X | X | X | |
| BSC27 | Silaha: Kumiliki silaha yoyote (kando na bunduki) kama ilivyofafanuliwa na § 18.2-308.1. | | | X | X | X | |

| SBAR | Kategoria E: Tabia ambazo Zinahatarisha Mtu au Watu Wengine (BESO), tabia hizi zinahatarisha afya, usalama, au ustawi wa mwanafunzi au watu wengine katika jamii ya shule. | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BESO1 | Shambulio: Kukusudia kusababisha madhara ya kimwili kwa mtu mwingine | X | X | X | X | | |
| BESO2 | Shambulio: Kusababisha madhara ya kimwili kwa mtu mwingine | | | X | X | X | X |
| BESO3 | Kupigana: Matumizi ya ukatili wa kimwili kati ya wanafunzi au mtu mwingine ambapo kuna majeraha madogo kama ilivyobainishwa na usimamizi wa shule | X | X | X | | | |
| BESO4 | Kuwagonga Wafanyakazi: Matumizi ya nguvu dhidi ya mfanyakazi bila majeraha | X | X | X | X | | |
| BESO5 | Dawa za kulevya: Kumiliki bidhaa zinazodhibitiwa, dawa haramu au dawa sanisi zenye kuleta njozi au dawa zisizoidhinishwa zinazoagizwa na daktari (lazima uripoti kwa Ofisi ya Usikilizaji) | | | X | X | X | * |
| BESO6 | Dawa za kulevya: kuwa chini ya ushawishi wa bidhaa zinazodhibitiwa, dawa haramu, au dawa sanisi zenye kuleta njozi au dawa zisizoidhinishwa zinazoagizwa na daktari | | | X | X | X | X |
| BESO7 | Dawa za kulevya: Kutumia bidhaa zinazodhibitiwa au kutumia dawa haramu au dawa sanisi zenye kuleta njozi au dawa zisizoidhinishwa zinazoagizwa na daktari | | | X | X | X | X |
| BESO9 | Moto: Kujaribu kuwasha, kusaidia katika kuwasha, au kuwasha moto | | X | X | X | | X |
| BESO10 | Tabia Zinazohusiana na Magenge: Kushiriki katika tabia zinazotisha au za hatari ambazo zinahusiana na magenge kama ilivyofafanuliwa katika <u>§18.2-46.1</u> | X | X | X | X | | |
| BESO11 | Udhalilishaji kama ilivyofafanuliwa katika <u>§18.2-56</u> na kunukuliwa katika <u>§ 22.1-279.6.</u> | | X | X | | | |
| BESO12 | Kutishia au kuchochea mzozo, majeraha au madhara kwa mfanyakazi | X | X | X | X | | ** |
| BESO13 | Kutishia au kuchochea mzozo, majeraha, au madhara kwa mwanafunzi mwingine | X | X | X | | | |
| BESO15 | Kutumia silaha yoyote kutishia au kujaribu kujeruhi wafanyakazi wa shule, wanafunzi, au wengine | | | | | X | X |
| BESO16 | Kutumia silaha yoyote kutishia au kujaribu kujeruhi mwanafunzi au watu wengine | | | | | X | X |
| BESO17 | Tishio la bomu - Kutoa tishio la bomu | X | X | X | X | | X |

| SBAR | Kategoria F: Tabia Hatari Zinazoendelea (PD) zilizofafanuliwa katika Sera ya Chaguo la Shule Isiyo salama ya Virginia inayohitajika na sheria ya serikali | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kategoria Ndogo I** | | | | | | | |
| PD1 | Mauaji-Silaha | | | | | X | X |
| PD2 | Mauaji-Silaha Nyingine | | | | | X | X |
| PD3 | Shambulio la Kingono | | | | | X | X |
| PD4 | Jaribio la Shambulio la Kingono | | | | | X | X |
| PD5 | Matumizi ya Bomu | | | | | X | X |
| **Kategoria Ndogo ya II** | | | | | | | |
| PD6 | Shambulio kwa kutumia Bunduki au Silaha | | | | | X | X |
| PD7 | Wizi Halisi au Jaribio | | | | X | X | X |
| PD8 | Utekaji nyara | | | | | X | X |
| PD9 | Kumjeruhi Mtu kwa Nia Mbaya bila kutumia Silaha | | | | | X | X |
| PD10 | Shambulio la Kingono kwa Mwanafunzi | | | | | X | X |
| **Kategoria Ndogo ya III** | | | | | | | |
| PD11 | Umiliki wa Bunduki Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD12 | Umiliki wa Bunduki Kubwa au Ndogo Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD13 | Umiliki wa Silaha Nyingine Yoyote Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD14 | Umiliki wa Bomu Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD15 | Umiliki wa Silaha Nyingine Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD16 | Umiliki wa Dawa na Vitu Vinavyodhibitiwa Kinyume na Sheria kwa Lengo la Kusambaza au Kuuza | | | | | X | X |

* Lazima uripoti kwa watekelezaji sheria ikiwa ni uhalifu.

** Lazima uripoti kwa watekelezaji sheria ikiwa imeandikwa na mwanafunzi hana ulemavu.

# MAJIBU YA KIWANGO CHA SHULE ZA UPILI KWA TABIA ZA WANAFUNZI

| SBAR | Kategoria A: Tabia ambazo zinazuia maendeleo ya kielimu (BAP) ya mwanafunzi au wanafunzi wengine | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BAP1 | Kutatiza masomo darasani (kuongea, kupiga kelele, tabia isiyofaa darasani, kutokuwa kwenye kiti chako, kumiliki vitu ambavyo vinakengeusha fikira) | X | X | | | | |
| BAP2 | Kutatiza masomo nje ya darasa (kupiga kelele, kukatiza darasa, n.k.) | X | X | | | | |
| BAP3 | Ukosefu wa uaminifu katika elimu (udanganyifu, wizi wa maandishi) | X | X | | | | |
| BAP4 | Kuchelewa darasani bila ruhusa | X | X | | | | |
| BAP5 | Kuchelewa shuleni bila ruhusa | X | X | | | | |

| SBAR | Kategoria B: Tabia zinazohusiana na Shughuli za Shule (BSO) zinatatiza shughuli za kila siku za taratibu za shule | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BSO1 | Kubadilisha hati au rekodi rasmi | X | X | | | | |
| BSO2 | Kutoa taarifa za uongo kwa wafanyakazi | X | X | X | | | |
| BSO3 | Kukataa kutii maombi ya wafanyakazi kwa njia ambayo inatatiza shughuli za shule | X | X | X | | | |
| BSO4 | Kushindwa kuwa mahali unapopaswa kuwa kwenye majengo ya shule | X | X | | | | |
| BSO5 | Kushindwa kuhudhuria mazingira uliyopewa ya kutiwa nidhamu (kizuizi, kuondoshwa kwa muda shuleni, shule ya Jumamosi) | X | X | | | | |
| BSO6 | Kuwaleta watu wasiodhinishwa shuleni au kuwaruhusu watu wasioidhinishwa kuingia katika majengo ya shule | X | X | X | | | |
| BSO7 | Ukiukaji wa Sheria za Mavazi | X | X | | | | |
| BSO8 | Uchezaji Kamari (michezo ya bahati nasibu ya kupata pesa au faida) | X | X | | | | |
| BSO9 | Kumiliki vitu ambavyo havifai shule (mifano ni vifaa vya kuchezea, vitabu, elektroniki) | X | X | | | | |
| BSO10 | Umiliki wa bidhaa zilizoibiwa | X | X | | | | |
| BSO11 | Matumizi yasiyoidhinishwa ya elektroniki za shule au vifaa vingine | X | X | | | | |
| BSO12 | Ukiukaji wa Matumizi Yanayokubalika ya Teknolojia/Sera ya Intaneti | X | X | | | | |
| BSO13 | Ukiukaji wa sera ya bodi ya shule kuhusu umiliki au matumizi ya vifaa vinavyobebeka vya mawasiliano | X | X | X | | | |
| BSO14 | Uharibifu, michoro ya grafiti, au uharibifu mwingine wa mali ya shule au ya kibinafsi | X | X | X | | | |

| SBAR | Kategoria C: Tabia za Mahusiano (RB) zinaunda uhusiano mbaya kati ya wanachama wawili au zaidi wa jamii ya shule (Hakuna madhara ya kimwili yaliyofanyika) | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| RB1 | Uonevu bila majeraha ya kimwili (Angalia Kiungo:Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) | X | X | | | | |
| RB2 | Maonevu ya mtandaoni (Angalia Kiungo:Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) | | X | X | | | |
| RB3 | Kuchapisha, kusambaza, kuonyesha, au kushiriki nyenzo au vitabu ambavyo ni vya kukashifu, ikiwemo kutumia njia za kielektroniki kuchapisha nyenzo kama hizo | X | X | X | | | |
| RB4 | Kusema au kuandika aidha moja kwa moja au kupitia mawasiliano ya kielektroniki maoni, vidokezo, mapendekezo yanayoamsha hamu ya ngono, au maoni mengine ya kingono. | X | X | X | | | |
| RB5 | Kuiba pesa au mali bila kutumia nguvu za kimwili | X | X | | | | |
| RB6 | Kumwongelesha mtu mwingine kwa njia isiyo na adamu na heshima | X | X | X | | | |
| RB7 | Kukejeli, kudhihaki, kushiriki katika makabiliano ya maneno, kuchochea vita kwa maneno | X | X | X | | | |

| SBAR | Kategoria C: Tabia za Mahusiano (RB) zinaunda uhusiano mbaya kati ya wanachama wawili au zaidi wa jamii ya shule (Hakuna madhara ya kimwili yaliyofanyika) | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| RB8 | Kutumia lugha au ishara chafu au ya matusi (kuapa, semi za chuki, ishara za magenge) | X | X | X | | | |
| RB9 | Kutumia matusi kwa msingi wa mbari, jamii, rangi, asili ya kitaifa, hali ya uraia/uhamiaji, uzani, jinsia, utambulisho wa kijinsia, hali ya kijinsia, mapendeleo ya kingono au ulemavu halisi au unaokisiwa. | X | X | X | | | |
| RB10 | Kushindwa kujibu maswali au maombi ya wafanyakazi | X | X | X | | | |
| RB11 | Mgusano usiotakikana au usiofaa wa kimwili | X | X | X | | | |

| SBAR | Kategoria D: Tabia zinazosababisha Wasiwasi wa Usalama (BSC) zinaunda hali zisizo salama kwa wanafunzi, wafanyakazi, na/au wageni wa shule | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BSC1 | Pombe: Kumiliki au kunywa pombe (lazima uripoti kwa Ofisi ya Usikilizaji) | X | X | X | | | * |
| BSC2 | Pombe: Kusambaza pombe kwa wanafunzi wengine (lazima uripoti kwa Ofisi ya Usikilizaji) | | X | X | X | | * |
| BSC3 | Dawa za kulevya: Kumiliki vifaa vya dawa za kulevya (lazima uripoti kwa Ofisi ya Usikilizaji) | X | X | X | | | * |
| BSC4 | Dawa za kulevya: Kukiuka sera ya dawa zisizoagizwa na daktari (Za kwenye kaunta) ya bodi ya shule | X | X | X | | | |
| BSC5 | Tumbaku Kumiliki/Kutumia bidhaa za tumbaku, sigara za elektroniki, vifaa vya kuvuta sigara, bidhaa zinazoiga tumbaku | X | X | X | | | |
| BSC6 | Tabia ya Maonevu bila maumivu ya kimwili ambayo inaendelea baada ya kuingilia kati (Angalia Kiungo:Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) Maonevu ambayo yanasababisha majeraha ya kimwili yanapaswa kuainishwa kama Shambulio. | | X | X | X | | |
| BSC7 | Maonevu ya mtandaoni ambayo yanaendelea baada ya kuingilia kati (Angalia Kiungo: Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) Maonevu ya mtandaoni ambayo yanasababisha tishio kwa usalama wa wanafunzi na wafanyakazi yanapaswa kushughulikiwa kwa kiwango cha juu cha kuingilia kati na matokeo. | | | X | X | X | |
| BSC8 | Unyanyasaji: Kurudia kumkera au kumshambulia mwanafunzi au kundi la wanafunzi au wafanyakazi kwa kuunda mazingira ya kutisha au mabaya ya elimu au ya kazi. | X | X | X | X | | |
| BSC9 | Basi: Kumvuruga dereva wa basi | X | X | X | | | |
| BSC10 | Basi: Kuhatarisha usalama wa wengine kwenye basi | X | X | X | | | |
| BSC11 | King'ora cha moto: Kuwasha king'ora cha msiba pasi sababu | | X | X | | | |
| BSC12 | Inayohusiana na Moto: Kumiliki vitu ambavyo vinaweza kuwasha au kusababisha moto au kiwango kikubwa cha moshi | X | X | X | | | |
| BSC13 | Kushiriki katika tabia ya uzembe ambayo inasababisha hatari ya majeraha kwako au kwa wengine | X | X | X | | | |
| BSC14 | Vita ambavyo havisababishi majeraha kama ilivyobainishwa na usimamizi wa shule | X | X | | | | |
| BSC15 | Kuchochea au kusababisha usumbufu mkubwa kwa shughuli za shule au usalama wa wafanyakazi na/au wanafunzi | | X | X | X | X | |
| BSC16 | Kurusha vitu ambavyo vina uwezo wa kusababisha usumbufu, majeraha, au uharibifu wa rasilimali | X | X | X | | | |
| BSC17 | Kumsukuma au kumgonga mwanafunzi bila majeraha yoyote yanayoonekana | X | X | | | | |
| BSC18 | Kuonyeshana sehemu za mwili, tabia chafu au utovu wa adabu kwa umma | X | X | X | X | | |
| BSC19 | Mgusano wa kimwili wa kingono - kugusa sehemu za mwili, kuchuna, kukunja nguo, | X | X | X | X | | |
| BSC21 | Kunyemelea kama ilivyofafanulia katika Sehemu ya Sheria za Virginia ya18.2-60.3 | | | | X | X | X |
| BSC22 | Kuiba pesa au mali kwa kutumia nguvu za kimwili (Hakuna silaha zilizotumika) | X | X | X | | | |
| BSC24 | Kuondoka majengo ya shule bila ruhusa | X | X | | | | |
| BSC25 | Kuingia bila ruhusa | | X | X | X | | |
| BSC26 | Kumiliki vifaa/vitu hatari ambavyo vinaweza kutumiwa kuwaumiza wengine | | X | X | X | | |
| BSC27 | Silaha: Kumiliki au kuuza silaha yoyote (bila kujumuisha bunduki) kama ilivyofafanuliwa na sera ya bodi ya shule | | | | X | X | X |

| SBAR | Kategoria E: Tabia ambazo Zinahatarisha Mtu au Watu Wengine (BESO). Tabia hizi zinahatarisha afya, usalama, au ustawi wa mwanafunzi au watu wengine katika jamii ya shule. | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| BESO1 | Shambulio: Kukusudia kusababisha madhara ya kimwili kwa mtu mwingine | | X | X | X | | |
| BESO2 | Shambulio: Kusababisha madhara ya kimwili kwa mtu mwingine | | | X | X | X | X |
| BESO3 | Kupigana: Matumizi ya ukatili wa kimwili kati ya wanafunzi au mtu mwingine ambapo kuna majeraha madogo kama ilivyobainishwa na usimamizi wa shule | X | X | X | | | |
| BESO4 | Kuwagonga Wafanyakazi: Matumizi ya nguvu dhidi ya mfanyakazi bila majeraha | | | X | X | X | X |
| BESO5 | Dawa za kulevya: Kumiliki bidhaa zinazodhibitiwa, dawa haramu au dawa sanisi zenye kuleta njozi au dawa zisizoidhinishwa zinazoagizwa na daktari (lazima uripoti kwa Ofisi ya Usikilizaji) | | | X | X | X | * |
| BESO6 | Dawa za kulevya: kuwa chini ya ushawishi wa bidhaa zinazodhibitiwa, dawa haramu, au dawa sanisi zenye kuleta njozi au dawa zisizoidhinishwa zinazoagizwa na daktari | | | | X | X | |
| BESO7 | Dawa za kulevya: Kutumia bidhaa zinazodhibitiwa au kutumia dawa haramu au dawa sanisi zenye kuleta njozi au dawa zisizoidhinishwa zinazoagizwa na daktari | | | | X | X | X |
| BESO9 | Moto: Kujaribu kuwasha, kusaidia katika kuwasha, au kuwasha moto | | | X | X | X | X |
| BESO10 | Tabia Zinazohusiana na Magenge: Kushiriki katika tabia zinazotisha au za hatari ambazo zinahusiana na magenge kama ilivyofafanuliwa katika §18.2-46.1 | | | X | X | X | |
| BESO11 | Udhalilishaji kama ilivyofafanuliwa katika §18.2-56 na kunukuliwa katika § 22.1-279.6. | | | | | X | |
| BESO12 | Kutishia au kuchochea mzozo, majeraha au madhara kwa mfanyakazi | | X | X | X | X | ** |
| BESO13 | Kutishia au kuchochea mzozo, majeraha, au madhara kwa mwanafunzi mwingine | | X | X | X | X | |
| BESO15 | Kutumia silaha yoyote kutishia au kujaribu kujeruhi mfanyakazi wa shule | | | | | X | X |
| BESO16 | Kutumia silaha yoyote kutishia au kujaribu kujeruhi mwanafunzi au watu wengine | | | | | X | X |
| BESO17 | Tishio la bomu - Kutoa tishio la bomu | | | | X | X | X |

| SBAR | Kategoria F: Tabia Hatari Zinazoendelea (PD) zilizofafanuliwa katika Sera ya Chaguo la Shule Isiyo salama ya Virginia inayohitajika na sheria ya serikali | Kiwango cha 1 | Kiwango cha 2 | Kiwango cha 3 | Kiwango cha 4 | Kiwango cha 5 | Arifu Watekelezaji wa Sheria |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Kategoria Ndogo I** | | | | | | | |
| PD1 | Mauaji-Silaha | | | | | X | X |
| PD2 | Mauaji-Silaha Nyingine | | | | | X | X |
| PD3 | Shambulio la Kingono | | | | | X | X |
| PD4 | Jaribio la Shambulio la Kingono | | | | | X | X |
| PD5 | Matumizi ya Bomu | | | | | X | X |
| **Kategoria Ndogo ya II** | | | | | | | |
| PD6 | Shambulio kwa kutumia Bunduki au Silaha | | | | | X | X |
| PD7 | Wizi Halisi au Jaribio | | | | X | X | X |
| PD8 | Utekaji nyara | | | | | X | X |
| PD9 | Kumjeruhi Mtu kwa Nia Mbaya bila kutumia Silaha | | | | | X | X |
| PD10 | Shambulio la Kingono kwa Mwanafunzi | | | | | X | X |
| **Kategoria Ndogo ya III** | | | | | | | |
| PD11 | Umiliki wa Bunduki Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD12 | Umiliki wa Bunduki Kubwa au Ndogo Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD13 | Umiliki wa Silaha Nyingine Yoyote Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD14 | Umiliki wa Bomu Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD15 | Umiliki wa Silaha Nyingine Kinyume na Sheria | | | | | X | X |
| PD16 | Umiliki wa Dawa na Vitu Vinavyodhibitiwa Kinyume na Sheria kwa Lengo la Kusambaza au Kuuza | | | | | X | X |

* Lazima uripoti kwa watekelezaji sheria ikiwa ni uhalifu.

** Lazima uripoti kwa watekelezaji sheria ikiwa imeandikwa na mwanafunzi hana ulemavu.

# TABIA ZA WANAFUNZI

Tafadhali fahamu kwamba kulingana na sheria za Virginia na/au sera za Bodi ya Shule ya Shule za Umma za Richmond, ukiukaji wa kanuni zingine za maadili mema unahitaji kwamba mwanafunzi apendekezwe kufukuzwa kutoka kwa Shule za Umma za Richmond.

### Kategoria A: Tabia ambazo Zinazuia Maendeleo ya Kielimu (BAP) ya mwanafunzi au wanafunzi wengine

- Kutatiza masomo darasani (kuongea, kupiga kelele, tabia isiyofaa darasani, kutokuwa kwenye kiti chako, kumiliki vitu ambavyo vinakengeusha fikira)
- Kutatiza masomo nje ya darasa (kupiga kelele, kukatiza darasa, n.k.)
- Ukosefu wa uaminifu katika elimu (udanganyifu, wizi wa maandishi)
- Kuchelewa darasani bila ruhusa
- Kuchelewa shuleni bila ruhusa

**Kuchelewa darasani na/au shuleni bila ruhusa**

Wanafunzi wanaowasili baada ya siku ya shule kuanza watachukuliwa kuwa wamechelewa. Wanafunzi hawapaswi kuchelewa shuleni au darasani bila ufafanuzi ulioandikwa au taarifa ya maneno kutoka kwa wazazi/walezi, walimu au wasimamizi.

Lazima mwanafunzi awahi kwa wakati na ahudhurie masomo yote aliyopewa. Mahudhurio ya mwanafunzi ni juhudi ya pamoja na shule itahusisha wazazi/walezi na mwanafunzi katika kukubali uwajibikaji wa mahudhurio ya mara kwa mara. Kila mzazi/mlezi wa mtoto ambaye yuko katika umri wa kuhudhuria shule kwa lazima atawajibika kwa mtoto huyo kama inavyohitajika kisheria. Wanafunzi watahudhuria shule mara kwa mara na watawahi kwa wakati isipokuwa kuwe na ruhusa kulingana na sera ya bodi ya shule. Wanafunzi hawatakosa au kuchelewa shuleni. Wanafunzi nao hawatatoka shuleni kabla ya mwisho wa siku ya masomo bila ruhusa ya mzazi, ruhusu ya shule au udhuru wowote mwingine halali. Kutokuwepo bila ruhusa kutajumuisha, lakini hakutakomea kwa, kuondoka kwenye majengo ya shule bila idhini.

### Kategoria B: Tabia zinazohusiana na Shughuli za Shule (BSO) Zinatatiza shughuli za kila siku za taratibu za shule

- Kubadilisha hati au rekodi rasmi
- Kutoa taarifa za uongo kwa wafanyakazi
- Kukataa kutii maombi ya wafanyakazi kwa njia ambayo inatatiza shughuli za shule
- Kushindwa kuwa mahali unapopaswa kuwa kwenye majengo ya shule
- Kushindwa kuhudhuria mazingira uliyopewa ya kutiwa nidhamu (kizuizi, kuondoshwa kwa muda shuleni, shule ya Jumamosi)
- Kuwaleta watu wasiodhinishwa shuleni au kuwaruhusu watu wasioidhinishwa kuingia katika majengo ya shule
- Ukiukaji wa Sheria za Mavazi
- Uchezaji Kamari (michezo ya bahati nasibu ya kupata pesa au faida)
- Matumizi yasiyoidhinishwa ya elektroniki za shule au vifaa vingine
- Ukiukaji wa Matumizi Yanayokubalika ya Teknolojia/sera ya intaneti
- Ukiukaji wa sera ya bodi ya shule kuhusu umiliki au matumizi ya vifaa vinavyobebeka vya mawasiliano
- Uharibifu, michoro ya grafiti, au uharibifu mwingine wa mali ya shule au ya kibinafsi

## Kubadilisha hati au rekodi rasmi/Kutoa taarifa za uongo kwa wafanyakazi

Wanafunzi hawapaswi kudanganya, kuiba maandishi au kutoa taarifa za uongo kwa kujua zinazohusiana na kazi au mitihani yoyote.

Kulingana na ubaya wa ukiukaji, huenda mwanafunzi asipokee sifa za kazi, kozi hiyo mahsusi, au pengine anaweza kuondoshwa kwa muda shuleni. Mwanafunzi anayepatikana akitumia simu ya mkononi wakati wa mtihani atanyanganywa kifaa hicho mara moja na atapoteza haki ya kutumia vifaa hivyo kwa muda uliosalia wa mwaka wa masomo. Huenda matokeo ya mtihani yakabatilishwa katika hali hii.

## Kukataa kutii maombi ya wafanyakazi kwa njia ambayo inatatiza shughuli za shule

Wanafunzi hawatakiuka maagizo yoyote ya maneno au yaliyoandikwa yaliyotolewa na wafanyakazi wa shule katika mawanda ya mamlaka yao.

Wanafunzi wana haki ya mazingira ya masomo ambayo hayana usumbufu wowote. Usumbufu wowote wa kimwili au wa maneno katika mazingira ya shule au wakati wa shughuli husika, ambao unatatiza au kuingilia mafunzo au taratibu za shughuli za shule, umepigwa marufuku. Wanafunzi hawatahusika katika tabia ambayo, au imekusudiwa, kutatiza shughuli, kazi au mchakato wowote wa shule au inayohatarisha afya au usalama wa wanafunzi na watu wengine.

Wanafunzi hawatacheza au kushiriki katika mchezo wowote ambao matokeo yake si dhahiri au wa bahati nasibu wa kupata pesa au vitu vingine vya dhamana kwenye rasilimali ya shule au wakati wa shughuli yoyote inayohusiana na shule.

***Kumbuka:*** *Hii haihusishi shughuli zinazofadhaliwa na kuidhinishwa na shule.*

## Ukiukaji wa Sheria za Mavazi

Sheria za mavazi zitatumika kuwasaidia wanafunzi wote kukuza mtazamo mwema wa kimwili, na mazingira fanisi ya elimu. Hatua zozote za kutekeleza sheria za mavazi zinapaswa kupunguza upotezaji unaowezekana wa saa za masomo. Usimamizi na utekelezaji wa sheria za mavazi utakuwa mmoja katika mili ya wanafunzi, haijalishi utambulisho halisi au unaokisiwa wa kijinsia au mapendeleo ya kingono, hali ya kijinsia, mbari, jamii na ukubwa na/au aina ya mwili. Isipokuwa katika hali ambazo shule zinahitaji sare, huenda shule zisitekeleze sera zenye vikwazo nyingi au sheria kali za mavazi.

Mavazi na mwonekano wa mwanafunzi haupaswi kuwa huna adabu, au unaosababisha, matatizo ya afya na/au usalama katika mazingira ya elimu.

**LAZIMA wanafunzi wavae:**

- Nguo za Juu na Chini, au sawa na hizo (marinda, n.k..)
- Viatu (champali haziruhusiwi, lakini lazima viatu vinavyofaa vya riadha vivaliwe wakati wa somo la PE na tahadhari ya ziada inapaswa kuzingatiwa kwa wanafunzi wakati wa mapumziko). ***Bodi ya Shule ya jiji la Richmond na/au Shule za Umma za Richmond haziwajibiki kwa majeraha yoyote ambayo yanaweza kufanyika kwa sababu ya wanafunzi kuvaa viatu visivyofaa.*
- Nguo zinazofunika sehemu nyeti, makalio na chuchu kwa nyenzo zisizopenyeza nuru

**Wanafunzi WANAWEZA kuvaa:**

- Mavazi yenye nembo za kibiashara au riadha
- Suruali zinazobana (suruali za yoga, soksi ndefu, na jinzi zinazobana)
- Jinzi zilizoraruka bila nguo za ndani kuonekana
- Wanafunzi wanaovaa mavazi ambayo hayalingani na jinsia inayokisiwa ya mwanafunzi sio ukiukaji

**Wanafunzi HAWAWEZI kuvaa:**

- Nguo ya ndani inayoonekana au mavazi ya kuogelea yenye muundo huo
- Mavazi yanayotumia picha au lugha inayoonyesha matumizi ya dawa za kulevya, shughuli zozote zisizo halali, vitisho, au kauli mbio za ubaguzi
- Mavazi ambayo yanahusisha semi za chuki, uchafu au ponografia
- Picha na/au lugha ambayo inaunda mazingira mabaya au ya kutisha ya elimu kwa msingi wa utambulisho au tabaka
- Kofia, skafu, tepe za kupanguzia jasho, bandana, barakoa za uso, au vifunika kichwa katika majengo ya shule isipokuwa a.) wakati zinavaliwa kwa sababu ya imani za kidini, b.) wakati zinavaliwa kwa sababu za kiafya au usalama, c.) wakati zinavaliwa kuhusiana na mpango unaofadhiliwa na shule *Barakoa za uso zinaweza kuvaliwa kulingana na hali kama vile COVID 19, matibabu, n.k.

## Matokeo yanayopendekezwa ya Kukiuka Sheria za Mavazi

Usimamizi wa shule unapaswa kupunguza kupoteza saa za masomo, na kuepuka kuwaita wazazi/walezi isipokuwa taarifa iwe inahitajika ili kuwaletea wanafunzi mavazi yanayofaa. La sivyo, usimamizi wa shule unapaswa kuarifu wazazi kuhusu ukiukaji wa sheria za mavazi baada ya siku ya shule imeisha. Hakuna mwanafunzi anayepaswa kulinganishwa, kuabishwa au kufanywa abadiishe nguo mbele ya darasa kwa sababu ya mavazi aliyoyavaa.

**Upili**

- **Kosa la 1**– Onyo na nafasi ya kubadilisha nguo ili kusahihisha ukiukaji wa sheria za mavazi;
- **Kosa la 2**– Onyo la pili na nafasi ya kubadilisha nguo ili kusahihisha ukiukaji wa sheria za mavazi;
- **Kosa la 3** – Kizuizi cha baada ya shule au kizuizi cha Jumamosi

*** Makosa yanayoendelea yatasababisha matokeo ya ziada.*

## Ukiukaji wa Matumizi Yanayokubalika ya Teknolojia/Sera ya Intaneti

Wanafunzi wa Shule za Umma za Richmond wanapewa ufikiaji wa mtandao wa kompyuta wa mfumo wa shule kwa ajili ya barua ya intaneti na ya elektroniki (barua pepe). Intaneti na barua pepe ni mitandao ya kiulimwengu. Kupitia mitandao hii, wanafunzi wanaweza kufikia maelfu ya maktaba, hifadhidata na tovuti za elimu, na wanaweza kubadilishana ujumbe na watumiaji wa intaneti duniani kote.

Wanafunzi wanawajibika kwa tabia zao kwenye mtandao wa kompyuta wa shule kama vile wanavyowajibika darasani. SCORE hii inatumika kwa matumizi yote ya mtandao wa kompyuta ya shule.

Mtandao umetolewa kwa wanafunzi kutekeleza utafiti na kuwasiliana na wengine kwa malengo ya kielimu pekee. Ufikiaji wa huduma za mtandao utatolewa kwa wanafunzi wanaotii sheria za matumizi yanayofaa.

Watumiaji wa mtandao wa kompyuta wa mfumo wa shule wanawajibika kwa tabia zao na mawasiliano yao kwenye mtandao huo.

Maeneo ya kuhifadhi mtandao, diski na/au hifadhi za nje zinazotumiwa pamoja na intaneti zitashughulikiwa kama makabati ya shule. Huenda wasimamizi wa mtandao wakakagua faili na mawasiliano ili kudumisha uadilifu wa mfumo na kuhakikisha wanafunzi wanatumia mfumo ipasavyo. Matumizi yafuatayo ya Intaneti yamepigwa marufuku:

- Kufikia, kutuma, au kuonyesha ujumbe, picha zinazokera, au lugha chafu na ya matusi
- Kutuma au kupokea ujumbe dhahiri wa kingono (ujumbe mchafu)
- Maonevu ya mtandaoni
- Kutuma ujumbe mfupi
- Kuharibu mitandao ya kompyuta
- Kukiuka sheria za hakimiliki
- Kutumia utambulisho au nenosiri la mtu mwingine, au kuingia katika kazi ya mtu mwingine bila ruhusa
- Kutumia mtandao kwa shughuli zozote zisizo halali kama ilivyofafanuliwa na sheria za jimbo au serikali
- Kuingia bila ruhusa

Mtalaa wa Usalama wa Intaneti wa RPS unatekelezwa katika shule zote. Masomo na shughuli zimejumuishwa katika maeneo yote ya masomo. Vidokezo vya usalama vya Intaneti na Sera za Matumizi Yanayokubalika yamechapishwa kwenye tovuti yetu.

Ikiwa itabainika kwamba matumizi ya teknolojia, na/au mitandao ya kijamii kwenye au nje ya rasilimali ya shule, yalisababisha usumbufu shuleni, shule ina mamlaka ya kumtia nidhamu mwanafunzi.

**Maonevu ya mtandaoni:** Maonevu ya mtandaoni yanaweza kujumuisha kutuma ujumbe wa ukatili au wa kutisha kwa akaunti za barua pepe za shule za mwanafunzi au kuchapisha uvumi, vitisho au maoni mabaya kuhusu wanarika mtandaoni. Shule zina mamlaka ya kuwatia nidhamu wanafunzi kwa matumizi mabaya ya kompyuta za mfumo wa shule, barua pepe na huduma za intaneti. Shule pia zina mamlaka za kuwatia nidhamu wanafunzi kwa shughuli za barua pepe au Intaneti ambazo ziko nje ya majengo ya shule na bila kutumia vifaa vya shule ikiwa tabia hiyo ilisababisha usumbufu mkubwa kwa mazingira ya shule.

## Ukiukaji wa sera ya bodi ya shule kuhusu umiliki au matumizi ya vifaa vinavyobebeka vya mawasiliano

Matumizi ya mwanafunzi ya aina yoyote ya kifaa kisichoidhinishwa cha elektroniki au cha mitambo ambacho si sehemu ya mpango wa mafunzo yamepigwa marufuku wakati wa saa za masomo. Kurekodi video na/au sauti ya wafanyakazi na/au wanafunzi wakati wa siku ya masomo au shughuli inayofadhiliwa na shule kumepigwa marufuku. Hii itajumuisha, lakini hazitakomea kwa: simu za mkononi, vifaa vinavyobebeka vya muziki, vielekezi vya leza; kamera, kompyuta za vipakatalishi, vichezaji MP3, iPod, vichezaji DVD vinavyobebeka, TV zinazobebeka, saa mahiri, n.k. Mwanafunzi ataruhusiwa kutumia simu za mkononi kwenye majengo ya shule au katika shughuli zilizofadhiliwa na shule kabla na baada ya saa za kawaida za masomo. Hata hivyo, lazima matumizi ya simu za mkononi zisitatize shughuli yoyote ya baada ya shule.

## Wanafunzi wa Pre-K na wa Shule ya Msingi (Pre-K – Gredi ya 5):

Simu za mkononi zimepigwa marufuku wakati wa saa za masomo, katika matukio yanayofadhiliwa na shule na kwenye basi. Wanafunzi wanaruhusiwa kuwa na simu za mkononi; hata hivyo, lazima simu hiyo iwe imezimwa na kuwekwa mbali.

## Wanafunzi wa Upili (Gredi ya 6 – 12):

Wanafunzi wanaweza kutumia simu za mkononi kwa wakati uliotengwa na kulingana na vigezo vilivyobainishwa katika sehemu ifuatayo:

Huenda wanafunzi wa upili wakatumia simu zao za mkononi wakiwa kwenye basi la shule kwa kutumia vifaa vya masikio vya kibinafsi ii wasiwasumbie wengine. Wanafunzi wa upili wanaweza kuwa na simu za mkononi. Hata hivyo, lazima simu hizo zizimwe na kuwekwa mbali baada ya kengele ya kwanza au nyingine kama hiyo inayoashiria kuanza kwa siku ya masomo. Lazima simu hizo zisalie zimezimwa hadi kengele ya mwisho au nyingine kama hiyo inayoashiria mwisho wa siku ya masomo.

Wanafunzi wanaweza kutumia simu zao, na vifaa vya kibinafsi vya kusikiliza, baada ya masomo na matukio yanayofadhiliwa na shule ilimradi hawatatizi tukio ambalo linaendelea.

## Matokeo ya ukiukaji wa simu za mkononi PK – Gredi ya 12:

Kifaa chochote kilichopigwa marufuku kinaweza kuchukuliwa na usimamizi wa shule na kurejeshwa kwa mzazi/mlezi kwa wakati unaofaa mwalimu mkuu na mzazi/mlezi (tarehe zinazotolewa na shule zitakuwa ndani ya siku 10 za shule za kifaa hicho kuchukuliwa). Ikiwa itabainika kwamba kifaa cha mawasiliano kilichotumika kwenye au nje ya majengo ya shule kilisababisha usumbufu shuleni, shule ina mamlaka ya kumtia nidhamu mwanafunzi kulingana na SCORE.

- **Kosa la 1:** Simu hiyo ya mkononi itachukuliwa na msimamizi/mwakilishi wa msimamizi na kurejeshwa kwa mwanafunzi mwisho wa siku.
- **Kosa la 2:** Simu hiyo ya mkononi itachukuliwa na msimamizi/mwakilishi wa msimamizi na kurejeshwa kwa mzazi/mlezi siku na saa iliyotengwa inayofaa msimamizi na mzazi (tarehe zinazotolewa na shule zitakuwa ndani ya siku 10 za shule).
- **Kosa la 3:** Haki za simu ya mkononi za mwanafunzi zitapigwa marufuku kwa muda uliosalia wa mwaka wa masomo.

****Shule Mbadala ya Richmond:** Mwanafunzi kumiliki shule za mkononi katika Shule Mbadala ya Richmond (mpango mbadala) umepigwa marufuku.

Shule za Umma za Richmond hazitawajiba kwa kupotea, kuharibika au kuibiwa kwa bidhaa zilizochukuliwa. Vifaa vilivyopotea au kuibiwa vya elektroniki ni suala la usimamizi na/au kiraia. Mwanafunzi anayepatikana akitumia simu ya mkononi wakati wa mtihani atanyanganywa kifaa hicho mara moja na atapoteza haki ya kutumia simu yake ya mkononi kwa muda uliosalia wa mwaka wa masomo. Isitoshe, huenda matokeo ya mtihani yakabatilishwa katika hali hii.

***Kumbuka:*** *Ukiukaji wa kanuni za simu za mkononi ambao unajumuisha pia ukiukaji mwingine wa SCORE unaweza kusababisha matokeo/hatua za ziada na/au kali zaidi. Mwishowe, kama ilivyobainishwa kwenye ukurasa wa 9 wa hati hii, katika kubainisha ni matokeo gani ya nidhamu yanayofaa zaidi, yafuatayo yatazingatiwa: a) hali na ubaya wa ukiukaji b) umri wa mwanafunzi na rekodi za awali za kinidhamu c) hali nyingine yoyote muhimu.*

## Matumizi Yasiyoidhinishwa ya Elektroniki za Shule au Vifaa Vingine

Wanafunzi hawatamiliki bidhaa za magendo kwenye majengo ya shule, katika kituo chochote cha mabasi ya shule, au katika shughuli yoyote inayofadhiliwa na shule. Bidhaa za magendo zinajumuisha bidhaa yoyote ambayo haifai katika mazingira ya shule na/au inayotatiza, au kuingiliana na mchakato wa elimu. Bidhaa hizi zinajumuisha, lakini hazijakomea kwa: viberiti, viwashiaji, michezo ya kompyuta ya mkononi, vielelezi vya leza, na kadi za michezo. Bidhaa za magendo zinaweza pia kujumuisha kompyuta za vipakatalishi ikiwa kompyuta hizo hazitumiwi kwa malengo yaliyoidinishwa ya kielimu.

Shule za Umma za Richmond na shule binafsi za wanafunzi hazitawajibika katika hali yoyote ile kwa hasara/uharibifu/ au wizi wa bidhaa ambazo zimechukuliwa kwa sababu ya ukiukaji wa kiwango hiki. Vitabu au nyenzo zozote zilizochukuliwa ambazo zinakiuka sheria zitawasilishwa kwa mamlaka ya kisheria.

Wanafunzi hawataharibu kwa makusudi jengo lolote la shule au mali yoyote inayomilikiwa au kudhibitiwa na Bodi ya Shule au mali ya mtu mwingine yeyote.

## Uharibifu, michoro ya Grafiti, au uharibifu mwingine wa mali ya shule au ya kibinafsi

Wanafunzi hawataharibu kwa makusudi jengo lolote la shule au mali yoyote inayomilikiwa au kudhibitiwa na Bodi ya Shule au mali ya mtu mwingine yeyote.

### Kategoria C: Tabia za Mahusiano (RB) zinaunda uhusiano mbaya kati ya wanachama 2 au zaidi wa jamii ya shule (Hakuna madhara ya kimwili yaliyofanyika)

- Uonevu bila majeraha ya kimwili (Angalia Kiungo:Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia)
- Maonevu ya mtandaoni (Angalia Kiungo:Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia)
- Kuchapisha, kusambaza, kuonyesha, au kushiriki nyenzo au vitabu ambavyo ni vya kukashifu, ikiwemo kutumia njia za kielektroniki kuchapisha nyenzo kama hizo
- Kusema au kuandika aidha moja kwa moja au kupitia mawasiliano ya kielektroniki maoni, vidokezo, mapendekezo yanayoamsha hamu ya ngono, au maoni mengine ya kingono.
- Kumwongelesha mtu mwingine kwa njia isiyo na adamu na heshima
- Kukejeli, kudhihaki, kushiriki katika makabiliano ya maneno, kuchochea vita kwa maneno
- Kutumia lugha au ishara chafu au ya matusi (kuapa, semi za chuki, ishara za magenge)
- Kutumia matusi kwa msingi wa mbari, jamii, rangi, asili ya kitaifa, hali ya uraia/uhamiaji, uzani, jinsia, utambulisho wa kijinsia, hali ya kijinsia, mapendeleo ya kingono au ulemavu halisi au unaokisiwa.
- Kushindwa kujibu maswali au maombi ya wafanyakazi
- Mgusano usiofaa wa kimwili ambao ni wa kingono au unaokiuka kanuni za shule kuhusu mgusano

Mwanafunzi yeyote aliyeshutumiwa kwa maonevu, na ambaye kuna ushahidi wa kutosha wa maonevu kama hayo, anaweza kuwekwa katika shule nyingine kulingana na Sera ya Bodi ya Shule ya 8.2.5 na 8-3. 14 kwa kuongezea hatua yoyote ya kinidhamu ambayo inaweza kutekelezwa na Divisheni ya Shule. Ushahidi unaoaminika wa maonevu unajumuisha, lakini hujakomea kwa: malalamishi yaliyowasilishwa kutoka kwa mhadhiriwa kwa wafanyakazi wa shule na/au usimamizi kuhusu matukio kati ya mwanafunzi anayehusika katika maonevu na mwanafunzi ambaye ni mhasiriwa wa maonevu, mashtaka ya jinai yaliyowasilishwa dhidi ya mwanafunzi anayeshutumiwa kwa maonevu na mwanafunzi na/au wazazi wa mwanafunzi ambaye amekuwa mhasiriwa wa maonevu, na/au hatia ya jinai ya mwanafunzi anayeshutumiwa kwa kumshambulia mwanafunzi ambaye amekuwa mhasiriwa wa maonevu.

Wanafunzi hawatamiliki, kuonyesha au kusambaza vitabu, nyenzo, vielelezo, na/au picha chafu.

Shule za Umma za Richmond na shule binafsi za wanafunzi hazitawajibika katika hali yoyote ile kwa hasara/uharibifu/ au wizi wa bidhaa ambazo zimechukuliwa kwa sababu ya ukiukaji wa kiwango hiki. Vitabu au nyenzo zozote zilizochukuliwa ambazo zinakiuka sheria zitawasilishwa kwa mamlaka ya kisheria.

## Kutumia lugha au ishara chafu au za matusi

Wanafunzi hawatatumia lugha chafu au ya matusi, ishara chafu, au kushiriki katika tabia chafu.

### Kategoria D: Tabia zinazosababisha Wasiwasi wa Usalama (BSC) zinaunda hali zisizo salama kwa wanafunzi, wafanyakazi, na/au wageni wa shule

- Pombe: Kumiliki au kutumia pombe
- Pombe: Kusambaza pombe kwa wanafunzi wengine
- Dawa za kulevya: Kumiliki vifaa vya dawa za kulevya
- Dawa za kulevya: Kukiuka sera ya dawa zisizoagizwa na daktari (Za kwenye kaunta) ya bodi ya shule
- Tumbaku Kumiliki/Kutumia bidhaa za tumbaku, sigara za elektroniki, vifaa vya kuvuta sigara, bidhaa zinazoiga tumbaku
- Tabia ya Maonevu bila maumivu ya kimwili ambayo inaendelea baada ya kuingilia kati (Angalia Kiungo:Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) Maonevu ambayo yanasababisha majeraha ya kimwili yanapaswa kuainishwa kama Shambulio.
- Maonevu ya mtandaoni ambayo yanaendelea baada ya kuingilia kati (Angalia Kiungo: Kielelezo cha Sera ya Kushughulikia Maonevu katika Shule za Umma za Virginia) Maonevu ya mtandaoni ambayo yanasababisha tishio kwa usalama wa wanafunzi na wafanyakazi yanapaswa kushughulikiwa kwa kiwango cha juu cha kuingilia kati na matokeo.
- Basi: Kumvuruga dereva wa basi
- Basi: Kuhatarisha usalama wa wengine kwenye basi
- King’ora cha moto: Kuwasha king’ora cha msiba pasi sababu
- Inayohusiana na Moto: Kumiliki vitu ambavyo vinaweza kuwasha au kusababisha moto au kiwango kikubwa cha moshi
- Kushiriki katika tabia ya uzembe ambayo inasababisha hatari ya majeraha kwako au kwa wengine
- Kuchochea au kusababisha usumbufu mkubwa kwa shughuli za shule au usalama wa wafanyakazi na/au wanafunzi
- Kurusha vitu ambavyo vina uwezo wa kusababisha usumbufu, majeraha, au uharibifu wa rasilimali
- Kumsukuma au kumgonga mwanafunzi bila majeraha yoyote yanayoonekana
- Kuonyeshana sehemu za mwili, tabia chafu au utovu wa adabu kwa umma
- Mgusano wa kimwili wa kingono - kugusa sehemu za mwili, kuchuna, kukunja nguo
- Unyanyasaji wa kingono wa kimwili na/au kumlazimisha mtu mwingine kushiriki katika shughuli ya kingono
- Kuiba pesa au mali bila kutumia nguvu za kimwili
- Kuiba pesa au mali kwa kutumia nguvu za kimwili (Hakuna silaha zilizotumika)
- Kuiba pesa au mali kwa kutumia silaha au vyombo hatari
- Kuondoka majengo ya shule bila ruhusa
- Kuingia bila ruhusa
- Silaha: Kumiliki au kuuza silaha yoyote (bila kujumuisha bunduki) kama ilivyofafanuliwa na sera ya bodi ya shule

Wanafunzi hawatashiriki katika tabia yoyote ambayo inaingiliana na mchakato unaoendelea wa elimu au ambayo inakiuka sheria za serikali, jimbo au za ndani.

#### Tabia ya Maonevu bila maumivu ya kimwili ambayo inaendelea baada ya kuingilia kati/ Maonevu ya mtandaoni ambayo yanaendelea baada ya kuingilia kati

Wanafunzi wote wana haki ya kusoma katika mazingira ambayo hayana hofu, wasiwasi, na unyanyasaji. Maonevu, kejeli, udhalilishaji, au vitendo vingine vya kutia hofu vinaweza kuwa na matokeo mabaya ya muda mrefu kwa ustawi wa kihisia na kielimu wa wanafunzi na, kwa hivyo, vimepigwa marufuku. Sehemu ya §22.1-276.01 ya sheria inafafanua maonevu kama tabia yoyote ya ukatili na isiyohitajika ambayo inalenga kudhuru, kutisha, au kumdhalilisha mhasiriwa; inahusisha ukosefu wa usawa wa nguvu wa kweli au unaokisiwa kati ya mkosaji; na mhasiriwa; na inarudiwa kwa muda au kusababisha kiwewe kikali cha kihisia. Hii inajumuisha maonevu ya mtandaoni. Haijumuishi utani wa kawaida, kuchezeana, mabishano, au mzozano wa wanarika. Bodi ya shule zinatarajiwa kujumuisha maonevu kama tabia iliyopigwa marufuku katika kanuni zao za maadili mema ya wanafunzi.

Wanafunzi hawatashiriki katika udhalilishaji, au vitendo vingine vya kutia hofu wanafunzi wengine. Udhalilishaji ni uhatarishaji wa uzembe au wa makusudi wa afya au usalama, au usababishaji wa majera ya kimwili kwa, mwanafunzi au wanafunzi kuhusiana na au kwa lengo la kuingizwa, kuchukuliwa, au kushirikishwa au kama sharti la kuendelea kuwa mwanachama wa klabu, shirika, undugu, udada, au chama cha wanafunzi bila kujali kama mwanafunzi au wanafunzi aliyehatarishwa au kuumizwa alishiriki kwa hiari katika shughuli husika.

Udhalilishaji ni kosa la jinai na mwanafunzi yeyote anayedhalilisha anaweza kupatikana na hatia ya Makosa ya Daraja la 1 ambayo ina adhabu ya hadi miezi 12 gerezani na/au faini ya hadi $2500.

Mwanafunzi yeyote ambaye amekuwa mhasiriwa wa uhalifu wa kibinafsi akiwa kwenye majengo ya shule au kwenye basi la shule, anaweza kuomba kuhamishwa kwenye shule nyingine katika divisheni ya shule ikiwa uhalifu huo ulitekelezwa na: (1) mwanafunzi mwingine; (2) mfanyakazi wa shule, mfanyakazi wa kibarua, mhudumu wa jamii, au mtu anayetetoa huduma shuleni mara kwa mara.

## Mgusano wa kimwili wa kingono - kugusa sehemu za mwili, kuchuna, kuvuta nguo, / Unyanyasaji wa kingono wa kimwili na/ au kumlazimisha mtu mwingine kushiriki katika shughuli ya kingono

Wanafunzi hawapaswi kutekeleza shambulio la kingono kwa mtu mwingine au kumfanya mtu mwingine kupitia aina yoyote ya unyanyasaji wa kingono.. Shambulio la kingono ni tabia yoyote isiyofaa ya kingono, ikiwemo, lakini haijakomea kwa, kugusa sehemu nyeti na sehemu za siri za mwili wa mtu.
Sexual harassment is any unwelcome advances, requests for sexual favors, *questions of sexuality or description of body parts*, and other inappropriate verbal or physical conduct or contact, including by electronic means, of a sexual nature that creates an intimidating, hostile, or offensive environment.

## Pombe/ Umiliki wa Dawa za Kulevya na/au Usambazaji

Wanafunzi hawapaswi kutumia, kuwa chini ya ushawishi wa, au kumiliki pombe ya aina yoyote (ikiwemo vinywaji vinavyoiga pombe*) kwenye majengo ya shule au katika shughuli zinazofadhiliwa na shule. Wakati kuna shaka ya kutosha kwamba mwanafunzi wa shule ya sekondari amekiuka sheria kwa kushiriki katika unywaji pombe wa watoto wadogo, "kipumuaji" kinaweza kutumiwa na maafisa wa shule ambao wamefunzwa kutumia mashine hiyo. Wanafunzi wa shule ya msingi hawatalazimika kufanyikiwa kipimo cha kipumuaji. Hata hivyo, wazazi/walezi wanapaswa kufahamu utaratibu punde tu mwanafunzi huyo anapoingia shule ya upili.

Wanafunzi hawatapeana, kuuza au kusambaza, au kumiliki kwa lengo la kupeana, kuuza au kusambaza kwenye majengo ya shule au katika shughuli zinazofadhiliwa na shule vinywaji vya aina yoyote *(ikiwemo vinywaji vinavyoiga pombe*).*

**Kwa malengo ya kiwango hiki, "vinywaji vinavyoiga pombe" itamaanisha kiowevu ambacho sio kinywaji cha pombe, lakini kwa mwonekano wa jumla, ikiwemo rangi, alama, pakiti na/au matangazo, au kulingana na uwakilishi, kimekusudiwa kusababisha, au kinaweza kusababisha mtu kuamini kwamba bidhaa hiyo ni kinywaji cha pombe.*

Wanafunzi hawapaswi kutumia, kuwa chini ya ushawishi, au kumiliki kwenye majengo ya shule au katika shughuli zinazofadhiliwa na shule bidhaa zozote zinazodhibitiwa, bangi au dawa za kusisimua misuli, kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Kudhibiti Dawa, Sura ya 34 au Kichwa cha 54.1 cha Sheria ya 21 U.S.C, Sehemu ya 812 ya Virginia, kitu kinachoiga bidhaa zinazodhibitiwa kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya 18.2-247 ya Sheria ya Virginia, au vifaa vya dawa za kulevya kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya 18.2-265.1 ya sheria za Virginia.

Kwa kukiuka au kutumia bidhaa zinazodhibitiwa, au dawa za kusisimua misuli kwenye majengo ya shule na/au shughuli zinazofadhiliwa na shule, mwanafunzi atapendekezwa kufukuzwa shuleni kwa mwaka mmoja (1). Wazazi na watekelezaji sheria wataarifiwa.

Kosa la kwanza la kumiliki bangi au dawa za kusisimua misuli: Badala ya kufukuzwa, msimamizi wa divisheni au mwakilishi wake anaweza kutekeleza hatua zifuatazo za nidhamu, ikiwa itaonekana inafaa hali hiyo: kuondoshwa shuleni kwa siku kumi na kuondoshwa kwa siku arobaini na tano kutoka kwa shughuli za shule. Mwanafunzi pia atahitajika kukamilisha ushauri wa dawa za kulevya na/au pombe*, kama ilivyofafanuliwa katika tathmini tondoti, pamoja na mzazi/mlezi wa mwanafunzi, kwa gharama ya familia.

Kufukuzwa kutapendekezwa na wanafunzi wa RPS waliopatikana na hatia ya kumiliki bangi na/au pombe baada ya tukio la kwanza.

**Ukamilishaji unafafanuliwa kama kukamilisha mpango ulioteuliwa wa kurekebisha tabia au kutii mpango wa kubadilisha tabia kwa miezi tisa, yoyote ambayo inakuja kwanza.*

## Dawa za kulevya: Kukiuka sera ya dawa zisizoagizwa na daktari (Za kwenye kaunta) ya bodi ya shule

**Dawa Zinazoagizwa na Daktari:** Katika hali ya dharura, na ili kuzuia biashara haramu ya dawa zinazoagizwa na daktari, lazima mamlaka ya shule ijue ni dawa gani ambazo mwanafunzi anatumia akiwa shuleni. Kwa hivyo, hakuna mwanafunzi anaweza kumiliki dawa zozote zinazoagizwa na daktari akiwa katika majengo ya shule na/au kwenye rasilimali ya shule, isipokuwa dawa hizo ziwe zimeagizwa na daktari kwa ajili ya mwanafunzi huyo; na mzazi/mlezi wa mwanafunzi awe ameomba na kupokea ruhusa iliyoandikwa kutoka kwa divisheni ya shule kwamba mwanafunzi huyo anaweza kumiliki na kutumia mwenyewe dawa hizo wakati wa siku ya masomo. Ikiwa mtoto anahitaji dawa za kuagizwa na daktari wakati wa siku ya masomo, lazima mzazi/mlezi apeleke dawa zote kwa ofisi ya muuguzi wa shule mwanzo wa siku ya shule ili kuwekwa salama, isipokuwa mwanafunzi awe anatimizi kigezo hapa chini. *

Wanafunzi waliopatikana kuwa na kisukari kutoka kwa daktari mwenye leseni lazima wafahamishe shule ambayo wanahudhuria. Ufafanuzi huu unajumuisha dawa au vifaa vyovyote vinavyotumiwa kutoa dawa kwa ajili ya matibabu au kudhibiti kisukari.

**Dawa Zinazonunuliwa Kwenye Kaunta:** Ili kuzuia madhara mabaya ya dawa au kutumia dawa kupita kiasi, wanafunzi hawapaswi kuwa na dawa zinazonunuliwa kwenye kaunta katika majengo ya shule na/au rasilimali ya shule isipokuwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi awe ameomba na kupokea ruhusa iliyoandikwa kutoka kwa divisheni ya shule ambayo inasema mwanafunzi anaweza kumiliki na kutumia mwenyewe dawa hizo wakati wa siku ya masomo. La sivyo, wanafunzi hawaruhusiwi kuleta dawa zinazonunuliwa kwenye kaunta shuleni. Ikiwa mtoto anahitaji kutumia dawa zinazonunuliwa kwenye kaunta wakati wa siku ya masomo, lazima dawa hizo zipelekwe kwa ofisi ya muuguzi wa shule na mzazi/mlezi isipokuwa iwe mwanafunzi huyo anakidhi kigezo kilicho hapa chini. *

Mwanafunzi aliyethibitishwa kuwa na pumu au mzio mkali, au zote, anaweza kuwa na dawa za kutumia mwenyewe za kuvuta pumzi za pumu au dawa ya epinephrine ya kujidunga mwenyewe, au zote, kulingana na hali, wakati wa siku ya masomo, katika shughuli zinazofadhiliwa na shule, au akiwa kwenye basi la shule au rasilimali nyingine ya shule. Matoleo yanajumuisha: 1) ridhaa iliyoandikwa ya mzazi wa mwanafunzi aliyethibitishwa kuwa na pumu au mzio mkali, au zote, kwamba mwanafunzi huyo anaweza kutumia mwenyewe dawa za kuvuta pumzi za pumu au kujidunga epinephrine, au zote; 2) ilani iliyoandikwa kutoka kwa mtoa huduma msingi wa mwanafunzi au mtaalamu wa matibabu, au daktari mwenye leseni au muuguzi mwenye leseni ambaye anamjua mwanafunzi; kusema kwamba mwanafunzi aliyethibitishwa kuwa na matatizo yaliyotajwa hapo juu, na ana idhini ya kutumia mwenyewe dawa za kuvuta pumzi za pumu au kujidunga epinephrine, au zote, kulingana na hali; kubainisha jina na kipimo cha dawa, marudio ambayo dawa inapaswa kutumiwa na hali nyingine ambazo zinaweza kusababisha matumizi ya dawa, kama vile kabla ya mazoezi au kushiriki katika shughuli za kimwili ili kuzuia kutokea kwa dalili za pumu. *(Angalia mpango kamili katika ofisi ya muuguzi)*

Wakati daktari anathibitisha pumu, mzazi anapaswa kufahamisha shule ya mwanfunzi. Ufafanuzi huu unajumuisha dawa au vifaa vyovyote vya kutumia dawa kwa ajili ya matibabu au kudhibiti kisukari wakati muuguzi wa shule hajaarifiwa kwamba mwanafunzi anahitaji dawa hizi.

## Ufafanuzi:

**Dawa Zinazoagizwa na Daktari:** Dawa au bidhaa yoyote ya kutibu ugonjwa, kuponya, na/au kutuliza maumivu ambayo lazima ipatikane kutoka kwa duka la dawa lenye leseni kulingana na maagizo ya daktari.

**Dawa Zinazonunuliwa Kwenye Kaunta:** Dawa au bidhaa yoyote ya kutibu ugonjwa, kuponya, na/au kutuliza maumivu ambayo inaweza kununuliwa katika duka lolote la rejareja ambalo linauza bidhaa hiyo. Bidhaa hizi zinajumuisha, lakini hazijakomea kwa, aspirin, dawa za kunywa za kukohoa, tembe za kahawa, na dawa zozote zinazokidhi ufafanuzi katika aya hii ambazo hazijaandikwa kwenye karatasi ya maagizo ya daktari.

Wanafunzi hawatapeana, kuuza au kusambaza, au kumiliki kwa lengo la kupeana, kuuza au kusambaza kwenye majengo ya shule au katika shughuli zinazofadhiliwa na shule vinywaji vya aina yoyote *(ikiwemo vinywaji vinavyoiga pombe*).*

**Kwa malengo ya kiwango hiki, "vinywaji vinavyoiga pombe" itamaanisha kiowevu ambacho sio kinywaji cha pombe, lakini kwa mwonekano wa jumla, ikiwemo rangi, alama, pakiti na/au matangazo, au kulingana na uwakilishi, kimekusudiwa kusababisha, au kinaweza kusababisha mtu kuamini kwamba bidhaa hiyo ni kinywaji cha pombe.*

Umiliki, matumizi, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za tumbaku au za matangazo ya tumbaku na wanafunzi umepigwa marufuku. Hii inajumuisha pia nikotini, mafuta ya hasi, mvukizo au bidhaa yoyote ambayo inaweza kutumika kwenye vifaa vya tumbaku, au bidhaa zinazoiga tumbaku.

Matumizi ya sigara za elektroniki yamepigwa marufuku katika basi la shule, rasilimali za shule, na shughuli zinazofadhiliwa na shule.

Kila bodi ya shule itajumuisha katika kanuni yake ya maadili mema ya wanafunzi marufuku ya kumiliki bidhaa yoyote ya tumbaku au bidhaa ya mvukizo ya nikotini, kwa kuwa masharti hayo yamefafanuliwa katika § 18.2-371.2, kwenye basi la shule, kwenye rasilimali ya shule, au kwenye shughuli ya shuleni au nje ya shule inayofadhiliwa na shule.

## King'ora cha moto

Wanafunzi hawapaswi kuwasha ving'ora vya moto bila sababu nzuri. Wanafunzi wanaweza kushtakiwa na watekelezaji sheria wa ndani.

## Kuiba Pesa au Mali

Mwanafunzi hatachukua mali ya kibinafsi ya mtu mwingine kwa makusudi bila ridhaa yake.

## Kuingia bila ruhusa

Mwanafunzi hataingia katika majengo ya shule kinyume na sheria. Hii inajumuisha, lakini haijakomea kwa, matukio ambayo:

a. Mwanafunzi asiyeidhinishwa au mtu mwingine anahudhuria au kutembelea Shule ya Umma ya Richmond, wakati wa siku ya kawaida ya shule bila idhini kutoka kwa msimamizi wa shule.
b. Mwanafunzi kuombwa na msimamizi au afisa mwingine wa shule kuondoka katika majengo ya shule na kukataa kufanya hivyo mara moja.
c. Mwanafunzi amesitishwa kuhudhuria au amefukuzwa na anaenda kwenye majengo ya shule.
d. Mwanafunzi ambaye amenyimwa faida za basi la shule na anaendelea kutumia usafiri wa basi la shule.
e. Mwanafunzi kuwa katika eneo ambalo linatumiwa kama kituo cha basi la shule.

Ikiwa mwanafunzi anaonekana au anasalia kwenye majengo ya shule na/au basi la shule katika matukio yaliyotajwa hapa juu, atachukuliwa kuwa anaingia bila ruhusa. Sehemu hii inatumika pia kwa shughuli yoyote inayofadhiliwa na shule ambayo haifanyiki katika rasilimali za RPS

**Kategoria E: Tabia ambazo Zinahatarisha Mtu au Watu Wengine (BESO), tabia hizi zinahatarisha afya, usalama, au ustawi wa mwanafunzi au watu wengine katika jamii ya shule.**

- Shambulio: Kukusudia kusababisha madhara ya kimwili kwa mtu mwingine
- Shambulio: Kusababisha madhara ya kimwili kwa mtu mwingine
- Kupigana: Matumizi ya ukatili wa kimwili kati ya wanafunzi au mtu mwingine ambapo hakuna majeraha kama ilivyobainishwa na usimamizi wa shule
- Kuwagonga Wafanyakazi: Matumizi ya nguvu dhidi ya mfanyakazi bila majeraha
- Dawa za kulevya: Kumiliki bidhaa zinazodhibitiwa, dawa haramu au dawa sanisi zenye kuleta njozi au dawa zisizoidhinishwa zinazoagizwa na daktari
- Dawa za kulevya: kuwa chini ya ushawishi wa bidhaa zinazodhibitiwa, dawa haramu, au dawa sanisi zenye kuleta njozi au dawa zisizoidhinishwa zinazoagizwa na daktari
- Dawa za kulevya: Kutumia bidhaa zinazodhibitiwa au kutumia dawa haramu au dawa sanisi zenye kuleta njozi au dawa zisizoidhinishwa zinazoagizwa na daktari
- Dawa za kulevya: Kusambaza bidhaa zinazodhibitiwa au dawa zinazoagizwa na daktari au dawa haramu au dawa sanisi zenye kuleta njozi au pombe kwa wanafunzi wengine
- Moto: Kujaribu kuwasha, kusaidia katika kuwasha, au kuwasha moto
- Tabia Zinazohusiana na Magenge: Kushiriki katika tabia zinazotisha au za hatari ambazo zinahusiana na magenge kama ilivyofafanuliwa katika §18.2-46.1
- Udhalilishaji kama ilivyofafanuliwa katika §18.2-56 na kunukuliwa katika § 22.1-279.6
- Kutishia au kuchochea mzozo, majeraha au madhara kwa mfanyakazi
- Kumiliki bunduki au kifaa kinachoangamiza kama ilivyofafanuliwa katika § 22.1-277.07.
- Kutumia silaha yoyote kutishia au kujaribu kujeruhi wafanyakazi wa shule, wanafunzi, au wengine
- Tishio la bomu– Kutoa tishio la bomu

## Kupigana/Shambulio/Kumgonga Mfanyakazi

Mwanafunzi hatashiriki katika mapigano. Mwanafunzi hapaswi kumgonga mtu kimwili au kutekeleza ushambulizi, au kumwonea mtu mwingine. Shambulio linamaanisha kumfanya mtu kuwa na hofu au kutishika kwa makusudi, ikiwemo kwa njia za elektroniki. Hii inajumuisha, lakini haijakomea kwa, unyanyasaji unaotegemea tofauti halisi au zinazokisiwa kama vile jinsia, mbari, rangi, dini, utaifa, mapendeleo ya kingono, au utambulisho wa kijinsia. Ushambulizi unamaanisha tabia ya kudhuru au ya kukera.

Wanafunzi wote wana haki ya kusoma katika mazingira ambayo hayana hofu, wasiwasi, na unyanyasaji. Maonevu, kejeli, udhalilishaji, au vitendo vingine vya kutia hofu vinaweza kuwa na matokeo mabaya ya muda mrefu kwa ustawi wa kihisia na kielimu wa wanafunzi na, kwa hivyo, vimepigwa marufuku. Sehemu ya § 22.1-276.01 ya sheria inafafanua maonevu kama tabia yoyote ya ukatili na isiyohitajika ambayo inalenga kudhuru, kutisha, au kumdhalilisha mhasiriwa; inahusisha ukosefu wa usawa wa nguvu wa kweli au unaokisiwa kati ya mkosaji; na mhasiriwa; na inarudiwa kwa muda au kusababisha kiwewe kikali cha kihisia. Hii inajumuisha maonevu ya mtandaoni. Haijumuishi utani wa kawaida, kuchezeana, mabishano, au mzozano wa wanarika. Bodi ya shule zinatarajiwa kujumuisha maonevu kama tabia iliyopigwa marufuku katika kanuni zao za maadili mema ya wanafunzi.

Katika kila tukio la vita, shambulio, au udhalilishaji, mzazi ataarifiwa. Wanafunzi ambao wanapigana kwa kutaka (kupigana kwa pamoja), hadi matukio ambapo wanafunzi wanachagua kulipiza kisasi badala ya kujiondoa au kuomba msaada kutoka kwa wafanyakazi, watachukuliwa hatua za kinidhamu. Wazazi na polisi wataarifiwa katika matukio ya hali zilizochochewa na/au ambapo matukio hayo yanajumuisha tishio la kuuwa au kutekeleza madhara ya kimwili. Tathmini ya tishio litakamilishwa ili kubainisha ukali wa vitisho. Msimamizi au mwakilishi wake hatachukua hatua ya kinidhamu kwa tishio ikiwa tathmini ya tishio halijakamilishwa ndani ya saa ishirini na nne (24) baada ya tukio. “Tathmini ya tishio” inafafanuliwa kama mchakato wa kutathmini rasmi hali ya tishio kwa mtu au chombo na kufafanua hali ya tishio hilo.

Mwanafunzi yeyote anayetekeleza ushambulizi dhidi ya mwalimu au mfanyakazi wa shule atapendekezwa kufukuzwa. Mwanafunzi anayepatikana kuwa ametekeleza ushambulizi dhidi ya mwalimu au mfanyakazi wa shule anaweza kubadilishwa shule kulingana na Sera ya Bodi ya 8-3.14.

## Shughuli Zinazohusiana na Magenge

Wanafunzi hawapaswi kushiriki katika shughuli za magenge. Genge ni shirika au kundi linaloendelea (1) lenye sifa moja, ikiwemo lakini hazijakomea kwa, taratibu za kuingizwa, ishara za mikono, mitindo ya mavazi, madai mahsusi ya kumiliki himaya ya kijiografia au uongozi unaoweza kutambuliwa; na (2) lenye watu watatu au zaidi, angalau mmoja wao ambaye ni mchanga, ambao wanajitambua kama kundi kwa jina au alama na wanahusika katika mtindo wa tabia zinazojirudia za uhalifu. Shughuli zinazohusiana na magenge zinaweza kusababisha mwanafunzi kupendekezwa kufukuzwa shuleni.

Shughuli za magenge zinafafanuliwa kama:

a. Kuvaa, kusambaza, au kumiliki mavazi yoyote, vito, nembo, beji, alama, ishara, rangi, au bidhaa nyingine ambayo ni ushahidi wa uanachama au kushirikiana na genge lolote.
b. Kutekeleza kitendo chochote, au kutumia semi, aidha kwa maneno au kutotumia maneno (kama vile ishara au salamu za mikono) zinazoonyesha uanachama au kushirikiana na genge lolote.
c. Kutekeleza kitendo chochote cha kuendeleza matakwa ya genge lolote, ikiwemo: (1) kuomba, kudhalilisha, kuwaapisha wengine kuwa wanachama katika genge lolote, (2) kuomba mtu yeyote kulipia ada ya ulinzi au kumtishia mtu yeyote, (3) kutekeleza kitendo chochote haramu au ukiukaji wowote wa SCORE na (4) kuwahimiza wanafunzi wengine kutekeleza vitendo vya ujeuri wa kutumia nguvu.
d. Tabia yoyote isiyofaa na/au shughuli ambazo zinaweza kusababisha hatari kwa mwili, madhara ya kimwili, au madhara ya kiakili kwa wanafunzi, wafanyakazi au wageni.

## Umilizi wa Dawa za Kulevya/Pombe

Kosa la kwanza la kumiliki bangi , au dawa za kusisimua misuli: Badala ya kufukuzwa, msimamizi wa divisheni au mwakilishi wake anaweza kutekeleza hatua zifuatazo za nidhamu, ikiwa itaonekana inafaa hali hiyo: kuondoshwa shuleni kwa siku kumi na kuondoshwa kwa siku arobaini na tano kutoka kwa shughuli za shule. Mwanafunzi pia atahitajika kukamilisha ushauri wa dawa za kulevya na/au pombe*, kama ilivyofafanuliwa katika tathmini tondoti, pamoja na mzazi/mlezi wa mwanafunzi, kwa gharama ya familia.

Kufukuzwa kutapendekezwa na wanafunzi wa RPS waliopatikana na hatia ya kumiliki bangi na/au pombe baada ya tukio la kwanza.

**Ukamilishaji unafafanuliwa kama kukamilisha mpango ulioteuliwa wa kurekebisha tabia au kutii mpango wa kubadilisha tabia kwa miezi tisa, yoyote ambayo inakuja kwanza.*

Wanafunzi hawatapeana, kuuza au kusambaza, au kumiliki kwa lengo la kupeana, kuuza au kusambaza kwenye majengo ya shule au katika shughuli zinazofadhiliwa na shule, bidhaa zozote zinazodhibitiwa, bangi au dawa za kusisimua misuli, kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya Kudhibiti Dawa, Sura ya 34 au Kichwa cha 54.1 cha Sheria ya 21 U.S.C, Sehemu ya 812 ya Virginia, kitu kinachoiga bidhaa zinazodhibitiwa kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya 18.2-247 ya Sheria ya Virginia.

Mwanafunzi huyo atapendekezwa kufukuzwa shuleni. Baada ya kupata kwamba hali maalum zipo, hatua nyingine ya kinidhamu au sheria ya kuondoshwa inaweza kutekelezwa na bodi ya shule. Wazazi na watekelezaji sheria wataarifiwa.

Wanafunzi hawapaswi kuwa na silaha ya aina yoyote (inayofanya kazi au isiyofanya kazi). Hii inajumuisha, ndani ya makabati yao, kwenye mali ya shule, au katika shughuli yoyote inayofadhiliwa na shule.

**Kulingana na Sehemu ya 22.1-277.07 ya Sheria ya Virginia,** mwanafunzi anayepatikana anamiliki bastola au kifaa chochote kama ilivyofafanuliwa hapa chini, kiziba bunduki au kituliza bunduki, au bunduki ya kani ya hewa kama ilivyofafanuliwa hapa chini, kwenye rasilimali ya shule au katika shughuli inayofadhiliwa na shule atafukuzwa shuleni kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja (1). Baada ya kupata kwamba hali maalum zipo, hatua nyingine ya kinidhamu au sheria ya kufukuzwa inaweza kutekelezwa. Wazazi, polisi na mamlaka ya watoto inapaswa kuarifiwa.

**Kama ilivyofafanuliwa na Va. Code §22.1-277.07,** "bastola' inamaanisha silaha yoyote, ikiwemo bunduki ya kuanzisha mbio, ambayo imeundwa au iko tayari kubadilishwa ili kurusha risasi moja au zaidi kwa hatua ya vilipuzi au nyenzo zinazoweza kulipuka au fremu au mpokeaji wa silaha yoyote kama hiyo. "Bastola" haihusishi bunduki yoyote kubwa.

**Kama ilivyofafanuliwa na Va. Code §15.2-915.4,** "bunduki ya kani ya hewa " humaanisha kifaa chochote, kilichoundwa kama bunduki ambacho kinatoa BB au risasi kwa njia ya shinikizo la hewa. "Bunduki ya kani ya hewa" inajumuisha bunduki ambayo inatoa risasi kwa hatua ya shinikizo la hewa kwa plastiki iliyojaa rangi lwa lengo la kuweka alama.

**Kulingana na Va. Code §308.1,** silaha zilizopigwa marufuku kwenye majengo ya shule au katika shughuli zinazofadhiliwa na shughuli zinajumuisha: silaha za kushtua au kisu chochote chenye bapa ya chuma ya inchi 3 au zaidi . Pia silaha zilizopigwa marufuku shuleni n zile zinazoweza kurusha kombora la aina yoyote kwa hatua ya kulipuka kwa bidhaa au nyenzo yoyote inayoweza kulipuka: dirk yoyote, kisu aina ya bowie, kisu cha kubadilisha bapa, kisu cha balistiki, panga, wembe, kombeo, spring stick, ngumi ya chuma, au blackjack, chombo chochote cha kuunganishwa chenye sehemu mbili au tatu ngumu zilizounganishwa ili kuwezesha kubembea kwa urahisi, ambacho kinaweza kujulikana kama nun chahka, nun chuck, nunchakus, shuriken, au nyororo ya kupigana, diski yoyote yenye angalau ncha mbili au bapa zilizochomoza ambazo zimeundwa kutupwa au kurushwa ambayo inaweza kujulikana kama throwing star au oriental dart; au silaha yoyote ya aina hiyo kama ilivyofafanuliwa hapa juu.


**Kulingana na Va. Code §22.1-277.07,** "kifaa angamizi" inamaanisha vilipuzi vyovyote, vifaa vya kuteketeza, au gesi yenye sumu, bomu, guruneti, roketi yenye uwezo wa kurushwa yenye zaidi ya aunsi nne, kombora lenye vilipuzi au nguvu ya kuteketeza ya zaidi ya aunsi robo moja, au kifaa kingine kama hicho; silaha yoyote, isipokuwa bastola au ganda la bastola linalotambuliwa kwa jumla kufaa kwa malengo ya michezo, kwa jina lolote lile linalojulikana au linaweza kubadilishwa kwa urahisi kurusha risasi kwa hatua ya kilipuzi chochote, na kwamba kina mtutu wenye shimo wa zaidi ya inchi moja na nusu kwa upana ambalo limeundwa nyumbani au ambao halikutengezwa na mtengenezaji wa silaha mwenye leseni, bunduki yoyote otomatiki, bastola yoyote iliyokatwa, au bunduki yoyote kubwa iliyokatwa kama ilivyofafanuliwa katika Sheria ya VA ya §18.2-299 au silaha yoyote iliyopigwa marufuku kumilikiwa na raia na sheria ya serikali; na mchanganyiko wowote wa sehemu zilizoundwa au kusudiwa kwa matumizi ya kugeuza kifaa chochote kuwa kifaa angamizi kilichofafanuliwa katika sehemu hii ndogo na ambacho kifaa angamizi kinaweza kutengenezwa kwa haraka.

"Kifaa angamizi" hakitajumuisha kifaa chochote ambacho kimeundwa au kuundwa upya ili kutumiwa kama silaha, au kifaa chochote ambacho kiliundwa asili kama silaha na kwamba kimeundwa upya kutumiwa kama ishara, fataki, kiweka mstari, usalama, au kifaa kingine kama hicho.

# KUONDOSHWA KWA MUDA, KUFUKUZWA, NA RUFAA

## Kuondoshwa Kwa Muda Mfupi (siku 10 au chini)

- Wanafunzi wanaweza kuondoshwa kwa muda shuleni kwa hadi siku tano (5) na mwalimu mkuu wa shule, naibu wa mwalimu mkuu au, ikiwa hawapo, mwakilishi wa mwalimu mkuu na kwa hadi siku tano (5) za shule na mwalimu mkuu wa shule kwa kukubaliana na Msimamizi au mwakilishi wake. Isipokuwa kama ilivyotolewa katika sehemu ndogo ya C au § 22.1-277.07 au 22.1-277.08, hakuna mwanafunzi katika shule ya chekechekea hadi gredi ya tatu atakayeondoshwa kwa zaidi ya siku tatu (3) za shule au kufukuzwa ili asihudhurie shule, isipokuwa (i) kosa hilo linahusisha madhara ya kimwili au tishio la kuaminika kwa wengine au (ii) bodi ya shule au msimamizi wa divisheni au mwakilishi wake amepata kwamba hali za kukasirisha zipo, kama ilivyofafaniliwa na Idara ya Elimu ya Virginia (VDOE). http://www.doe.virginia.gov/info_management/data_collection/support/school_safety/
- Kabla ya kutekeleza hatua ya kuondoshwa, lazima mwalimu mkuu au mwakilishi wa mwalimu mkuu afahamishe mwanafunzi kuhusu mashtaka dhidi yake. Ikiwa mwanafunzi atakataa mashtaka, lazima apewe ufafanuzi wa maelezo yanayojulikana na nafasi ya kuwasilishwa maoni yake. Ikiwa ataona inafaa, mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu au mwakilishi wa mwalimu mkuu atatekeleza uchunguzi zaidi wa suala hilo kabla ya kuamua kama mwanafunzi anapaswa kuondoshwa.
- Wanafunzi ambao uwepo wao unaweza kusababisha hatari inayoendelea kwa watu au mali au tishio linaloendelea la usumbufu wanaweza kuondolewa shuleni mara moja. Ilani ya mashtaka, ufafanuzi wa maelezo, na nafasi ya kuwasilisha maoni yake ya yale yaliyofanyika itatolewa na mwanafunzi hataka iwezekanavyo.
- Baada ya mwanafunzi kuondoshwa shuleni, mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu au mwakilishi wa mwalimu mkuu ataripoti maelezo ya kesi hiyo kwa kumwandikia Msimamizi au mwakilishi wake' na wazazi/walezi wa mwanafunzi kwenye fomu iliyoidhinishwa na Msimamizi. Ilani kama hiyo kwa wazazi/walezi itajumuisha muda wa kuondoshwa shuleni, maelezo kuhusu upatikanaji wa mipango ya elimu ya kijamii, elimu mbadala au mipango mingine, na haki ya mwanafunzi ya kurudi katika mahudhurio ya kawaida ya shule baada ya kuondoshwa shuleni. Gharama ya mpango wowote wa elimu ya kijamii au mpango mbadala wa elimu au chaguo la elimu, ambayo sio sehemu ya mpango wa elimu unaotolewa na divisheni ya shule, utasimamiwa na wazazi/walezi wa mwanafunzi.
- Baada ya maombi yaliyoandikwa ya mzazi, na baada ya kupitia hatua iliyochukuliwa, Msimamizi au mwakilisha wake atathibitisha au kukataa hatua kama hiyo kulingana na uchunguzi wa rekodi ya tabia ya mwanafunzi. Lazima maombi kama hayo yaliyoandikwa yawasilishwe kwa Msimamizi au mwakilishi wake ndani ya siku tano (5) za masomo za ilani ya kuondoshwa au haki ya kukagua Msimamizi au mwakilishi wake itaondolewa.
- Mwanafunzi na wazazi/walezi wake wanaweza kuomba rufaa kuhusu uamuzi wa Msimamizi au mwakilishi wake kwa Kamati ya Nidhamu ya Bodi ya Shule. Kamati ya Nidhamu itazingatia maombi ya rufaa baada ya rekodi ya kuondoshwa katika mkutano wake ufuatao wa kawaida ulioratibiwa.




- Wanafunzi walio na ulemavu wataadhibiwa kulingana na sheria husika za jimbo na serikali.

## Kuondoshwa kwa Zaidi ya Siku Kumi au Kufukuzwa

Kuondoshwa kwa muda mrefu ni hatua ya kinidhamu ambapo mwanafunzi haruhusiwi kuhudhuria shule kwa siku 11 hadi 45 za masomo. Ikiwa, baada ya mwanafunzi kuwa na nafasi ya kujielezea/kutoa maoni yake ya yale yaliyofanyika, mwalimu mkuu au mwakilishi wake ataamua kuondoshwa kwa zaidi ya siku kumi (10) za masomo (siku 11 hadi 45 za masomo) au kufukuzwa kunafaa, ataawarifu mara moja wazazi wa mwanafunzi, kwa kuandika barua kuhusu yafuatayo:

- Hatua inayopendekezwa na sababu zake.
- Kwamba uamuzi wa kumwondosha mwanafunzi kwa zaidi ya siku kumi (10) za masomo utaamuliwa kupitia kusikilizwa kwa jopo mbele ya Msimamizi na mwakilishi wake, ambapo anaweza kuwakilishwa na mshauri na/au kuonyesha ushahidi, na nakala ya taratibu za usikilizaji huu.
- Upatikanaji wa elimu ya jamii, elimu mbadala, au mipango ya kuingilia kati ambayo mwanafunzi anaweza kuhudhuria wakati wa kuondoshwa kwake, na kwamba gharama ya elimu yoyote ya jamii, elimu mbadala, au mpango wa kuingilia kati ambao sio sehemu ya mpango wa elimu unaotolewa na divisheni ya shule ambayo mwanafunzi anaweza kuhudhuria wakati wa kuondoshwa kwake itasimamiwa na mzazi wa mwanafunzi.

Ndani ya siku kumi (10) za masomo za msimamizi au mwakilishi wake kupokea ilani, msimamizi au mwakilishi wake ataamua kama kuondoshwa kwa zaidi ya siku kumi (10) au kufukuzwa kunafaa na atawaarifu wazazi/walezi wa mwanafunzi kwa kuandika barua. Katika tukio kwamba msimamizi au mwakilishi wake ataamua kwamba kuondoshwa kwa zaidi ya siku kumi (10) za masomo kunafaa, atawaarifu wazazi/walezi mara moja, kwa kuandika barua, kuhusu yafuatayo:

- Hatua inayopendekezwa na sababu zake.
- Muda wa kuondoshwa shuleni.
- Upatikanaji wa elimu ya jamii, elimu mbadala, au mipango ya kuingilia kati ambayo mwanafunzi anaweza kuhudhuria wakati wa kuondoshwa kwake, na kwamba gharama ya elimu yoyote ya jamii elimu mbadala, au mpango wa kuingilia kati ambao sio sehemu ya mpango wa elimu unaotolewa na divisheni ya shule ambayo mwanafunzi anaweza kuhudhuria wakati wa kuondoshwa kwake itasimamiwa na mzazi wa mwanafunzi.
- Wakati mwanafunzi atastahiki kurudi kwa mahudhurio ya kawaida ya shule, au kuhudhuria mpango mbadala wa elimu na Bodi ya Shule, au mpango wa elimu ya gumbaru unaotolewa na divisheni ya shule, wakati au baada ya muda kuisha wa kuondoshwa kwa muda, na sheria au masharti baada ya muda kuisha wa kuondoshwa.

Uamuzi wa kutekeleza kuondoshwa kwa muda mrefu unaweza kukatiwa rufaa kwa kamati ya Bodi ya Shule, ambayo itakuwa na angalau wanachama watatu. Kamati hii inaweza kuthibitisha au kuidhinisha kuondoshwa kwa muda kwa mwanafunzi. Ikiwa uamuzi wa kamati si wa kauli moja, mwanafunzi au mzazi wake anaweza kukata rufaa kuhusu uamuzi wa kamati kwa Bodi kamili ya Shule. Bodi ya Shule itaamua kuhusu maombi hayo ya rufaa ndani ya siku thelathini (30).

Bodi ya Shule inaweza kuwasilisha au kuhitaji wanafunzi kuondoshwa kufuatia sehemu hii kuhudhuria mpango mbadala wa elimu unaotolewa na bodi ya shule kwa muda wa kuondoshwa huko.

## Kufukuzwa

**Tafadhali fahamu kwamba, kulingana na sheria za Virginia na/au sera za Bodi ya Shule ya Shule za Umma za Richmond, ukiukaji wa kanuni zingine za maadili mema unahitaji kwamba mwanafunzi apendekezwe kufukuzwa kutoka kwa Shule za Umma za Richmond.**

Ikiwa baada ya mwanafunzi kuwa na nafasi ya kujielezea/kutoa maoni yake ya yale yaliyofanyika, mwalimu mkuu au mwakilishi wake ataamua kwamba pendekezo la kufukuzwa kwa mwanafunzi kunafaa, ataawarifu mara moja wazazi wa mwanafunzi, kwa kuandika barua kuhusu yafuatayo:

- Hatua inayopendekezwa na sababu zake;
- Kwamba Usikilizaji mbele ya Msimamizi au mwakilishi wake utafanyika ndani ya siku kumi (10) ya ilani ili kubainisha kama kufukuzwa kwa mwanafunzi kutapendekezwa na Bodi ya Shule, au kama hatua nyingine ya nidhamu inafaa zaidi, na ambapo usikilizaji unaweza kuwakilishwa na mshauri na/au kuwasilisha ushahidi, na nakala ya taratibu ya usikilizaji huu; na
- Upatikanaji wa elimu ya jamii, elimu mbadala, au mipango ya kuingilia kati ambayo mwanafunzi anaweza kuhudhuria wakati wa kuondoshwa kwake, na kwamba gharama ya elimu yoyote ya jamii, elimu mbadala, au mpango wa kuingilia kati ambao sio sehemu ya mpango wa elimu unaotolewa na divisheni ya shule ambayo mwanafunzi anaweza kuhudhuria wakati wa kuondoshwa kwake itasimamiwa na mzazi wa mwanafunzi.

Ndani ya siku kumi (10) za masomo za kupokea ilani, Msimamizi au mwakilishi wake ataamua kama kufukuzwa kwa mwanafunzi au hatua nyingine ya nidhamu inafaa na atawaarifu wazazi/walezi wa mwanafunzi kwa kuandika barua. Katika tukio kwamba Msimamizi au mwakilishi wake ataamua kwamba kufukuzwa kunafaa, atawaarifu wazazi/walezi mara moja, kwa kuandika barua, kuhusu yafuatayo:

- Hatua inayopendekezwa na sababu zake;
- Muda wa kufukuzwa;
- maelezo kuhusu upatikanaji wa elimu ya jamii, elimu mbadala, au mipango ya kuingilia kati ambayo mwanafunzi anaweza kuhudhuria wakati wa kufukuzwa kwake, na kwamba gharama ya elimu yoyote ya jamii elimu mbadala, au mpango wa kuingilia kati ambao sio sehemu ya mpango wa elimu unaotolewa na divisheni ya shule ambayo mwanafunzi anaweza kuhudhuria wakati wa kufukuzwa itasimamiwa na mzazi wa mwanafunzi;
- Kama mwanafunzi atastahiki kurudi kwa mahudhurio ya kawaida ya shule au la, au kuhudhuria mpango mbadala wa elimu na Bodi ya Shule, au mpango wa elimu ya gumbaru unaotolewa na divisheni ya shule, wakati au baada ya muda kuisha wa kufukuzwa, na sheria au masharti ya kuchukuliwa tena;
- Kwamba gharama ya elimu yoyote ya jamii, mafunzo, au mpango wa kuingilia kati ambao sio sehemu ya mpango wa elimu unaotolewa na divisheni ya shule ambao mwanafunzi anaweza kuhudhuria wakati wa kufukuzwa kwake itasimamiwa na mzazi wa mwanafunzi; na
- Ikiwa Bodi ya Shule itaamua kwamba mwanafunzi hastahiki kurudi kwa mahudhurio ya kawaida ya shule au kuhudhuria wakati wa kufukuzwa katika mpango mbadala wa elimu au mpango wa elimu ya gumbaru katika divisheni ya shule, ilani iliyoandikwa pia itamshauri mzazi wa mwanafunzi huyo kwamba mwanafunzi anaweza kuomba kwa bodi ya shule akubaliwe tena kuanzia mwaka mmoja wa kalenda kuanzia tarehe ya kufukuzwa kwake, na masharti, kama yapo, ambapo kuchukuliwa huko kunaweza kukubaliwa.

Uamuzi wa kuthibitisha au kukataa kufukuzwa kwa mwanafunzi unaweza kufanywa kamati ya Bodi ya Shule, ambayo itakuwa na angalau wanachama watatu. Ikiwa uamuzi wa kamati si wa kauli moja, mwanafunzi au mzazi /walezi wake wanaweza kukata rufaa kuhusu uamuzi wa kamati kwa Bodi kamili ya Shule. Bodi ya Shule itaamua kuhusu maombi hayo ya rufaa ndani ya siku thelathini (30).

Bodi ya Shule inaweza kuwasilisha au kuhitaji wanafunzi waliofukuzwa kufuatia sehemu hii kuhudhuria mpango mbadala wa elimu unaotolewa na bodi ya shule kwa muda wa kufukuzwa huko.

## Taratibu za Kusikilizwa mbele ya Msimamizi au Mwakilishi wake

- Usikilizaji wa jopo utafanyika ndani ya siku kumi (10) kuanzia tarehe ya ilani hii isipokuwa mwanafunzi na/au wazazi/walezi, inapofaa, waombe mwendelezo na mwendelezo huo ukubaliwe na afisa wa usikilizaji.
- Wakati wa usikilizaji wa jopo, ambao utarekodiwa, mwalimu mkuu au mwakilishi wake atawasilisha ushahidi wowote unaounga mkono pendekezo na mwanafunzi, wazazi/walezi, au mwakilishi anaweza kuwakilishwa na mshauri na anaweza kuwasilisha ushahidi. Wahusika wote wanaweza kuwauliza maswali mashahidi, na afisa wa usikilizaji atakuwa huru kuuliza maswali wakati wowote. Afisa wa usikilizaji anaweza kuendelea na usikilizaji wakati ataona hatua kama hiyo inafaa ili kupata maelezo kamili.
- Afisa wa usikilizaji anaweza kupendekeza kwa Msimamizi kwamba adumishe pendekezo la mwalimu mkuu kikamilifu au kwa sehemu, au anaweza kulikataa kabisa.
- Barua itatumwa kwa wazazi/walezi ikiwafahamisha kuhusu uamuzi wa Msimamizi na haki ya kukata rufaa kwa Bodi ya Shule katika kisa cha kuondoshwa na kwa usikilizaji mwingine mbele ya Bodi ya Shule au katika kisa cha ufukuzwaji unaopendekezwa. Barua hii itakuwa na matoleo yote yanayopendekezwa ya ilani. Nakala ya barua hii itatumwa kwa Mkuu wa Wafanyakazi, Mwalimu Mkuu na Meneja wa Huduma za Wafanyakazi wa Wanafunzi.

## Rufaa za Kuondoshwa kwa Muda Mrefu na Kufukuzwa

Katika kisa cha kuondoshwa kwa muda mrefu, mwanafunzi au wazazi/walezi wake wanaweza kuomba rufaa ya uamuzi wa Msimamizi au mwakilishi wake kwa Bodi ya Shule (au, kwa uamuzi wa Bodi ya Shule, kamati), kwa kuarifu Karani wa Bodi ya Shule kwa kuandika barua kuhusu lengo lao la kuomba rufaa ndani ya siku saba (7) za siku za kalenda kuanzia kupokea uamuzi. Kushindwa kuwasilisha maombi yaliyoandikwa ndani ya muda uliobainishwa kutasababisha kuondolewa kwa haki ya kuomba rufaa. Bodi ya Shule itazingatia maombi ya rufaa baada ya rekodi ya usikilizaji wa kuondoshwa ndani ya siku thelathini (3) za kalenda ya maombi ya rufaa. Mwanafunzi ataendelea kuwa ameondoshwa shuleni kwa muda wa maombi hayo ya rufaa.

- Mwanafunzi au wazazi/walezi wanaweza kuomba rufaa mbele ya Bodi ya Shule, (au, kwa uamuzi wa Bodi ya Shule, kamati), kuhusu uamuzi wa Msimamizi na mwakilishi wake wa kupendekeza kuondoshwa kwa kuarifu Karani wa Bodi ya Shule kwa kuandika kuhusu ombi lao ndani ya siku saba (7) za kalenda kuanzia kupokea uamuzi huu. Kushindwa kuwasilisha ombi lililoandikwa ndani ya muda uliobainishwa kutasababisha kuondolewa kwa haki ya kusikilizwa mbele ya kamati ya Bodi ya Shule.

Usikilizaji utafanyika katika mkutano ufuatao wa kawaida isipokuwa ombi la kusikilizwa lipokewe chini ya siku tano (5) kabla ya mkutano, ambapo usikilizaji huo utawekwa na Mwenyekiti haraka iwezekanavyo. Mwanafunzi ataendelea kuwa ameondoshwa shuleni huku akisubiri usikilizaji wa kamati ya Bodi ya Shule. Bod ya Shule ina mamlaka ya kubatilisha uamuzi wa Msimamizi au kurekebisha uamuzi wa Msimamizi katika hali yoyote. Uamuzi wowote wa kumfukuza mwanafunzi unahitaji hatua ya Bodi ya Shule ili uweze kutumika.

- Uamuzi uliofanywa na Bodi ya Shule au kamati, utawasilishwa kwa mwanafunzi na wazazi/walezi wake kwa kuandika barua, na utafuata matoleo husika ya ilani.
- Hakuna kitu chochote katika sehemu hii kitachukuliwa kupiga marufuku Bodi ya Shule dhidi ya kuruhusu na kuwahitaji wanafunzi waliofukuzwa, kulingana na sehemu hii ndogo, dhidi ya kuhudhuria mpango mbadala wa elimu wa Bodi ya Shule.

**Wanafunzi walio na Ulemavu chini ya Sheria ya Kuboresha Elimu kwa Watu walio na Ulemavu ya 2004 (IDEA), Wanafunzi walio na Ulemavu Walihitimu chini ya Sehemu ya 504 ya Sheria ya Urekebishaji Tabia ya 1973, na Wanafunzi wanaoondoshwa ambao ni walemavu lakini bado hawajabainika kuwa wanastahiki au wanahitimu**

Sehemu hii imelengwa kuwa maombi na muhtasari wa sheria na masharti ya serikali katika Sheria ya Kuboresha Elimu kwa Watu walio na Ulemavu ya 2004 (IDEIA). Sheria na Masharti ya Elimu Maalum ya Serikali na Virginia inachukua nafasi ya kwanza kuliko hati hii. Familia inaweza kupata maelezo ya ziada kuhusu wanafunzi walio na ulemavu na mchakato wa nidhamu katika Virginia kutoka kwa Idara ya Elimu ya Virginia.

Mwongozo wa Kuelewa Elimu Maalum ya Idara ya Virginia (2010) inaweza kupatikana kwenye:
http://www.doe.virginia.gov/special_ed/parents/parents_guide.pdf

## Idadi ya Wanafunzi

Kwa lengo la kuondoshwa na kufukuzwa kwa wanafunzi, taratibu fulani maalum za elimu za mchakato yakinifu zinatolewa kwa wanafunzi wafuatao:

- Mwanafunzi ambaye ametambuliwa kuwa na ulemavu chini ya IDEIA au chini ya Sehemu ya 504:
- Mwanafunzi ambaye anashukiwa kuwa na ulemavu, lakini bado hajabainishwa kustahiki au kuhitimu kupokea huduma.
- Wanafunzi ambao wamebainishwa kustahiki elimu maalum na huduma husika chini ya IDEIA au ambao hawajastahiki elimu maalum au huduma husika chini ya Sehemu ya 504, na ambao wamehusika katika tabia ambayo inakiuka kanuni yoyote ya maadili, wanaweza kudai kinga zozote zilizotolewa chini ya IDEIA ikiwa divisheni ya shule ina “msingi wa ufahamu” kwamba mwanafunzi alikuwa mwanafunzi mwenye ulemavu kabla ya tabia ambayo ilisababisha hatua ya kinidhamu iliyochukuliwa. Divisheni ya shule ina “msingi wa ufahamu” kwamba mwanafunzi ni mwanafunzi mwenye au anayeshukiwa kuwa mlemavu ikiwa:

Wazazi/walezi wa mwanafunzi wameonyesha wasiwasi kwa kuandika (au kwa maneno ikiwa mzazi haandiki au ana ulemavu ambao unamzuia kuandika taarifa) kwa mhudumu wa shule kwamba mwanafunzi anahitaji elimu maalum na huduma husika:

- Wazazi/walezi wameomba kwamba mtoto wao atathminiwe ili kubainisha kustahiki kwa elimu maalum na huduma husika.
- Mwalimu wa mwanafunzi, au mhudumu wa shule, ameonyesha wasiwasi kuhusu mtindo wa tabia ya mwanafunzi moja kwa moja kwa Mkurugenzi wa Elimu ya Kipekee wa Shule za Umma za Richmond au kwa mhudumu mwingine wa ushauri wa Shule za Umma za Richmond.

Vighairi vya “msingi huu wa ufahamu” katika sehemu iliyo hapo juu hufanyika ikiwa:

- Mzazi hakuruhusu tathmini ya mwanafunzi au alikataa huduma ya elimu maalum na huduma husika.
- Tathmini ilitekelezwa na ikabainishwa kwamba mwanafunzi hana ulemavu.

## Taratibu za Kuondolewa

### Kuondolewa kwa Mwanafunzi kwa Siku Kumi (10) za Masomo au chini katika Mwaka wa Masomo (Kuondolewa kwa Muda Mfupi)

- Mhudumu wa shule anaweza kumwondoa mwanafunzi mwenye ulemavu kwa “muda mfupi” kutoka kwa mazingira ya sasa ya elimu hadi kwa mazingira mbadala ya muda yanayofaa ya elimu, mazingira mengine, au kumwondosha mwanafunzi husika kwa kadri ambavyo mipango hiyo mbadala inaweza kutumika kwa mwanafunzi asiyekuwa na ulemavu.
- Hatua za ziada za kuondolewa kwa muda mfupi zinaweza kutumika kwa mwanafunzi aliye na ulemavu ndani ya mwaka wa masomo kwa matukio tofauti ya utovu wa nidhamu ilimradi kuondolewa huko kusiwe ni mtindo.

- Shule za Umma za Richmond hazihitajiki kutoa huduma wakati wa siku kumi (10) za kwanza za masomo katika mwaka wa masomo ambao mwanafunzi mwenye ulemavu ameondolewa kutoka kwa mazingira yake ya sasa ya elimu.
- Kwa hatua za ziada za kuondolewa kwa muda mfupi, ambazo sio za mtindo, Shule za Umma za Richmond zitatoa huduma kwa kadri itakavyobainishwa inafaa ili kuwezesha mwanafunzi kuendelea kushiriki katika mtalaa wa jumla wa elimu na kuendelea kuwadia kutumiza malengo ya IEP ya mwanafunzi. Mhudumu wa shule, kwa kushirikiana na mwalimu wa elimu maalum wa mwanafunzi, atafanya maamuzi haya ya huduma.
- Ikiwa idadi ya siku za shule ambazo mwanafunzi ataondolewa shuleni zitafikia siku kumi (10), msimamizi wa majengo au mwakilishi wake anaweza kukusanya timu ya IEP ya kukagua na kupitia IEP. Mkutano huu unaweza kushughulikia mabadiliko yoyote yanayohitajika katika huduma au mipango. Timu ya IEP inaweza kutengeneza na kukamilisha Tathmini ya Tabia (FBA), na inaweza kutengeneza na kutekeleza Mpango wa Kuingilia Kati Tabia (BIP). Ikiwa BIP ipo, timu ya IEP itapitia na kurekebisha BIP kama inavyohitajika.

**Mwanafunzi Kuondolewa kwa Zaidi ya Siku 10 za Masomo katika Mwaka wa Masomo (Kuondolewa kwa Muda Mrefu)**

- Wanafunzi wanaweza kuondolewa kwa zaidi ya siku kumi (10) mtawalia za siku za masomo bila kikomo wakati wa mwaka wa masomo, ikiwa kuondolewa huko sio kubadilishwa kwa mpango.
- Kubadilishwa kwa mpango hufanyika ikiwa: kuondolewa kwa mwanafunzi ni kwa zaidi ya siku kumi (10) mtawalia au mwanafunzi aondolewe kwa muda mfupi mara kadhaa ndani ya mwaka wa masomo ambao inakuwa ni mtindo. Mhudumu wa shule ataamua ikiwa mfululizo huu wa kuondolewa utasababisha kubadilishwa kwa mpango. Ili kuamua hii, mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:

    a. Muda wa kila hatua ya kuondolewa.
    b. Ukaribu wa kila hatua ya kuondolewa.
    c. Ikiwa tabia ya mwanafunzi ni sawa na tabia ya mwanafunzi huyo katika matukio ya hapo awali ambayo yalisababisha mfululizo wa kuondolewa.
    d. Jumla ya muda ambao mwanafunzi umetengwa darasani. Lazima mzazi afahamishwe kwa kuandikiwa kuhusu matokeo ya uamuzi huu.

Wakati uondoaji hausababishi kubadilishwa kwa mpango, huenda mwanafunzi akaondolewa kutoka kwa mpango wake wa elimu kulingana na taratibu za kuondoshwa kwa wanafunzi wasio kuwa na ulemavu. Hata hivyo, lazima taratibu zifuatazo zitekelezwe:

a. Kutoa, ikiwa zipo, huduma ambazo zitamwezesha mwanafunzi kuendelea inavyofaa katika mtalaa wa kawaida na kuendelea zaidi inavyofaa katika kuelekea kutumiza malengo ya IEP. Huduma hizi zinaamuliwa na timu ya IEP ya mwanafunzi.
b. Ikiwa inafaa, kusanya timu ya IEP kabla au ndani ya siku tano (5) za kazi baada ya kumwondoa mwanafunzi kwa mara ya kwanza kwa zaidi ya siku kumi (10) za masomo ili kutekeleza tathmini ya kitabia, na kubainisha huduma zinazofaa za kuingilia kati tabia na marekebisho ambayo yameundwa kushughulikia ukiukaji wa tabia ambao unaweza kufanyika.

Wakati kuondolewa huko kunasababisha mabadiliko ya mpango, lazima taratibu zifuatazo zitekelezwe:

a. Kutoa, ikiwa zipo, huduma ambazo zitamwezesha mwanafunzi kuendelea inavyofaa katika mtalaa wa kawaida na kuendelea zaidi inavyofaa katika kuelekea kutumiza malengo ya IEP. Huduma hizi zinaamuliwa na timu ya IEP ya mwanafunzi.
b. Ikiwa inafaa, kusanya timu na IEP kabla au ndani ya siku tano (5) za kazi baada ya kumwondoa mwanafunzi kwa mara ya kwanza kwa zaidi ya siku kumi (10) za masomo ili kutekeleza tathmini ya kitabia, na kubainisha huduma zinazofaa za kuingilia kati tabia na marekebisho ambayo yameundwa kushughulikia ukiukaji wa tabia ambao unaweza kufanyika.

Lazima timu ya IEP ijibu pia maswali yafutayo:

1. Je, tabia ya mwanafunzi ilisababishwa na, au ilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na ulemavu wa mwanafunzi?
2. Je, tabia ya mwanafunzi ilitokana moja kwa moja na kushindwa kwa divisheni ya shule kutekeleza IEP?
   Katika visa ambavyo timu ya IEP inaamua kwamba tabia ilitokana na ulemavu wa mwanafunzi huenda kuondolewa au kufukuzwa kusifanyike na timu ya IEP:

    1. Itatekeleza FBA na kukuza BIP ya mwanafunzi.
    2. Ikiwa BIP tayari ipo, pitia mpango uliopo na uurekebishe kama inavyofaa ili kushughulikia tabia hii.
    3. Itamrejesha mwanafunzi kwa mpango wa elimu ambapo aliondolewa, isipokuwa wazazi/walezi na wahudumu wa shule wakubaliane mabadiliko ya mpango kama sehemu ya kurekebisha mpango wa kuingilia kati tabia.
    4. Itakagua na kupitia IEP kama inavyohitajika ili kushughulikia tabia ambayo inaweza kujumuisha mabadiliko na/au nyongeza katika malengo, huduma na mpango.

Kwa uondoaji utakaofuata, wakati mabadiliko ya mpango yamefanyika, uamuzi wa sababu lazima ufanywe na wazazi/walezi na wanatimu husika wa IEP, ndani ya siku tano (5) za biashara za uamuzi wa kuondoshwa.

## Silaha/Dawa za Kulevya/Bidhaa Zinazodhibitiwa/Majeraha Mabaya ya Kimwili

Matoleo yafuatayo yanatumika kwa mwanafunzi yeyote aliye na ulemavu ambaye: (a) anabeba silaha, au anamiliki silaha, shuleni, kwenye rasilimali ya shule au kwenye hafla ya shule; (b) kwa kujua anamiliki, kutumia, kuuza au kuomba kuuza dawa haramu au bidhaa yoyote inayodhibitiwa akiwa shuleni, kwenye rasilimali ya shule au hafla ya shule; au (c) amemjeruhi vibaya kimwili mtu mwingine akiwa shuleni, kwenye majengo ya shule au katika hafla ya shule:

Msimamizi wa shule, pamoja na mwakilishi wa Ofisi ya Elimu ya Kipekee na Huduma za Wanafunzi, anaweza kumweka mwanafunzi katika mazingira mbadala ya muda ya elimu (IAES) kwa siku zisizozidi arobaini na tano (45) za masomo. Ruhusa ya mzazi haihitajiki. Mwanafunzi akiwa katika mpango wa IAES, mhudumu wa shule:

a. Lazima amwezeshe mwanafunzi kuendelea katika mtalaa wa kawaida ijapokuwa katika mazingira tofauti.
b. Lazima atoe huduma na marekebisho yaliyofafanuliwa katika IEP ya sasa ambayo yatamwezesha mwanafunzi kukidhi malengo ya IEP.
c. Atekeleze, kama inavyotakikana, tathmini ya kitabia, na kuamua huduma na marekebisho yanayofaa ya kuingilia kati tabia ambayo yameundwa kushughulikia ukiukaji wa tabia ili usifanyike tena kama ilivyotolewa katika Hatua za Kuondolewa kwa Muda Mrefu katika 2b hapo juu.
d. Wakati IAES inapoisha muda wake, mwanafunzi atarudi kwa mpango wake wa zamani wa elimu, isipokuwa mzazi/walezi na LEA wakubaliane kivingine kupitia mkutano wa IEP. Pia, Afisa wa Usikilizaji au amri ya mahakama inaweza kuongezea IAES.

## Mengineyo

- Shule zinaweza kuripoti uhalifu kwa polisi hata kama mwanafunzi anayehusika katika ukiukaji anachukuliwa, au anashukiwa, kuwa na ulemavu.
- Mwanafunzi aliye na ulemavu ana haki ya usikilizaji sawia wa kesi ambao wanafunzi wote wanao chini ya sera na taratibu za nidhamu za Shule ya Umma ya Richmond.
- Ikiwa wakati wa kupitia IEP ya mwanafunzi inayofaa hatua ya nidhamu, timu ya IEP ione mapungufu katika IEP au mpango wa mwanafunzi, timu ya IEP, itachukua hatua za haraka kurekebisha mapungufu hayo.
- Huenda mwanafunzi asiondolewe shuleni kwa zaidi ya siku kumi (10) huku michakato ya timu ya IEP ikianzishwa na kukamilishwa, isipokuwa wazazi/walezi watoe ruhusa ya mabadiliko ya mpango kupitia mkutano wa timu ya IEP. Hii haitumiki kwa matukio yanayohusisha silaha, dawa za kulevya, bidhaa zinazodhibitiwa, majeraha mabaya ya kimwili. Matukio haya yanaweza kusababisha kuondolewa mara moja kwa IAES kwa siku arobaini na tano (45) za masomo.
- Lazima makala ya taratibu za ulinzi zipewe wazazi/walezi wa mwanafunzi aliye na ulemavu siku ambayo uamuzi unafanywa wa kuchukua hatua ya kinidhamu ya mwanafunzi kuondolewa ambayo inasababisha kubadilishwa kwa mpango kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni ya maadili mema ya wanafunzi.
- Ikiwa mwanafunzi yuko chini ya tathmini ya IDEIA au Sehemu ya 504 wakati tukio la kinidhamu linafanyika, tathmini itaharakishwa.
- Wakati wa kiahirisho cha kesi yoyote ya hatua ya nidhamu, mwanafunzi atasalia katika mpango wake wa sasa wa elimu, ambao unaweza kuwa IAES.

## Usikilizaji Ulioharakishwa

Huenda Shule za Umma za Richmond zikaomba mchakato ulioharakishwa wa usikilizaji wa kesi ikiwa zitashikilia kwamba ni hatari kwa mwanafunzi kuwa katika mpango wa sasa wa elimu (mpango wa elimu kabla ya kuondolewa kwa mazingira mbadala ya muda) huku usikilizaji wa mashtaka ukisubiri. Huenda wazazi/walezi wakaomba usikilizaji ulioharakishwa ikiwa hawakubaliani na:

- Uamuzi wa kwamba tabia ya mwanafunzi haikutokana na ulemavu wa mtoto.
- Uamuzi wowote kuhusu mpango wa elimu chini ya taratibu za nidhamu.

***Kumbuka:*** *Maneno IEP au timu ya IEP yanatumika pia kwa mipango ya 504 au timu za 504.*

## Ufafanuzi wa Maneno

**Mtindo:** Mfuatano wa kuondolewa shuleni kwa sababu ya matukio yasiyohusiana kwa zaidi ya siku kumi (10) za shule kwa mwaka kwa sababu ya mambo kama vile muda wa kila hatua ya kuondolewa, jumla ya muda wa kuondolewa, na ukaribu wa kila hatua ya kuondolewa.

**IAES:** Mazingira ya Elimu Mbadala ya Umma ambayo humwezesha mwanafunzi kuendelea katika mtalaa wa kawaida katika mazingira tofauti na kupokea huduma na marekebisho katika IEP. Mpango huu utamwezesha pia mwanafunzi kutimiza malengo yake ya IEP na huduma zimeundwa kuzuia tabia mbaya dhidi ya kutokea tena.

**Watu wengine wanaohitimu:** wamejumuishwa ili kuhakikisha kwamba watu wa uchunguzi na wengine wamo katika mkutano wa IEP kwa ajili ya utaalamu wao katika kutathmini masuala yanayopitwa na timu ya IEP.

**Majeraha mabaya ya kimwili:** Madhara ambayo yanahusisha hatari ya kifo, maumivu makali ya kimwili, kupoteza kiungo, au kupoteteza au kuharibika kwa kiungo cha mwili, ogani au kiungo.

# TAARIFA ZA SHUGHULI ZINAZODAIWA ZA UTOVU WA NIDHAMU

Huenda bodi ya shule, kulingana na taratibu zilizowekwa katika Makala ya 3 (§ 22.1- 276.01 et seq.) za Sura ya 14 na baada ya matokeo kwamba mtoto mwenye umri wa kwenda shule (i) amehukumiwa kwa kosa linalohusiana na sheria za Jumuiya ya Madola, au kwa ukiukaji wa sera za bodi ya shule, kuhusu silaha, pombe na dawa za kulevya, au kumuumiza mtu mwingine kwa makusudi; (ii) amepatikana ana hatia ya uhalifu ambao ulisababisha au unaweza kusababisha majeraha kwa wengine, au kosa ambalo linahitaji kufichuliwa kwa divisheni ya shule kulingana na sehemu ndogo ya G ya § 16.1-260; (iii) ameondoshwa kwa muda kulingana na § 22.1-277.05; au (iv) amefukuzwa shuleni kulingana na § 22.1-277.06 au 22.1- 277.07 au sehemu ndogo ya C ya § 22.1-277, inahitaji mtoto kuhudhuria mpango mbadala wa elimu kama ilivyotolewa katika § 22.1-209.1:2 au 22.1-277.2:1.

Kulingana na Va. Code §16.1-260(G), msimamizi wa divisheni ya shule lazima apokee taarifa ikiwa:

Mhusika katika maombi anadai kwamba mwanafunzi ambaye ni mtoto ametekeleza kitendo, mahali popote kilichofanyika, ambacho kitakuwa uhalifu ikiwa kimetekelezwa na mtu mzima, au kwamba mwanafunzi huyo ambaye ni mtu mzima ametekeleza uhalifu na anadaiwa kuwa katika mamlaka ya mahakama. Ripoti hiyo itamwarifu msimamizi wa divisheni kuhusu uwasilishaji wa maombi na hali ya kosa, ikiwa ukiukaji huo unahusisha:

- Kosa la silaha kulingana na Makala ya 4 (§ 18.2-279 et seq.), 5 (§ 18.2-288 et seq.), 6 (§ 18.2-299 et seq.), au 7 (§ 18.2-308 et seq.) ya Mlango wa 7 wa Kichwa cha 18.2.
- Mauaji, kulingana na Makala ya 1 (§ 18.2-30 et seq.) ya Sura ya 4 Kichwa cha 18.2,
- Shambulio la kikatili na majeraha ya kimwili, kulingana na Makala ya 4 (§ 18.2-51 et seq.) ya Sura ya 4 Kichwa cha 18.2.
- Shambulio la kingono, kulingana na Makala ya 7 (§ 18.2-61 et seq.) ya Sura ya 4 Kichwa cha 18.2.
- Utengenezaji, uuzaji, zawadi, usambazaji au umiliki wa bidhaa zinazodhibitiwa za Ratiba ya 1 au ya II, kulingana na Makala ya 1 (§ 18.2-247 et seq.) ya Sura ya 7 ya Kichwa cha 18.2.
- Utengenezaji, uuzaji au usambazaji wa bangi, au bangi ya kemikali, kulingana na Makala ya 1 (§ 18.2-247 et seq.) ya Sura ya 7 Kichwa cha 18.2.
- Uchomaji na uhalifu husiika, kulingana na Makala ya 1 (§ 18.2-77 et seq.) ya Sura ya 5 Kichwa cha 18.2.
- Wizi wa uvunjaji na makosa husika, kulingana na §§ 18.2-89 hadi 18.2-93.
- Wizi wa mabavu kulingana na § 18.2-58.
- Shughuli zilizopigwa marufuku za jinai za magenge ya mitaa kulingana na § 18.2-46.2.
- Kuwasajili watoto katika shughuli za jinai za magenge ya mitaa kulingana na § 18.2-46.2.
- Tendo la uhasama la umati wa watu kulingana na § 18.2-42.1.
- Kushindwa kutoa maelezo kuhusu shule ambayo mwanafunzi ambaye ni mhusika wa maombi amesajiliwa kutakuwa sababu za kukataa kuwasilisha maombi.
- Maelezo yaliyotolewa kwa msimamizi wa divisheni kulingana na sehemu hii yanaweza kufichuliwa tu kama yalivyotolewa katika § 16.1-305.2.

## Maelezo ya Rufaa

Wazazi/walezi wana haki ya kuomba maombi ya rufaa kuhusu kuwekwa katika mazingira mbadala ya elimu. Ikiwa mzazi/mlezi anataka kuomba rufaa ya uamuzi, anapaswa kuomba rufaa kwa kumwandikia Afisa Mkuu wa Shule. 301 North Ninth Street, 17th floor, Richmond, VA 23219. Lazima maombi haya yatumwe ndani ya siku saba (7) za kazi kuanzia kupokea kwa ilani hii ya kuwekwa katika mazingira mbadala ya elimu. Kushindwa kuwasilisha maombi yaliyoandikwa ndani ya muda mahususi kutasababisha kuondolewa kwa haki ya kuomba rufaa.

Ikiwa mzazi/mlezi angependa kuomba rufaa ya uamuzi uliofanywa na Afisa Mkuu wa Shule kuhusu kuhamishwa kwa mpango mbadala wa elimu, maombi hayo yanapaswa kutumwa kwa kuandika kwa chool Board of the City of Richmond, C/O Clerk of the School Board. Lazima maombi haya yatumwe ndani ya siku saba (7) za biashara kuanzia kupokewa kwa uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Elimu ya Kipekee na Huduma za Wanafunzi. Kushindwa kuwasilisha maombi yaliyoandikwa ndani ya muda mahususi kutasababisha kuondolewa kwa haki ya kuomba rufaa.

Tafadhali zingatia kwamba ni lazima mwanafunzi ahudhurie mpango mbadala akisubiri mchakato wa rufaa. Wanafunzi wanaoshindwa kuhudhuria wanaweza kuripotiwa kwa utoro.

# KUKUZA TABIA NZURI YA WANAFUNZI KWENYE MABASI YA SHULE

Wanafunzi wote watasimamiwa na kanuni za sehemu hii wakisafiri kwenye mabasi ya shule kwenda na kutoka shuleni au shughuli zinazohusishwa na shule, kama vile, lakini haijakomea kwa, safari za kimasomo, makongamano, au matukio ya riadha. Usimamizi wa shule na wahudumu wa Ulinzi na Usalama wana haki ya kutekeleza ukaguzi usiokuwa na mpangilio maalum wa mabasi ya shule na, kukiwa na tashwishi ya kuaminika, abiria wa basi la shule.

Matokeo yanayowahusisha wanafunzi walio na ulemavu, wale ambao wameshughulikiwa chini ya Sehemu ya 504, na wanafunzi wale ambao kwa sasa wako chini ya tathmini ya watoto, au michakato ya kustahiki itatekelezwa kulingana na haki zao chini ya sheria za serikali na jimbo.

Kuabiri basi la shule ni fadhila. Fadhila hii inaweza kubatilishwa ikiwa utovu wa nidhamu unahatarisha shughuli salama za basi la shule au usalama wa wanafunzi wanaopanda basi. Tabia au shughuli inayohatarisha shughuli salama za basi la shule au kuhatarisha maslahi ya abiria wengine zimepigwa marufuku. Dereva wa kila basi atashirikiana na msimamizi wa shule katika kazi yake katika shule ambayo anawasafirisha wanafunzi kwa kufika kwa wakati unaofaa kila asubuhi na kusubiri jioni hadi wanafunzi wote waruhusiwe kutoka shuleni na usimamizi wa shule na kupanda basi kwa usalama. Madereva watakuwa makini zaidi wakiwa katika njia yao asubuhi na kuwapa wanafunzi wanaoonekana muda unaofaa ili wapande basi. Dereva atawajibika kudumisha maadili mema kwenye basi. Madereva wataripoti ukiukaji wowote wa maagizo yao au kanuni, kupitia fomu za rufaa, kwa usimamizi wa shule.

Wafanyakazi wa usimamizi watapitia rufaa za madereva na kujibu kwa hatua inayofaa ya nidhamu ikihitajika. Nakala ya ripoti ya utovu wa nidhamu itarejeshwa kwa msimamizi wa mabasi ya shule. Kwa ujumla, utovu wa nidhamu kwenye basi la shule hakutamzuia mwanafunzi kufika darasani. Hata hivyo, kuondoshwa kwa muda shuleni, pamoja na kufukuzwa, kunaweza kufanyika katika visa maalum vya utovu wa nidhamu ambao unasababisha hatua hiyo.

| Matokeo ya Ukiukaji Unaohusiana na Usafiri wa Wanafunzi unajumuisha, lakini Haujakomea kwa: | | | |
|---|---|---|---|
| **KOSA LA 1** | **KOSA LA 2** | **KOSA LA 3** | **KOSA LA 4** |
| **Simu kwa Mzazi/Mlezi** | **Mkutano wa Mzazi/Mlezi** | **Kusimamishwa Kutumia Basi (Siku 1 hadi 5)** | **Kusimamishwa Kutumia Basi (Siku 6 hadi 10)** |

Utovu wa nidhamu ufuatao utasababisha hatua za kinidhamu. Orodha hii sio kamili na haitakuwa kizuizi cha mamlaka ya Bodi ya Shule au maafisa wa shule kushughulikia na aina nyingine za utovu wa nidhamu ambazo zinaingilia utendakazi sahihi wa shule. Wakati mwanafunzi amesimamishwa kutumia basi, hataruhusiwa kuhudhuria au kushiriki katika shughuli zozote za baada ya masomo.

### Matokeo ya Tabia Zisizofaa katika Basi la Shule

## Tabia ya Kutisha
Tabia ya kutisha inayoelekezwa kwa wanafunzi wengine na/au wahudumu watu wazima wa shule hushughulikiwa katika Viwango vya Tabia ya Wanafunzi Nambari 9 - Kupigana, Shambulio, Maonevu; na mwanafunzi yeyote anayekiuka Kiwango hiki kwenye basi la shule ataadhibiwa kulingana na kiwango hicho. Kutakuwa na matokeo yanayolingana kwenye basi la shule kwa mwanafunzi huyo kama matokeo ya tabia yake.

## Kupigana
Kupigana kumeshughulikiwa katika Kategoria E: Tabia ambazo Zinakuhatarisha Wewe Mwenyewe au Wengine (BESO) na mwanafunzi yeyote anayepigana kwenye basi ataadhibiwa kulingana na kiwango hicho. Kutakuwa na matokeo yanayolingana kwenye basi la shule kwa mwanafunzi huyo kama matokeo ya tabia yake.

## Silaha
Silaha zimeshughulikiwa katika Kategoria E: Tabia ambazo Zinakuhatarisha Wewe Mwenyewe au Wengine (BESO) na mwanafunzi yeyote anyemiliki silaha kwenye basi la shule ataadhibiwa kulingana na kiwango hicho. Kutakuwa na matokeo yanayolingana kwenye basi la shule kwa kosa hili.

## Tabia ya Kuvuruga

Tabia ya kuvuruga inajumuisha, lakini hayajakomea kwa, kutoa maoni yasiyofaa wakati wa kupanda/kushuka basi, kukataa kutii opareta wa basi, kupiga kelele, kunywa na kula kwenye basi, na matumizi ya lugha chafu. Ikiwa tabia zozote kati ya hizi zitafanyika kwa njia inayotisha, zinapaswa kushughulikiwa kulingana na Kategoria B: Tabia zinazohusiana na Shughuli za Shule (BSO). Isipokuwa matokeo ya tabia ya kuvuruga isemwe wazi, huenda mwalimu mkuu/mwakilishi wake:

a. Akakutana/kumshauri mwanafunzi na au bila wazazi/walezi na dereva wa basi ikiwezekena:
b. Akatekeleza mkataba wa tabia ya mwanafunzi
c. Akamwondosha mwanafunzi kwenye basi kwa siku moja (1) hadi tatu (3); akamwondosha mwanafunzi kwa siku tatu (3) hadi tano (5) kwenye basi na mkutano wa mzazi/mlezi; akamwondosha mwanafunzi kwa zaidi ya siku tano (5)
d. Akaomba usikilizaji wa kinidhamu katika kiwango cha shule kwa kuondoshwa kwenye basi kwa zaidi ya siku kumi (10) (isipokuwa kama ilivyoandikwa katika sehemu inayohusu wanafunzi wenye ulemavu)

## Uharibifu wa mali

Uharibifu wa mali ya shule unapaswa kushughulikiwa kulingana na Kategoria B iliyopo: Tabia zinazohusiana na Shughuli za Shule (BSO). (Ambazo zinahitaji kwamba wanafunzi/wazazi walipie hasara inayotokana na uharibifu wa mali) na hata pia taratibu zilizopo za Usalama na Ulinzi za kushtaki matukio ya uharibifu wa mali. Chini ya sera iliyopo ya Idara ya Usafiri, wanafunzi na wazazi wanapewa chaguo la kusafisha basi badala ya malipo ya hasara. Mamlaka ya watoto wadogo yataarifiwa.

## Usalama

Makosa ya kuhatarisha usalama yanajumuisha, lakini hayajakomea kwa, kushindwa kumtii dereva wa shule, kuweka sehemu yoyote ya mwili (au mwili wa mtu mwingine) nje ya dirisha, kutupa vitu mahali popote, kushindwa kusalia umeketi chini, kuharibu vifaa vya basi la shule, kuwasha viberiti au viwashi, na kumiliki mali ya magendo kwenye basi la shule. (Ikiwa yoyote kati ya tabia hizi zitafanyika kwa njia ya ukaidi, zitashughulikiwa kwa Kategoria B: Tabia zinazohusiana na Shughuli za Shule (BSO). Matokeo ya tabia ya kuhatarisha usalama yanajumuisha, lakini hayajakomea kwa:

a. Mwanafunzi kushauriwa.
b. Siku mbili (2) hadi tano (5), kuondoshwa kwenye basi, kuhudhuria mkutano na mwanafunzi, wazazi/walezi wake, mwalimu mkuu na dereva wa basi kabla ya mwanafunzi kurudi kwenye basi, na kutekeleza mkataba wa tabia.
c. Kuhudhuria darasa la usalama wa basi.
d. Usikilizaji wa kinidhamu katika kiwango cha shule kwa kusimamishwa kutumia basi kwa zaidi ya siku kumi (10), isipokuwa katika kisa cha wanafunzi fulani wanaolindwa ambapo kukomesha huduma, bila kujumuisha usafiri na huduma husika, hakuruhusiwi.
e. Kuarifu mamlaka yanayofaa ya kisheria.

- **Umiliki au Matumizi ya Tumbaku au Bidhaa za Tumbaku** *(Angalia Kategoria D: Tabia zinazosababisha Wasiwasi wa Kiusalama, BSC)*
- **Umiliki au Matumizi ya Dawa Haramu au Pombe** *(Angalia Kategoria E: Tabia ambazo Zinakuhatarisha Wewe au Wengine, BESO)*
- **Usambazaji au Uuzaji wa Pombe au Dawa Haramu au Kumiliki kwa Lengo la kuuza au kusambaza** *(Angalia Kategoria D: Tabia zinazosababisha Wasiwasi wa Kiusalama ( BSC)*
- **Umiliki au Matumizi ya Dawa na Dawa Zinazoagizwa na Daktari** *(Angalia Kategoria E: Tabia ambazo Zinakuhatarisha Wewe au Wengine, BESO)*
- **Shambulio na Unyanyasaji wa Kingono** *(Angalia Kategoria E: Tabia ambazo Zinakuhatarisha Wewe au Wengine, BESO)*
- **Vifaa vya Kurekodi Video na Sauti** *(Angalia Kategoria B: Tabia zinazohusiana na Shughuli za Shule, BSO)*

Mabasi mengi ya shule sasa yana vifaa vya kurekodi video na sauti. Zana hizi hufuatilia eneo la abiria la basi. Lengo lake ni kutoa zana ya ziada ya kumsaidia dereva na usimamizi katika kudhibiti tabia za wanafunzi kwenye mabasi ya shule, ili kutoa mazingira salama na mazuri.

# TITLE IX

## Title IX ni nini?

Title IX ya Marekebisho ya Elimu ya 1972 yanapiga marufuku ubaguzi kwa msingi wa jinsia (ikiwemo unyanyasaji wa kingono, ukatili wa kijinsia, na unyanyasaji kwa msingi wa jinsia) katika mipango na shughuli za elimu ambazo zinapokea usaidizi wa kifedha wa serikali. Baadhi ya maeneo makuu ambayo wapokeaji wana wajibu wa Title IX ni:  Uandikishaji, usajili, na ushauri; msaada wa kifedha; riadha; unyanyasaji kwa msingi wa jinsia, kuwatendea wanafunzi wajawazito na wazazi; nidhamu; elimu ya ngono, na ajira.

## Inamaanisha nini?

Pia, mpokeaji hawezi kulipiza kisasi dhidi ya mtu yeyote kwa kupinga kanuni haramu za kielimu, au kufanya mabadiliko, kutoa ushahidi au kushiriki katika hatua yoyote ya malalamiko chini ya Title IX. Kwa mpokeaji kulipiza kisasi kwa njia yoyote ile inachukuliwa kuwa ukiukaji wa Title IX. Shule zimepigwa marufuku dhidi ya kuzuia usajili au kushiriki katika shughuli kwa msingi wa jinsia. Kuhusu michezo, lazima wanafunzi wanaume na wanawake wawe na nafasi sawa za kushiriki. Maelezo ya Title IX yaliyotolewa hapa yanatumika kwa vituo, shughuli na mipango yote ya Shule za Umma za Richmond. Divisheni na vyuo vyote vya shule vinapokea aina fulani ya ufadhili wa serikali, kwa hivyo hii inatumika kwa kila mtu.

## Kwa nini Title IX ni muhimu?

Ofisi ya Haki za Raia (OCR) ilitoa barua ya "Mpendwa Mshirika" na hata pia hati ya Maswali na Majibu ya kurasa 46 kuhusu jinsi mipango ambayo ilipokea fedha za serikali inapaswa kushughulikia malalamishi ya ubaguzi na/au ukatili wa kijinsia yanayokiuka Title IX.



# KUFAFANUA “Njia YA RPS” YA KUREJESHA MAADILI

## Kanuni za “Kurejesha Maadili” ni nini?

Kanuni za kurejesha maadili ni njia za makusudi ambazo viongozi wa shule, walimu, wafanyakazi, na wanafunzi wanaanzisha mahusiano mema ili kuunda jamii ndani ya shule. Kanuni za Kurejesha Maadili hukuza uadilifu, usawa, na heshima, na zinaweza pia kutumiwa kurekebisha makosa katika jamii ya shule, ikihitajika.

## Kanuni za kurejesha maadili zinatoshea aje katika Dreams4RPS?

Kutekeleza kanuni za kurejesha maadili katika shule zetu ni muhimu kufikia Kipaumbele cha 3 cha Dreams4RPS: Mazingira Salama na ya Upendo ya Shule. Wakati zitatumika kabisa katika mazingira ya RPS, kanuni hizi zitasaidia kuongezea mahudhurio, kupunguza kuondoshwa, na kuboresha masomo. Kwa kufanya hivyo, tunaamini zitaboresha pia kuridhika kwa wafanyakazi.

## Tunarajia kufanikisha nini katika Awamu ya 1 ya kazi ya kanuni za kurejesha maadili?

Ili kuanza, tutaenda kuzingatia kanuni mbili:

- **Makundi ya Jamii.** Makundi ya Jamii ni mikutano ya mara kwa mara ya makundi madogo ya wananfunzi yaliyo na mwezeshaji mtu mzima (msimamizi, mwalimu, mfanyakazi wa kusaidia, kocha, n.k.). Mikutano hutumia itifaki za makusudi zilizoundwa kuunda nafasi salama na kukuza kwa wanafunzi wote. Mada za mikutano zinaweza kutofautiana: kuanzia kuangalia jinsi wanafunzi wanahisi siku hiyo hadi kuchunguza mada fulani (k.m. Tukio ambalo lilifanyika shuleni). Kwa ufupi, Makundi ya Jamii yanalenga kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wana kundi msingi la marafiki na angalau mtu mzima mmoja ambaye wana mahusiano wazi, mazuri na thabiti. Kanuni za kuwajali wengine hujumuishwa mara kwa mara kwenye Makundi ya Jamii ili kuwasaidia wanafunzi kuwepo na kuwa wazi zaidi wakati wa mazungumzo.

- **Makundi ya Msaada.** Makundi ya Msaada yamebuniwa kuwapa watu ambao wamesababisha madhara nafasi ya kukubali maumivu waliyoyasababisha, kukubali kuwajibika, na kujitolea kwa hatua zinazofuata zinazohitajika kurejesha imani iliyovunjika katika jamii. Makundi ya Msaada hutumia itifaki ya makusudi na yanayoongozwa na wafanyakazi waliofunzwa kimahsusi katika kila shule. Ndoto yetu ya muda mrefu ni kwamba Makundi ya Msaada yatafanywa katika chumba kinacho wajali wengine katika kila shule ya PRS. Vyumba kama hivyo vitapatikana pia kwa wanafunzi, walimu, na wafanyakazi kutumia ili kupunguza mizozo na kudhibiti hisia. Kumbuka: Makundi ya Msaada hayachukui nafasi ya kuondoshwa kwa muda au matokeo mengine. Yanalenga kurekebisha madhara yaliyosababishwa na watu katika jamii ili kuongezea nafasi kwamba madhara kama hayo hayatafanyika tena.

# Kufafanua “Njia ya RPS” ya Mazoea ya Kukabiliana na Kiwewe

## “Mazoea ya kukabiliana na kiwewe” ni nini?

Mazoea ya kukabiliana na kiwewe yanatokana na kanuni sita za kuelekeza zilizotolewa kutoka Kituo cha Kudhibiti Magonjwa (CDC), ambazo zinasisitiza: usalama, uaminifu na uwazi, msaada wa wanarika, ushirikiano na maafikiano , sauti ya uwezeshaji na chaguo na masuala ya kitamaduni, kihistoria na jinsia. Mazoea yanayotokana na kanuni hizi hufundishwa na kutumiwa na wafanyakazi wa mafunzo, wafanyakazi wa usaidizi na wasimamizi.

## Mazoea ya kukabiliana na kiwewe yanaingiliana vipi katika Dreams4RPS?

Kutekeleza mazoea ya kukabiliana na kiwewe katika shule zetu ni muhimu kufikia Kipaumbele cha 3 cha Dreams4RPS: *Mazingira Salama na ya Upendo ya Shule*. Kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu, yenye maana kwa walimu wetu kuhusu uenezo na ujuzi unaohitajika ili kuwahudumia kwa ufanisi wanafunzi na familia zinazokabiliwa na msongo mbaya katika maisha yao.

## Je, tumekuwa tukishughulikia nini katika kazi yetu ya kukabiliana na kiwewe?

- Mafunzo yanayoendelea kwa wafanyakazi wa shule kuhusu uenezi wa kiwewe, jinsi athari ya kiwewe inavyoathiri masomo na tabia, na athari za kiwewe kali.
- Kuwafunza wafanyakazi wa shule huongeza mazoea ya darasani ya kukabiliana na kiwewe.
- Kuongeza fursa za kufundisha na kujifunza kudhibiti hisia. Ni muhimu kutoa fursa kwa wanafunzi na wafanyakazi kujifunza mikakati ya kutuliza siku nzima. Haya yanafundishwa na kutekelezwa kupitia Vikundi vya Kuimarisha Jamii, mahali patulivu madarasani na katika majengo, mapumziko ya akili siku nzima na kupitia mtaala wa Masomo ya Kijamii na Kihisia (SEL).
- Kutoa fursa kwa wafanyakazi kupata uzoefu wa kudhibiti dhiki na mbinu za ustawi ili kupunguza kiwewe kali.

# SERA YA MAHUDHURIO YA WANAFUNZI

Idadi ya Juu ya Kutokuwepo ambayo Inaruhusiwa Kulingana na Sera ya Bodi ya Shule 8-2.4 Kutowepo/Utoro wa mahudhurio ya Wanafunzi

Idadi ya Juu ya Kutokuwepo ambayo Inaruhusiwa, Wanafunzi hatakosa shuleni (kwa sababu zinazoruhusiwa au la, bila kujumuisha kuondoshwa kwa muda) kwa:

- Siku kumi na nane (18) au zaidi kwa mwaka.
- Vipindi kumi na nane (18) vya masomo (siku tisa (9) kwa somo moja la muhula).

## Kwa nini Mahudhurio ni Muhimu?

Sehemu ya 22.1-254 ya Sheria za Virginia zinahitaji kwamba divisheni zote za shule ziwafahamishe wazazi kuhusu mahitaji ya kuhudhuria kwa lazima na taratibu za utekelezaji ndani ya siku thelathini (30) ya mwanzo wa kila mwaka wa masomo. Mahudhurio ya kawaida ya shule ni muhimu kwa maendeleo ya elimu ya wanafunzi na huchangia maendeleo ya mazingira salama ya shule. Shule za Umma za Richmond zinatarajiwa, na zinahitajika, kuunga mkono sera za mahudhurio za shule.

Shule za Umma za Richmond zinatarajiwa kuchukua hatua kadhaa ili kuunga mkono ufuatiliaji na utekelezaji wa mahudhurio.

- Kutambua na kukuza orodha ya watoto na vijana wote wenye umri wa kwenda shule ambao hawajasajiliwa katika mpango ulioidhinishwa wa elimu;
- Kuchunguza ukiukaji unaowezekana wa mahitaji ya kuhudhuria kwa lazima; na
- Kutekeleza mahitaji ya mahudhurio.

Chini ya mwongozo wa Msimamizi, walimu wakuu wa shule, kwa kushirikiana na Maafisa wa Mahudhurio wa Shule za Umma za Richmond, watatekeleza mahitaji ya lazima ya mahudhurio, ikiwemo kushindwa kuhudhuria shule ya majira ya joto, ikihitajika. Kipaumbele kitapewa watoto na vijana wasiosajiliwa kati ya umri wa miaka 5 na 18. Chaguo za utekelezaji zinajumuisha zifuatazo:

- Kujaza ombi la Mtoto Anayehitaji Usimamizi (CHINS) na mahakama ya watoto.
- Kufungua mashtaka ya jinai (makosa ya Daraja la 3) dhidi ya wazazi/walezi wa wanafunzi watoro na wasiosajiliwa.
- Kutekeleza mahitaji ya mahudhurio ya lazima wakati wa vikao vya majira ya joto ikiwa msimamizi ataamua kwamba mahudhurio kama hayo ni muhimu kwa wanafunzi kupandishwa cheo, kupita mitihani ya Viwango vya Masomo (SOL, au kufanikiwa ifaavyo shuleni.

Isitoshe chaguo hizi za utekelezaji, Shule za Umma za Richmond zinahitajika kuripoti wapokeaji wote wa Misaada ya Muda ya Familia zenye Mahitaji (TANF) wanaokiuka mahudhurio ya lazima ya shule na matoleo ya utoro kwa Idara ya Huduma za Jamii kwa uchunguzi zaidi na uwezekano wa kupunguzwa kwa faida.

Tafadhali hakikisha wanafamilia wako wanajua kuhusu mahitaji haya. Ni muhimu kwamba sote tufanye kazi pamoja katika kukuza mahudhurio ya kawaida ya shule, ambayo ni muhimu kwa ufanisi wa wanafunzi. Tafadhali wasiliana na Culture, Climate and Student Services kwenye 804-780-6070 ikiwa una maswali yoyote.

### Ni Katika Hali Gani Wanafunzi wa Zamani Wanahudhuria Shule?

Kama kanuni ya jumla, mtu ambaye amefikia umri wa miaka ishirini (20), mnamo au kabla ya Agosti 1 ya mwaka wa masomo, ataruhusiwa kuhudhuria shule akiwa na ruhusa maalum pekee ya Msimamizi. Bodi ya Shule, kwa uamuzi wake, inaweza kutoza ada kwa wanafunzi kama hao.

Huenda Bodi ya Shule ikakubali na kutoa mipango kwa wanafunzi ambao Kiingereza ndio lugha yao ya pili walioingia shule katika Virginia kwa mara ya kwanza baada ya kufikia umri wa miaka kumi na miwili (12), na ambao hawajafikia umri wa miaka ishirini na na miwili (22) mnamo au kabla ya Agosti 1 ya mwaka wa masomo. Hakuna ada itakayotozwa kwa wanafunzi kama hao ikiwa ufadhili wa jimbo umetolewa kwa mipango kama hiyo.

Wanafunzi walio na ulemavu ambao wanahitaji elimu maalum na huduma husika (1) ambao siku yao ya pili ya kuzaliwa iko mnamo au kabla ya Septemba 30 na hawajafikia siku yao ya kuzaliwa ya ishirini na mbili (22) mnamo au kabla ya Septemba 20; na (2) bado hawajahitimu na diploma ya kawaida au ya juu ya elimu, watastahiki kuhudhuria shule bila malipo.

### Kutokuwepo Ukiwa na Ruhusa ni nini?

Kutokuwepo ukiwa na ruhusa huainishwa kama zile ambazo zimefanyika kutokana na hali zaidi ya udhibiti wa wanafunzi, wazazi/walezi, au shule, na itahesabika katika hesabu ya mwisho ya kutokuwepo. Bodi ya Shule inachukulia zaidi ya siku kumi na tano (15) za kutokuwepo ukiwa na ruhusa katika muhula kuwa zimepita kiasi. Udhuru wa pekee unaoruhusiwa ambao utachukuliwa kuwa unakubaliwa ni:

- Ugonjwa wa kibinafsi:  Ikiwa ni zaidi ya siku tatu (3), shule itahitaji barua kutoka kwa daktari.
- Kuhudhuria mahakama binafsi.
- Kifo katika familia (baba, mama, mwenzi, mwana wa kiume, wa kike, dada, ndugu, babu/nyanya, shangazi, mjomba na mpwa.
- Sikukuu za kidini zinazoadhimishwa mara kwa mara na mwanafunzi.
- Mambo makali, kama ilivyoidhinishwaa na usimamizi wa shule.

## Ni Lini Wanafunzi Wanazingatiwa Wapo Ijapokuwa Sio Shuleni?

Wanafunzi wanazingatiwa wapo wakati wanashiriki katika safari za kielimu, matukio ya riadha, shughuli zinazosimamiwa na serikali, na kazi nyingine zinazotekelezwa na shule. Wanafunzi wanarekodiwa wapo kwenye rekodi zote za shule.

## Kuchelewa/Kuondoka Shuleni Bila Ruhusa

Kwa kawaida utoro ni dalili ya matatizo ya kibinafsi au ya kifamilia. Divisheni ya shule itafanya juhudi zinazofaa kusaidia kutatua kiini cha matatizo ambacho kinaathiri mahudhurio ya kawaida ya wanafunzi’ Rufaa kwa mashirika ya nje na idara nyingine katika Shule za Umma za Richmond zitatumiwa kusaidia kutatua na kupunguza utoro.

- Kuchelewa / Kuondoka Mapema - Lazima wanafunzi wawasili kwa wakati na wachukuliwe kwa muda ulioratibiwa wa kuachiliwa shule. Kuchelewa na kuondoka mapema kunaweza kuzingatiwa kumeruhusiwa kwa sababu zile zilizoorodheshwa za kutokuwepo. Kwa malengo ya sera hii, lazima mwanafunzi achelewe kwa zaidi ya dakika thelathini (30) shuleni, au aondoke dakika thelathini (30) mapema, bila ruhusa iliyoidhinishwa na mwalimu mkuu au mwakilishi wake. Wanafunzi wanaohudhuria shule nje ya kanda za mtaa walio na ruhusa maalum ambapo wazazi/walezi wanawajibika kutoa usafiri) watahitajika kuhudhuria shule mara kwa mara au waondolewe shuleni kwa kuwaarifu wazazi/walezi na Ofisi ya Huduma za Wahudumu wa Wanafunzi. Matoleo ya Sheria ya Shule ya Lazima ya Virginia yanatumika kwa shule zote.
- Kuondoka shuleni bila ruhusa - Punde tu mwanafunzi anapowasili kwenye rasilimali ya shule, hawezi kuondoka bila ruhusa ya usimamizi.

## Majukumu ya Wazazi

- Ni lazima wazazi na walezi watume barua inayotoa sababu na tarehe za kutokuwepo shuleni, siku ambayo mwanafunzi anarudi shuleni. Ikiwa barua haitatolewa ndani ya siku tano (5) za masomo  ya siku ya mwisho ya kukosa shule, kipindi cha kutowekupo kitachukuliwa hakikuwa na ruhusa.
- Huenda wazazi walezi wakaomba idhini ya kutokuwepo kwa kujaza ombi mapema na mwalimu mkuu au mwakilishi wake. Maombi kama hayo yatatiwa saini na mwalimu mkuu au mshauri wake na kurejeshwa kwa wazazi/walezi. Nakala itahifadhiwa ili kurejelewa.

## Kazi ya Kurudia Inaweza Kuombwa?

Kwa kutokuwepo ukiwa na sababu na kutokuwa na sababu, wazazi/walezi wanahitajika kuomba kazi ya kurudia baada ya kurudi shuleni. Walimu watapanga na kuratibu kazi ya kurudia inayofaa, ambayo inapaswa kukamilishwa ndani ya siku tano (5) ya mwanafunzi kurudi shuleni. Kazi iliyotolewa ya kurudia, lakini haijakamilishwa wakati wa kipindi kilichowekwa, itarekodiwa kama kuanguka gredi kwa kazi hiyo isipokuwa mwalimu atoe muda wa ziada.

Walimu watoa kazi ya kurudia ikiwa wana sababu ya kutohudhuria. Ni wajibu wa wazazi/walezi kuomba kazi ya kurudia kwa kutokuwepo bila ruhusa. Wanafunzi ambao wamefukuzwa shuleni watapokea na kukamilisha kazi zote za elimu (kazi ya darasani na ya nyumbani) wakati wa kipindi cha kuondoshwa na kuwasilisha kazi iliyokamilishwa kwa mwalimu wake wa darasa baada ya kurudi shuleni.

***Kumbuka:*** *Lazima wazazi/walezi waelewe kwamba masomo mengine hayawezi kutolewa kazi ya kurudia ya kukamilisha nje ya darasa, hasa ikiwa mwanafunzi hakuwa wakati somo lilifunzwa.*

## Jukumu la Shule ni Nini Wakati Mwanafunzi hayupo?

Sheria ya Virginia inahitaji kwamba, “Kila mwalimu katika kila shule katika Jumuiya ya jamii aweke rekodi sahihi ya kila siku ya mahudhurio ya watoto wote. Kadi ya mahudhurio ya wanafunzi na rekodi ya darasa ya mwalimu ndio rekodi rasmi za kutokuwepo kwa wanafunzi.

Shule itawasiliana na wazazi/walezi kila siku ambayo mwanafunzi hayupo shuleni. Ikiwa mwanafunzi atalimbikiza kutokuwepo mara nne (4) bila sababu, taarifa iliyoandikwa itatumwa kwa wazazi/walezi. Ikiwa mwanafunzi atalimbikiza kutokuwepo mara tano (5), mwalimu mkuu au mwakilishi wake atafanya juhudi  ya kuhakikisha kwamba mawasiliano ya moja kwa moja yamefanywa na wazazi/walezi, aidha ana kwa na au kupitia mazungumzo ya simu, na afisa wa mahudhurio ili kupata ufafanuzi wa kutokuwepo kwa mwanafunzi na kuwafafanulia wazazi/walezi matokeo ya kuendelea kutokuwepo. Mwalimu mkuu wa shule au mwakilishi wake, kama vile afisa wa mahudhurio, mwanafunzi na wazazi/walezi wa mwanafunzi, watatengeneza pamoja mpango wa kutatua kutohudhuria kwa mwanafunzi// Mpango kama huo utajumuisha hati za sababu ya mwanaffunzi kutokuwepo.

Ikiwa mwanafunzi hayupo kwa zaidi ya siku moja ya ziada baada ya kuwasiliana moja kwa moja na mzazi wa mwalimu, na mhudumu wa shule hajapokea ishara kwamba mzazi wa mwanafunzi anafahamu na kuunga mkono kutokuwepo kwa mwanafunzi, mwalimu mkuu wa shule au mwakilishi wake atapanga mkutano na mwanafunzi, mzazi wake, na mhudumu wa shule. Mkutano kama huo unaweza kumhusisha afisa wa mahudhurio na watoa huduma wengine wa jamii ili kutatua matatizo yanayohusiana na kutohudhuria kwa mwanafunzi. Mkutano utafanywa

siku 10 za masomo baada ya mwanafunzi kutokuwepo kwa mara ya kumi, haijalishi kama mzazi ameidhinisha mkutano huo. Timu ya mkutano itafuatilia mahudhurio ya mwanafunzi na inaweza kukutana tena kama inavyofaa ili kushughulikia wasiwasi na kupanga hatua za ziada ikiwa mahudurio hayataimarika. Katika hali ambazo kwa makusudi mzazi hafuati mahitaji ya mahudhurio ya lazima au mwanafunzi anakataa juhudi za mzazi za kutii mahitaji ya lazima ya mahudhurio, mwalimu mkuu au mwakilishi wake atamwelekeza kwa afisa wa mahudhurio. Afisa wa mahudhurio atapanga mkutano na mwanafunzi na mzazi wake ndani ya siku 10 za shule na anaweza (i) kuwasilisha malalamiko na mahakama ya watoto na mahusiano ya kinyumbani akidai mwanafunzi huyo ni mtoto anayehitaji kusimamiwa kama ilivyofafanuliwa § 16.1-228 au (ii) kuanzisha kesi dhidi ya mzazi kulingana na § 18.2-371 au 22.1-262. Katika kuwasilisha malalamiko dhidi ya mwanafunzi, afisa wa mahudhurio atatoa hati zilizoandikwa za juhudi za kutii matoleo ya sehemu hii. Katika tukio kwamba wazazi wote wanashirikiana ulezi kulingana na § 20-124.2 na shule imepokea ilani ya amri kama hiyo, wazazi wote wataarifiwa kwenye anwani za mwisho zilizojulikana za wazazi.

### Sera ya Ruhusa ya Kutohudhuria

Chini ya hali nyingine, msamaha wa sera hizi za mahudhurio zinaweza kuzinatiwa na msimamizi wa divisheni. Mwanafunzi na mzazi wake au mlezi wa kisheria wanaweza kuomba, na msimamizi wa divisheni au mwakilishi wake anaweza kuwapa, msamaha kwa sababu zifuatazo: (1) ugumu wa kimatibabu (hali ambayo mwanafunzi hangeweza kuhudhuria kama ilivyohakikishwa na daktari mwenye leseni) (2) hali nyingine maalum sana, kama ilivyobainishwa na msimamizi wa divisheni au mwakilishi wake. Ombi la msamaha litafanywa kwa kuandikia barua msimamizi wa divisheni na linaweza kufanywa wakati wowote wakati wa mwaka wa masomo punde tu kutokuwepo kunazidisha kiwango kinachoruhusiwa. Ombi litajumuisha (a) idadi ya jumla ya kutokuwepo kwa mwanafunzi, (b) ufafanuzi wa ugumu wa matibabu au hali nyingine maalum sana, (c) uthibitishaji kwamba kazi ya kurudia ilikamilishwa.

# TARATIBU ZA MATUMIZI YANAYOKUBALIKA YA INTANETI YA SHULE ZA UMMA ZA RICHMOND

Matumizi yanayofaa ya wanafunzi ya Intaneti yameshughulikiwa katika SCORE Kiwango hiki kinatambua jukumu la wanafunzi kama watumiaji wanaowajibika wa Intaneti na rasilimali zinazotolewa. Wanafunzi katika Shule za Umma za Richmond watapewa ufikiaji wa intaneti kwa malengo ya elimu. Watapewa akaunti binafsi za barua pepe au ufikiaji usiosimamiwa wa zana nyingine za kutumia intaneti. Kwa hivyo, SCORE itatumika kama mwongozo wa ufafanuzi wa matumizi yanayokubalika ya Intaneti katika Shule za Umma za Richmond. Ikiwa una maswali kuhusu kufikia Intaneti, wasiliana na msimamizi wa shule yako. Maelezo hapa chini yametolewa kwa kitivo na usimamizi kama ya nyongeza ili kushiriki na wanafunzi katika kuwandaa kwa matumizi yao ya intaneti.

### Matumizi ya Intaneti kwa Ajili ya Mafunzo ya Shule za Umma za Richmond

Wanafunzi wa RPS watafuata njia iliyopangwa ya kupata ujuzi ambao utawawezesha kuwa watumiaji huru, wanaowajibika wa Intaneti. Njia hii inashughulikia matumizi ya intaneti kulingana na umri na mada zinazofaa.

Katika shule za msingi ((K-5), kitivo kitasimamia matumizi ya wanafunzi ya intaneti. Wanafunzi watafikia rasilimali za Intaneti ambazo walimu wao wamechunguza na kuchagua awali. Kitivo kitafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaelekezwa tu kwa tovuti ambazo zinafaa umri na mada.

### Taratibu za Matumizi Yanayokubalika ya Intaneti ya Shule za Umma za Richmond

Lengo la Taratibu za Matumizi Yanayokubalika ya Intaneti ya RPS ni kuhakikisha kwamba watumiaji wote wanaohusika katika kufikia rasilimali za intaneti wanafuata maazimio na malengo yaliyosemwa ya RPS na SCORE Na nafasi hii, kuna wajibu wa matumizi yanayofaa. Inatarajiwa kwamba kompyuta zote za divisheni zinazofikia Intaneti zitumiwe kwa njia ya kuwajibika, inayofaa, ya kimaadili na halali.

RPS itatoa ufikiaji wa intaneti kwa wanafunzi, kituo, na usimamizi wote. Wanafunzi kukubali taratibu hizi umeongezwa na kujumuishwa kwao katika SCORE Kitivo, usimamizi, na wanafunzi lazima wakubali taratibu hizi kabla ya kupewa akaunti binafsi za kufikia rasilimali za intaneti.

Matumizi ya rasilimali za intaneti ni fadhila, sio haki. Matumizi yasiofaa ya intaneti yatasababisha kughairishwa kwa faida hizo na/au hatua ya kinidhamu na maafisa wa shule. Shughuli zote za watu wote wakati wa kutumia intaneti katika Shule za Umma za Richmond lazima ziunge mkono elimu na utafiti, na zilingane na malengo ya kielimu ya Shule za Umma za Richmond. Watu wote wanaofikia intaneti kutoka kwa kituo cha shule wanawajibika kwa shughuli zote za mtandaoni ambazo zinafanyika kupitia ufikiaji huo. Wakati unatumia mtandao mwingine wa shirika au rasilimali za kompyuta, watu wote lazima watii sheria zinazofaa za mtandao huo.

## Matumizi Yanayokubalika

Hatua zifuatazo, ambazo sio kamili, zinajumuisha matumizi yanayokubalika ya Intaneti, iwe matumizi hayo yameanzishwa na shule au kituo kingine chochote:

1. Utafiti uliopangiwa miradi ya darasani.
2. Kutuma barua pepe kwa watumiaji wengine.
3. Kufikia na kubadilishana maelezo.
4. Kutumia Intaneti kwa malengo ya kielimu pekee.

## Mali ya Kisheria

1. Tii sheria za alama za biashara na hakimiliki na makubaliano yote ya leseni. Kupuuza sheria sio utetezi na hakukupi kinga ya aina yoyote. Ikiwa huna uhakika kuhusu upakuaji wa nyenzo yoyote, muulize mwalimu au msimamizi kabla ya kuchukua hatua.
2. Wizi wa maandishi ni ukikaji wa SCORE Taja vyanzo vyote vilivyotumiwa, iwe vimenukuliwa au kufupishwa. Hii ni pamoja na aina zote za midia kwenye Intaneti, kama vile michoro, filamu, muziki, na maandishi.
3. Matumizi au umiliki wa programu za kuingia bila ruhusa umepigwa marufuku na wakiukaji watasimamiwa na sheria za SCORE za Shule za Umma za Richmond Ukiukaji wa sheria husika au sheria za jimbo utasababisha mashtaka ya jinai na/au hatua ya kinidhamu na Shule za Umma za Richmond.

## Matumizi Yasiokubalika

Hatua zifuatazo, ambazo sio kamili, zinajumuisha matumizi yasiyokubalika ya Intaneti, iwe matumizi hayo yameanzishwa na shule au kituo kingine chochote:

1. Kutumia lugha ya ujeuri, ya matusi, isiyofaa, na/au mbovu katika ujumbe wa umma au binafsi.
2. Kutumia Intaneti kwa njia ambazo zinakiuka sheria za serikali, jimbo, au za ndani.
3. Kutumia Intaneti shuleni kwa shughuli zisizohusiana na shule.
4. Kutuma ujumbe ambao unaweza kusababisha kupoteza kazi au mifumo ya mpokeaji.
5. Kutuma barua za mfuatano au mipango ya piramidi kwa orodha au watu, na aina nyingine yoyote ya matumizi ambayo yanaweza kusababisha msongamano wa mtandao au kutatiza kazi ya wengine.
6. Kutumia Intaneti kwa malengo ya kibiashara.
7. Kutumia Intaneti kwa ushawishi wa kisiasa.
8. Kubadilisha faili yoyote ya kompyuta ambayo si ya mtumiaji.
9. Kuchapisha, kutuma au kupokea nyenzo zenye hakimiliki bila ruhusa.
10. Kupeana nenosiri la mtu mwingine kwa wengine kwa kujua.
11. Kutumia nenosiri la mtu mwingine.
12. Kutumia ufikiaji wa Intaneti kutuma, kuepua, kuunda, na au/au kutazama nyenzo za hakimiliki.
13. Kuchapisha faili zisizofaa za matini au faili ambazo ni hatari kwa uadilifu wa mtandao wowote.
14. Kubadilisha hatua za usalama kwenye kompyuta za shule, kompyuta au mitandao ya mbali.
15. Kujaribu kufikia rasilimali, programu au data nyingine.
16. Kuharibu, ambayo inafafanuliwa kama jaribio lolote la nia mbaya la kuharibu data ya mtumiaji mwingine kwenye Intaneti, na inajumuisha kupakia au kuunda virusi vya kompyuta.
17. Kuiba utambulisho wa mtu wakati unatumia Intaneti.

Shule za Umma za Richmond hutumia zana za teknolojia zinazojulikana kama Gaggle katika viwango vya shule ya msingi, kati na upili ili kusaidia divisheni kudumisha mazingira salama ya mtandaoni kwa wanafunzi wote. Gaggle ni zana ya teknolojia ya uchanganuzi ambayo inafuatilia na kupitia faili za Google za mwanafunzi, 24-7 kwa picha na maudhui yasiyofaa.

Taarifa za Gaggle huunga mkono maendeleo ya mwanafunzi katika matumizi yanayofaa ya teknolojia ya elimu na Chromebooks.

- Taarifa zinazohusisha maudhui au picha zisizofaa, vitisho vya kujiumiza mwenyewe au vitisho kwa wengine zitaripotiwa kwa usimamizi wa shule na wanatimu wa ofisi kuu, ambao watawasiliana na wazazi moja kwa moja. Vitisho vinavyokaribia vya usalama na ustawi vitariporiwa kwa mhudumu anayefaa wa dharura ili kutoa msaada.
- Taarifa kuhusu picha au video za ngono za watoto zitaripotiwa na Gaggle kwa wasimamizi wa shule, watekelezaji sheria wa ndani na Kituo cha Kitaifa cha Watoto Waliopotea na Kutumiwa Vibaya ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi.

Sheria zote za shule zinatumika kwa maudhui kwenye Google Drive ya mwanafunzi. Wanafunzi wanahimizwa kukagua picha na filamu zilizohifahiwa hapo. Ikiwa mwanafunzi hawezi kuunganisha simu ya mkononi kwenye Chromebook na anaruhusu simu kupakia picha na filamu, wanaweza kuwajibika kwa nyenzo zisizofaa.

# KAMUSI

| KOSA | UFAFANUZI |
|---|---|
| **Pombe** | Kukiuka sheria au amri, inayopinga utengenezaji, uuzaji, ununuzi, usafiri, umiliki, au matumizi ya vinywaji vinavyolewesha vya pombe au bidhaa inayowasilishwa kama pombe. Tuhuma ya kuwa chini ya ushawishi wa pombe inaweza kujumuishwa ikiwa itasababisha hatua ya kinidhamu. |
| **Mabishano** | Makabiliano, vita au uchokozi wa maneno / kimwili ambao hausababishi majeraha. |
| **Uchomaji kwa makusudi** *(Uliofanyika / Kujaribiwa)* | Kuharibu kinyume na sheria na kwa makusudi au kujaribu kuharibu mali yoyote ya shule au ya kibinafsi kwa moto au kifaa cha kutia moto. Vibaruti, fataki, na moto wa pipa la taka unaweza kujumuishwa katika kategoria hii ikiwa zilikuwa mambo yanayochangia moto wa kuharibu |
| **Shambulio kwa kutumia Bastola au Silaha Nyingine Dhidi ya Wafanyakazi** | Kumgusa au kumgonga mfanyakazi kwa njia ya kukera, ya lazima, ya ukatili na ya makusudi kinyume cha mapenzi yake, ambayo kwa makusudi husababisha madhara ya kimwili kupitia kutumia matumizi ya bastola au silaha nyingine. |
| **Shambulio bila kutumia Bastola au Silaha Dhidi ya Wafanyakazi** | Shambulio la kukera na la makusudi dhidi ya mfanyakazi ambalo kwa makusudi husababisha madhara ya kimwili bila kutumia bastola au silaha. |
| **Shambulio kwa kutumia Bastola au Silaha Nyingine Dhidi ya Mwanafunzi** | Kumgusa au kumgonga mwanafunzi kwa njia ya kukera, ya lazima, ya ukatili na ya makusudi kinyume cha mapenzi yake, au kushiriki kwa pamoja katika vita ambavyo kwa makusudi vinasababisha madhara ya kimwili kwa kutumia matumizi ya bastola au silaha nyingine. |
| **Shambulio bila kutumia Bastola au Silaha Dhidi ya Mwanafunzi** | Kumgusa au kumgonga mfanyakazi kwa njia ya kukera na ya makusudi kinyume cha mapenzi yake ambayo au kushiriki kwa pamoja katika vita ambavyo husababisha madhara ya kimwili bila kutumia bastola au silaha. |
| **Shambulio, Kumjeruhi Mtu kwa Nia Mbaya bila kutumia Silaha** | Kusababisha majeraha ya kimwili kwa mtu kwa makusudi (bila silaha) na lengo la kulemaza, kuharibu au kuua. |
| **Shambulio bila Majeraha ya Kimwili** | Shambulio, bila majeraha ya kimwili, ya mtu yeyote kwenye basi la shule, kwenye rasilimali za shule, au katika tukio linalofadhiliwa na shule. |
| **Kuvunja na Kuingia** *(Wizi wa uvunjaji)* | Kuingia au kujaribu kungia jengo au muundo mwingine kinyume na sheria na lengo la kutekeleza uhalifu. |
| **Ushambulizi** | Shambulio lolote la kimwili, haijalishi kiwango, linalofanywa kwa mtu mwingine kwa njia ya hasira, ukatili au ulipizaji kisasi. |
| **Udhalimu** | Sehemu ya § 22.1-276.01 ya sheria inafafanua maonevu kama tabia yoyote ya ukatili na isiyohitajika ambayo inalenga kudhuru, kutisha, au kumdhalilisha mhasiriwa; inahusisha ukosefu wa usawa wa nguvu wa kweli au unaokisiwa kati ya mkosaji; na mhasiriwa; na inarudiwa kwa muda au kusababisha kiwewe kikali cha kihisia. Hii inajumuisha maonevu ya mtandaoni. Haijumuishi utani wa kawaida, kuchezeana, mabishano, au mzozano wa wanarika. Bodi ya shule zinatarajiwa kujumuisha maonevu kama tabia iliyopigwa marufuku katika kanuni zao za maadili mema ya wanafunzi. |
| **Unyakuzi** | Kushikilia na/au kuchukua mali ya mwanafunzi katika juhudi za kupunguza/kuzuia usumbufu katika mazingira ya shule. |
| **Tabia Zisizokubalika / Kutotii** | Kutotaka kutii mamlaka au kukataa kutii ombi lolote linalofaa. Kitendo chochote ambacho kwa makusudi kinatatiza shughuli za kawaida za shule. Tabia yoyote ambayo inatatiza pakua mazingira ya kawaida ya masomo. |
| **Tabia ya usumbufu** | Tabia ambayo inatatiza mazingira ya masomo. Kosa husika la tabia zisizokubalika linafafanuliwa kama kuhusisha lengo la kusababisha usumbufu kwa umma, kukera au wasiwasi, au kusababisha hatari bila kujali. |
| **Sheria ya Mavazi na Usafi** | Humaanisha tabia, sera au sehemu yoyote ya kanuni ya maadili ya wanafunzi iliyochukuliwa na bodi ya shule ambayo inasimamia au kuzuia mavazi, mwonekano, au usafi, ikiwemo mtindo wa nywele, wa mwanafunzi yeyote aliyesajiliwa. |
| **Ukiukaji wa Dawa za Kulevya Ratiba I na II** *(Dawa za Kusisimua Misuli, Matumizi/Kumiliki Bangi)* | Ukiukaji wa sheria au amri zinazopiga marufuku utengenezaji, usafiri, umiliki na matumizi ya bangi, dawa za kulevya za Ratiba I na II, na matumizi ya dawa za kusisimua misuli. Tuhuma ya kuwa chini ya ushawishi wa bangi inaweza kujumuishwa ikiwa itasababisha hatua ya kinidhamu. |

| | |
|---|---|
| **Ukiukaji wa Dawa za Kulevya Matumizi / Kumiliki Dawa Zinazofanana na Nyingine** | Kutumia, kupanda, kutengeneza, kununua, kumiliki, kusafirisha, au kuleta bidhaa yoyote kinyume na sheria inayowasilisha kama inafanana na dawa nyingine. |
| **Ukiukaji wa Dawa za Kulevya Vivutiaji** | Kutumia, kupanda, kutengeneza, kununua, kumiliki, kusafirisha, au kuleta vivutiaji vyovyote. |
| **Ukiukaji wa Dawa za Kulevya Dawa Zinazoagizwa na Daktari** *(Wizi /Jaribio la Wizi)* | Kumiliki au kujaribu kumiliki kinyume cha sheria dawa zilizoagiziwa mtu mwingine. |
| **Ukiukaji wa Dawa za Kulevya Ratiba I na II** *(Dawa za Kusisimua Misuli, Mauzo/ Usambazaji wa Bangi)* | Kumiliki kinyume cha sheria kwa lengo la kusambaza, kuuza, au kuomba dawa yoyote ya Ratiba I au II, bangi, au dawa za kusisimua misuli. |
| **Ukiukaji wa Dawa za Kulevya Ratiba III– VI** *(Matumizi, Umiliki, Usambazaji, Kumiliki Vifaa)* | Kutumia au kumiliki kinyume cha sheria kwa lengo la kusambaza, kuuza, au kuomba dawa yoyote inayodhibitiwa au bidhaa za nikotoni zisizobainishwa katika kategoria za awali za dawa. Kuwa na vifaa, ambavyo vinaweza kutumiwa katika matumizi ya dawa haramu, katika mfuko, begi, gari au kabati la mtu. |
| **Ukiukaji wa Dawa za Kulevya Dawa za Kununuliwa Kwenye Kaunta** *(Matumizi/Umiliki/Usambazaji)* | Matumizi, usambazaji, uuzaji, uombaji, ununuzi, umiliki, usafiri au kuleta nchini kinyume cha sheria dawa za Kununuliwa kwenye kaunta. |
| **Sigara za Elektroniki** | Kumiliki, kutumia, kusambaza, au kuuza sigara za elektroniki au vifaa kwenye majengo ya shule, katika matukio yanayofadhiliwa na shule, na/au kwenye usafiri wa shule. |
| **Vifaa vya Elektroniki** | Kutumia vifaa vya elektroniki ambavyo vinachukuliwa havifai katika mazingira ya elimu. |
| **Unyanganyi** | Kupata au kujaribu kupata kitu cha thamani kutoka kwa mtu mwingine kinyume cha sheria kwa kumlazimisha mtu huyo kukupa kwa tishio la kuumizwa kimwili na/au majeraha mengine kwa mtu huyo au mali ya mtu huyo. |
| **Kupigana BILA Majeraha au Majeraha Madogo** | Kushiriki kwa pamoja katika vita vinavyohusisha vurugu ya kimwili ambapo majeraha ni madogo au hayapo. Majeraha yanaweza kujumuisha, lakini hayajakomea kwa yafuatayo: kukwaruzwa mwili au kuchibuka kidogo. |
| **Kucheza kamari** | Kufanya, kuweka au kupokea beti yoyote ya kifedha ya kitu kingine chochote cha thamani, kilichofanyika ili kupata nafasi ya kushinda zawadi, hisa au mazingatio mengine au kitu cha thamani. |
| **Shughuli za Magenge** | Genge linamaanisha shirika, au kundi lolote linaloendelea la watu watatu au zaidi, liwe rasmi au lisilo rasmi, ambalo lina mojawapo ya malengo au shughuli zake kuu ni kutekeleza shughuli moja au zaidi za uhalifu au zisizo za uhalifu (i) ambalo lina mojawapo ya malengo au shughuli zake kuu katika kuwezesha shughuli moja au zaidi, (iii) ambalo lina jina linaloweza kutambuliwa au ishara inayoweza kutambuliwa, na (iii) ambalo wanachama wake kivyao au kwa pamoja wameshiriki katika utekelezaji, jaribio la utekelezaji, au kufanya vitendo viwili au zaidi vya jinai, angalau moja ambalo ni kitendo cha mzozo, ilimradi vitendo hivyo havikuwa sehemu ya kitendo au muamala wa kawaida." Hii inajumuisha mavazi ambayo yanaonyesha ushirika, matambiko, au shughuli zinazotambuliwa na makundi ya wanafunzi. |
| **Unyanyasaji Usio wa Kingono** *(Kimwili, Maneno au Kisaikolojia)* | Kurudia kumkera au kumshambulia mwanafunzi au kundi la wanafunzi , au wafanyakazi wengine ambayo husababisha mazingira ya hofu au mabaya ya elimu au ya kazi. |
| **Udhalilishaji** | Kutekeleza vitendo dhidi ya mwanafunzi au kumlazimisha mwanafunzi kutekeleza vitendo ambavyo vinasababisha majeraha kwa mtu ili kuingizwa katika shirika, timu, au darasa la wanafunzi. |
| **Mauaji Dhidi ya Mfanyakazi kwa Kutumia Bunduki** | Kifo chochote cha mfanyakazi kinachosababishwa na matumizi ya bunduki (kando na kujidhuru au kujitoa uhai). |
| **Mauaji Dhidi ya Mwanafunzi kwa Kutumia Bunduki** | Kifo chochote cha mwanafunzi kinachosababishwa na matumizi ya bunduki (kando na kujidhuru au kujitoa uhai). |
| **Mauaji Dhidi ya Mfanyakazi kwa Kutumia Silaha Nyingine** | Kifo chochote cha mfanyakazi kinachosababishwa na matumizi ya silaha (kando na kujidhuru kwa bahati mbaya au kujitoa uhai). |
| **Mauaji Dhidi ya Mwanafunzi kwa Kutumia Silaha Nyingine** | Kifo chochote cha mwanafunzi kinachosababishwa na matumizi ya silaha (kando na kujidhuru kwa bahati mbaya au kujitoa uhai). |

| | |
|---|---|
| **Kuchochea Ghasia** | Kutumia nguvu au vurugu kinyume na sheria ambako kunahatarisha pakubwa usalama, amani, au mpangilio wa umma. Watu watatu au zaidi wakishirikiana. |
| **Utekaji Nyara** | Kuchukua, kusafirisha, na/au kumfunga mtu kinyume cha mapenzi yake na kinyume cha sheria, au mtoto bila ridhaa ya mzazi mlezi au mlezi wa kisheria. Kategoria hii inajumuishwa utekaji nyara. |
| **Ukiukaji Mwingine** | Ukiukaji ambao haufai kwa tabia ya shule. |
| **Urejeshaji** | Kurejesha bidhaa ambazo ziliibiwa au kuharibiwa au kutoa thamani ya haki ya soko kwa njia ya fidia au huduma. |
| **Wizi** | Kuchukua au kujaribu kuchukua kitu chochote chenye thamani kinachomilikiwa na mtu au shirika lingine chini ya mazingira ya makabiliano kwa nguvu au tishio la nguvu au uhasama na/au kwa kumfanya mhadhiriwa kuwa na hofu. |
| **Unyemeleaji** | Kushiriki katika tabia inayomlenga mtu mwingine kwa lengo la kumfanya mtu huo kuwa na hofu ya kifo, shambulio la kingono, au majeraha ya kimwili. |
| **Shambulio la Kingono** | Shambulio la kingono kwa mtu kwa kutumia nguvu, tishio, au kutumia hofu. |
| **Unyanyasaji wa Kingono** | Utongozaji wa kingono usiotakikana, maombi ya fadhila za kingono, au tabia nyingine za kimwili au za maneno au mawasiliano ya hali ya kingono, ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia ambao unaunda mazingira mabaya ya hofu, au ya kielimu au ya kikazi. |
| **Shambulio la Kingono Dhidi ya Wafanyakazi** | Shambulio la Kingono dhidi ya Wafanyakazi linahusisha tishio la kukera au la makusudi, matumizi ya hofu au ya kimwili ya kutoweza kujisaidia ya unyanyasaji wa kingono. Shambulio ka kingono ni kosa la Daraja la 1. |
| **Shambulio la Kingono Dhidi ya Mwanafunzi** | Shambulio la Kingono dhidi ya mwanafunzi linahusisha tishio la kukera au la makusudi, matumizi ya hofu au ya kimwili ya kutoweza kujisaidia ya unyanyasaji wa kingono. Shambulio ka kingono ni kosa la Daraja la 1. |
| **Makosa ya Kingono Dhidi ya Wafanyakazi** | Kuingilia mfanyakazi kingono bila ridhaa (k.m. mdomo, mkundu au uke). |
| **Makosa ya Kingono ya Lazima Dhidi ya Mwanafunzi** | Makosa ya Kingono ya Lazima Dhidi ya Mfanyakazi yanajumuisha pia ubakaji wa watoto, ambao unafafanuliwa kama kuingilia kingono na au bila ridhaa ya mtoto. |
| **Jaribio la Shambulio la kwa Lazima** | Jaribio la kuingilia kingono (k.m mdomo, mkundu au uke) bila idhini ya mwanafunzi, ikiwemo ubakaji, au kuingilia kingono bila au na ridhaa ya mtoto. |
| **Makosa ya Kingono Dhidi ya Wanafunzi** | Tabia mbaya, ufichuzi usiofaa ambao unajumuisha kujamiiana, tabia za kingono, au tabia nyingine kinyume cha sheria au tabia inayolenga kusababisha kuridhika kingono bila kutumia nguvu au vitisho. Zingatia umri, tabia inayofaa kwa ukuaji, na hali ya ulemavu kabla ya kutumia kategoria hii. |
| **Makosa ya kingono - Kumgusa Mfanyakazi kwa Kukera** | Mgusano usiofaa wa kimwili dhidi ya mfanyakazi ambao unakera, haufai, na/au usiotakikana kama ilivyobainishwa na mhasiriwa. |
| **Makosa ya kingono - Kugusa kwa Kukera** | Mgusano usiofaa wa kimwili dhidi ya mwanafunzi ambao unakera, haufai, na/au usiotakikana kama ilivyobainishwa na mhasiriwa. |
| **Tishio Shuleni Tishio la Bomu** *(Tishio la Uharibifu au Madhara)* | Tishio lolote (la maneno, kuandikwa, au elektroniki) na mtu la kubomu au kutumia vitu au vifaa vingine kwa lengo la kulipua, kuchoma, kusababisha hasara kwa jengo la shule au mali ya shule, au kuwadhuru wanafunzi au wafanyakazi. Kutoa ripoti ya uongo kwa makusudi ya madhara yanayowezekana kutokana na kemikali hatari au mawakala wa kibiolojia. |
| **Matumizi ya Teknolojia** *(Ukiukaji/Matumizi)* | Ukiukaji usiodhinishwa wa matumizi ya teknolojia kulingana na Sera ya Matumizi Yanayokubalika. |
| **Vitisho/Hofu Dhidi ya Wafanyakazi** | Kuwaweka wafanyakazi katika hofu ya kuumizwa kimwili kinyume cha sheria kupitia vitisho vya kimwili, maneno, vilivyoandikwa au vya elektroniki ambavyo vinaunda mara moja hofu ya madhara bila kuonyesha silaha au kumshambulia mtu kimwili. Zingatia umri, tabia inayofaa kwa ukuaji, na hali ya ulemavu kabla ya kutumia kategoria hii. |
| **Vitisho/Hofu Dhidi ya Mwanafunzi** | Kuwemka mfanyakazi katika hofu ya kuumizwa kimwili kinyume cha sheria kupitia vitisho vya kimwili, maneno, vilivyoandikwa au vya elektroniki bila kuonyesha silaha au kumshambulia mtu kimwili. Zingatia umri, tabia inayofaa kwa ukuaji, na hali ya ulemavu kabla ya kutumia kategoria hii. |

| | |
|---|---|
| **Makosa ya Wizi** *(Bila Kutumia Nguvu)* | Kuchukua, kubeba, kusababisha, au kunyakua mali kinyume cha sheria kutoka kwa mtu mwingine. Inaweza kujumuisha kuiba mifukoni, kuiba kutoka kwa majengo, wizi wa data ya elektroniki, wizi kutoka kwa magari, au wizi kutoka kwa mashine zinazotumia sarafu. |
| **Kosa la Wizi waa Magari** | Kuchukua, kubeba, au kuendesha gari kinyume cha sheria au jaribio la wizi wa gari. Kategoria hii inajumuisha wizi wa gari, pikipiki, gari la kuchezea, gari la kutumiwa kwa theluji, RV, au kitu chochote ambacho kinajiendesha. |
| **Tumbaku** *(Matumizi, Umiliki, Mauzo, Usambazaji)* | Kumiliki, kutumia, kusambaza, au kuuza bidhaa za tumbaku, ikiwemo tumbaku zisizokuwa na moshi, kwenye majengo ya shule, katika matukio yanayofadhiliwa na shule, na/au kwenye usafiri wa shule. |
| **Vifaa vya Tumbaku** | Kuleta vifaa vya tumbaku shuleni au kwa tukio la shule. |
| **Kuingia bila ruhusa** | Kuingia au kusalia kwenye kampasi ya umma au shule au kituo cha bodi ya shule bila idhini au mwaliko na bila lengo halali la kuingia. Hii inajumuisha wanafunzi wanaoondoshwa au kufukuzwa na watu waliodhinishwa wanaoingia au kusalia kwenye kambia au kituo cha bodi ya shule baada ya kuagizwa kuondoka. |
| **Uharibifu wa mali** | Kuharibu kwa kutaka na/au kwa nia mbaya, kuharibu mali ya umma au ya binafsi bila ridhaa ya mmiliki au mtu anayetunza au kudhibiti mali. Kategoria hii inajumuisha grafiti. |
| **Silaha (1) Bunduki / Bastola** | Umiliki au kuleta bunduki/bastola shuleni au kwa tukio linalofadhliiwa na shule. |
| **Silaha (2) Bunduki / bunduki kubwa** | Umiliki au kuleta bunduki/bunduki kubwa shuleni au kwa tukio linalofadhiliwa na shule. |
| **Silaha (3) Zinazorusha** | Kumiliki au kuleta shuleni au kwenye tukio linalofadhiliwa na shule silaha yoyote iliyoundwa kurusha au ambalo linaweza kubadilishwa kuwa bunduki ili kurusha kwa hatua ya kifaa kinacholipua. |
| **Silaha (4) Kisu** | Kumiliki au kuleta shuleni au katika tukio linalofadhiliwa na shule kifaa chochote kikali ambacho kimeainishwa kama kisu yenye bapa ya inchi tatu au zaidi. |
| **Silaha (5) Bunduki Nyingine** | Kumiliki au kuleta silaha nyingine yoyote shuleni au katika tukio la shule ambalo limeundwa kurusha kwa hatua ya kilipuzi. Hii inajumuisha bunduki isiyotajwa awali (inayofanya kazi au isiyofanya kazi, iliyo au isiyokuwa na risasi) kama vile, lakini haijakomea kwa bunduki ya kuanzisha mbio. |
| **Silaha (6) Silaha Nyingine** | Kumiliki au kuleta silaha yoyote, kifaa, au kitu shuleni au kwa tukio la shule ambalo linaweza kusababisha madhara kwa mtu mwingine. (K.m., kigoe cha kucheza gofu, gongo la besiboli, minyororo, nunchakus, au vijiti/nightsticks/Billy clubs) |
| **Bunduki ya kani ya hewa** *(Bunduki ya BB)* | Kumiliki au kuleta bunduki yoyote ya kani ya hewa kwa shule au tukio la shule. Bunduki ya kani ya hewa inajumuisha bunduki za BB, za kurusha rangi na peleti. |
| **Umiliki wa Kifaa cha Kilipuzi** | Kumiliki au kuwakilisha silaha yoyote ambayo inalipuka au imeundwa au inaweza kubadilishwa haraka ili kulipuka. |
| **Matumizi ya Bomu na Kifaa cha Kilipuzi** | Kutumia silaha yoyote ambayo imeundwa kulipuka kwa kutumia kifaa cha kuanzisha au kwa matokeo ya kemikali ambayo yanasababisha kulipuka. |
| **Umiliki wa Risasi** | Umiliki wa aina yoyote ya risasi. Risasi inamaanisha mtutu wa risasi, kesi, au poda ya kichochezi iliyoundwa kutumiwa katika bunduki yoyote. |
| **Silaha / Bidhaa Zinazofanana** | Kifaa chochote ambacho kinafanana na bunduki ya kweli kama vile bunduki ya kuchezea (k.m. Bunduki ya maji). Kategoria hii inajumuisha bia silaha zinazofanana. |
| **Silaha / Bidhaa zenye Kemikali** | Kumiliki au kuleta shuleni au kwenye tukio linalofadhiliwa na shule bidhaa yoyote inayotumiwa kama silaha. Vitu kama vile panya, gesi ya machozi, na kinyunyizia pilipili. |
| **Silaha Zinazowezekana** | Kumiliki kisu ambacho kiko chini ya inchi tatu, bapa za wembe, vikata sanduku, fataki, baruti, au bomu shuleni au katika tukio la shule. |
| **Kumiliki Bunduki ya Kushtukiza** | Kumiliki au kuleta mbinu yoyote ambayo imeundwa kutoa umeme, sumaku au chaji yoyote au mshtuko kupitia matumizi ya mrusho na inayotumiwa kwa lengo la kumlemaza mtu kwa muda. |
| **Kumiliki Bunduki ya Kushtukiza** | Kumiliki au kuleta mbinu yoyote ambayo imeundwa kutoa umeme, sumaku au chaji inayozidi usawa wa hatzi 60 miliampu za Kushtukiza na kutumiwa kwa lengo la kumlemaza mtu kwa muda. |

## NAMBARI ZINAZOPIGWA MARA KWA MARA

| | |
|---|---|
| **Maelezo ya Jumla** | **804-780-7710** |
| **Idara ya Mtalaa na Mafunzo** | **804-780-7751** |
| **Idara ya Usafiri wa Wanafunzi** | **804-674-1234** |
| **Elimu ya Kipeke** | **804-780-7911** |
| **Culture, Climate and Student Services** | **804-780-6070** |
| **Huduma za Afya** | **804-780-7801** |
| **Ofisi ya Usikilizaji** | **804-780-7808** |
| **Pupil Placement Services** | **804-780-7811** |
| **Huduma za Kazi za Jamii** | **804-780-7850** |
| **Ofisi ya Bodi ya Shule** | **804-780-7716 / FAKSI: 804-780-8133** |

## WANACHAMA WA BODI YA SHULE

| | | |
|---|---|---|
| **WILAYA YA 7** | **Cheryl Burke, Mwenyekiti** | ***cburke2@rvaschools.net*** |
| **WILAYA YA 4** | **Jonathan Young, Makamu wa Mwenyekiti** | ***jyoung7@rvaschools.net*** |
| **WILAYA YA 1** | **Elizabeth Doerr** | ***edoerr@rvaschools.net*** |
| **WILAYA YA 2** | **Mariah White** | ***mwhite4@rvaschools.net*** |
| **WILAYA YA 3** | **Kenya Gibson** | ***kgibson@rvaschools.net*** |
| **WILAYA YA 5** | **Stephanie Rizzi** | ***srizzi@rvaschools.net*** |
| **WILAYA YA 6** | **Shonda Harris-Muhammed** | ***smuhamme@rvaschools.net*** |
| **WILAYA YA 8** | **Dawn Page** | ***dpage@rvaschools.net*** |
| **WILAYA YA 9** | **Nicole Jones** | ***njones6@rvaschools.net*** |

RPS RICHMOND PUBLIC SCHOOLS

# Kalenda Rasmi ya Mwaka wa Masomo wa 2022-23

## 2022

**Julai 2022**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 1 | 2 |
| 3 | 4* | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 |
| 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |
| 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 |
| 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 |
| 31 | | | | | | |

**Agosti 2022**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29 | 30 | 31 | | | |

**Septemba 2022**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2* | 3 |
| 4 | 5* | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | |

**Oktoba 2022**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5* | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24* | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |
| 30 | 31 | | | | | |

**Novemba 2022**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| 6 | 7 | 8* | 9 | 10 | 11 | 12 |
| 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 |
| 20 | 21 | 22 | 23 | 24* | 25* | 26 |
| 27 | 28 | 29 | 30 | | | |

**Disemba 2022**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 |
| 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19 | 20 | 21 | 22 | 23* | 24 |
| 25 | 26* | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 |

**Januari 2023**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2* | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
| 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 |
| 15 | 16* | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 |
| 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 |
| 29 | 30 | 31 | | | | |

**Februari 2023**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20* | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | | | | |

## 2023

**Machi 2023**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 | 18 |
| 19 | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 | 25 |
| 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | 31 | |

**Aprili 2023**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7* | 8 |
| 9 | 10* | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |
| 30 | | | | | | |

**Mei 2023**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
| 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 |
| 14 | 15 | 16 | 17 | 18 | 19 | 20 |
| 21 | 22 | 23 | 24 | 25 | 26 | 27 |
| 28 | 29* | 30 | 31 | | | |

**Juni 2023**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | 1 | 2 | 3 |
| 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
| 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 | 17 |
| 18 | 19* | 20 | 21 | 22 | 23 | 24 |
| 25 | 26 | 27 | 28 | 29 | 30 | |

**Julai 2023**

| S | M | T | W | T | F | S |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 1 |
| 2 | 3 | 4* | 5 | 6 | 7 | 8 |
| 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 |
| 16 | 17 | 18 | 19 | 20 | 21 | 22 |
| 23 | 24 | 25 | 26 | 27 | 28 | 29 |
| 30 | 31 | | | | | |

Changanua msimbo wa QR ukitumia simu yako ili uone kalenda, mikutano na taarifa zetu zingine muhimu kwenye tovuti yetu.

**Legend**

- Siku za Kawaida za Shule
- Tarehe za Mwanzo na Mwisho wa Robo na Muhula
- Sikukuu na Mapumziko
- *Mapumziko na Sikukuu za Wafanyakazi wanaofanya Kazi Miezi 12
- Ratiba ya Kwenda Nje Ijumaa katika Msimu wa Kiangazi kwa Wafanyakazi Walioteuliwa
- Siku ya Masomo ya Kitaalamu (Shule Zinafungwa kwa Wanafunzi)
- Siku za Upangaji wa Walimu (Shule Zinafungwa kwa Wanafunzi)
- Siku ya Mkutano wa Watunzaji/Walimu (Shule Zinafungwa kwa Wanafunzi)

## Tarehe za Mwaka wa Masomo wa 2022-2023

- Julai 4: Sikukuu ya Uhuru (RPS Imefungwa)
- Agosti 19: Uelekezaji kwa Walimu Wageni kwa RPS
- Agosti 22 -23: Siku ya Masomo ya Kitaalamu Shuleni
- Agosti 24: Siku ya Masomo ya Chaguo la Kitaalamu
- Agosti 25 -26: Siku ya Upangaji wa Walimu
- **Agosti 29: Siku ya Kwanza ya Shule**
- Agosti 29 - Septemba 1 Wiki ya Kuunda Utamaduni na Uhusiano
- Septemba 2: Siku Kabla ya Sikukuu ya Wafanyakazi: (RPS Imefungwa)
- Septemba 5: Sikukuu ya Wafanyakazi: (RPS Imefungwa)
- Oktoba 5: Yom Kippur (RPS Imefungwa)
- Oktoba 24: Diwali (RPS Imefungwa)
- Novemba 3: Mwisho wa Robo ya Kwanza (Siku ya 45)
- Novemba 7: Siku ya Upangaji wa Walimu (Shule zinafungwa kwa wanafunzi)
- Novemba 8: Sikukuu ya Uchaguzi: (RPS Imefungwa)
- Novemba 21: Siku ya Mkutano wa Watunzaji/Walimu (Shule zinafungwa kwa wanafunzi)
- Novemba 22: Siku ya Masomo ya Chaguo la Kitaalamu (Shule zinafungwa kwa wanafunzi)
- **Novemba 23 -25: Mapunziko ya Shukrani** (Jumatano ya ripoti ya wafanyakazi wanaofanya kazi miezi 12)
- Disemba 19-30: Mapumziko ya Msimu wa Baridi (Shule zitakuwa zimefungwa, angalia * kwa sikukuu za wafanyakazi wanaofanya kazi miezi 12)
- Januari 2: Siku ya Kuadhimisha Mwaka Mpya (RPS Imefungwa)
- Januari 16: Sikukuu ya Martin Luther King, Jr (RPS Imefungwa)
- Februari 1: Mwisho wa Robo ya Pili/Muhula wa Kwanza (Siku ya 90)
- Februari 3: Siku ya Upangaji wa Walimu (Shule zinafungwa kwa wanafunzi)
- Februari 20: Sikukuu ya Rais (RPS Imefungwa)
- Machi 9: Siku ya Masomo ya Chaguo la Kitaalamu (Shule zinafungwa kwa wanafunzi)
- Machi 10: Siku ya Mkutano wa Watunzaji/Walimu (Shule zinafungwa kwa wanafunzi)
- **Aprili 3-7: Mapumziko ya Majira ya kuchipua (Hakuna Masomo)**
- Aprili 10: Jumatatu ya Pasaka (RPS Imefungwa)
- Aprili 19: Mwisho wa Robo ya 3 (Siku ya 135)
- Aprili 21: Siku ya Upangaji wa Walimu (Shule zinafungwa kwa wanafunzi)
- Mei 29: Sikukuu ya Kumbukumbu (RPS Imefungwa)
- Juni 19: Juneteeth (RPS Imefungwa)
- **Juni 23: Kuachiliwa Saa Mbili Mapema/Siku ya Mwisho ya Shule (siku ya 179)**
- Julai 4: Sikukuu ya Uhuru (RPS Imefungwa)

## MANUKUU:

# MAJUKUMU YA WAZAZI NA KUHUSIKA NA UKUBALIFU WA UKAGUZI WA KANUNI YA MAADILI MEMA YA UWAJIBIKAJI WA WANAFUNZI

Wazazi/Walezi wa wanafunzi waliosajiliwa katika Shule za Umma za Richmond wana wajibu wa kusaidia shule katika kutekeleza Kanuni hizi za Maadili ya Uwajibikaji ya Wanafunzi na mahudhurio ya lazima ya shule ili kila mwanafunzi aweze kuelimishwa katika mazingira ambayo hayana usumbufu, hayana vitisho kwa mtu au mali, na yanasaidia haki za kila mtu.

Hadi hapo, Sehemu ya §22.1-279.3 ya Kanuni ya Virginia inahitaji kwamba wazazi wa kila mwanafunzi aliyesajiliwa atie saini na arejeshe Taarifa ya Majukumu ya Wazazi kwa shule ambayo mwanafunzi alisajiliwa.

## Taarifa ya Majukumu ya Wazazi

Mimi, (andika jina lako) ____________________________________ mzazi/mlezi wa kisheria wa

____________________________________________ (andika jina la mwanafunzi) mwanafunzi aliyesajiliwa katika:

____________________________________________, ninakiri kwamba nilipokea Kanuni ya Maadili ya Uwajibikaji ya Wanafunzi ya Shule za Umma za Richmond (SCORE) na nakala ya sheria ya mahudhurio ya lazima. Ninaelewa kwamba ni lazima nitie saini na niweke tarehe taarifa hii na niirejeshe kwa shule ya mtoto wangu.

Ninaelewa kwamba kukubali kwangu kupokea SCORE na sheria ya mahudhurio ya lazima ya shule hakuondoi haki zozote za mzazi zilizolindwa na katiba au sheria za serikali au jimbo, ikiwemo haki yangu ya kuomba rufaa ya hatua za kuondoshwa kwa muda au kufukuzwa kama ilivyotolewa katika §22.1-277.04 na §22.1-277.05 ya Sheria ya Virginia na kwamba nina haki ya kupinga sera na/au maamuzi ya shule au ya divisheni ya shule.

Tafadhali pitia **Kanuni ya Maadili ya Uwajibikaji ya Wanafunzi (SCORE)** na mtoto wako. Shule itajadili SCORE na sera na masharti inayorejelea kama sehemu muhimu ya maisha ya kila siku ya mwanafunzi, na kuunga mkono mazingira salama ya mafunzo. Kutakuwa na uhakiki wa mara kwa mara wa sehemu muhimu za Kanuni mwaka mzima, hasa sehemu zinazohusiana na:

- **Uadilifu wa Elimu**
- **Matumizi ya Rasilimali za Teknolojia na Wanafunzi**
- **Maonevu, Maonevu ya mtandaoni, Unyanyasaji, Hofu na Udhalilishaji**

Ni muhimu kwamba familia na shule zifanye kazi pamoja ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanatimiza matarajio ya juu yaliyowekwa katika Kanuni ya Maadili ya Uwajibikaji ya Wanafunzi. Hii huwawezesha wanafunzi kufanikiwa shuleni, nyumbani, na katika jamii yetu.

**Baada ya kupitia Kanuni ya Maadili ya Uwajibikaji ya Wanafunzi na mtoto wako, tafadhali tia saini na urejeshe fomu hii iliyotiwa saini kwa shule kabla ya Ijumaa, 30 Septemba 2022.**

Kama mzazi/mlezi wa mwanafunzi hapo juu, nimesoma na kujadili Kanuni ya Maadili ya Uwajibikaji ya Wanafunzi na mtoto wangu na ninaelewa kwamba sera na masharti, yaliyorejelewa katika SCORE yanatumika kwa wanafunzi wote, na kila wakati tukiwa kwa majengo ya divisheni ya shule, ikiwemo majengo, mabasi na magari.

_________________________________ _____________________________

**Saini ya Mzazi/Mlezi wa Kisheria** **Tarehe**

_________________________________ _____________________________

**Saini ya Mwanafunzi** **Tarehe**

# Matumizi Yanayokubalika

## Makubaliano wa Mwanafunzi

Nimesoma maelezo kuhusu matumizi yanayokubalika kwenye kurasa za 39 na 40. Ikiwa sikuelewa maana ya sehemu yoyote ndani yake, nilimuuliza mtu mzima kuifafanua kwangu. Ninakubali kufuata kanuni hizi nyakati zote wanakati ninatumia bidhaa za RPS na/au intaneti. Kushindwa kufuata kanuni hizi kunaweza kusababisha hatua ya kinidhamu kulingana na SCORE na kupoteza fadhila.

_________________________________ _____________________________

**Saini ya Mwanafunzi** **Tarehe**

## Mzazi au Mlezi wa Kisheria

Mwanangu, aliyetajwa hapo juu, anaelewa sheria ambazo anapaswa kufuata katika kutumia intaneti na/au vifaa. Nimeongea na mtoto wangu ili kuhakikisha kwamba kanuni hizi zinaeleweka. Ninagundua kwamba walimu na maafisa wengine wa shule watajaribu wawezavyo kutoa nyenzo zinazofaa kielimu kutoka kwa intaneti kwa mtoto wangu na kwamba, iwapo picha au maelezo ya kupingwa yatatokea kwa bahati mbaya, mhudumu wa shule atachukua hatua mara moja ili kurekebisha hali hiyo. Ninatoa ruhusa yangu kwa Shule za Umma za Richmond kwa mtoto wangu kutumia inavyofaa intaneti na/au kifaa.

_________________________________ _____________________________

**Saini ya Mzazi/Mlezi wa Kisheria** **Tarehe**

RPS RICHMOND PUBLIC SCHOOLS

Chapisho la

# SHULE ZA UMMA ZA RICHMOND

Richmond, Virginia

Kulingana na sheria za serikali, sheria za Jumuiya ya madola ya Virginia na sera za Bodi ya Shule ya Jiji la Richmond, Shule za Umma za Richmond hazibagui kwa msingi wa jinsia, mbari, rangi, umri, dini, ulemavu, au asili ya kitaifa katika matoleo ya ajira na huduma. Timu ya Shule za Umma za Richmond huendesha mipango ya haki sawa na usawa wa kijinsia kwa wanafunzi na wafanyakazi. Timu ya Shule za Umma za Richmond ni mwajiri anayetoa nafasi sawa na usawa wa kijinsia. Bodi ya Shule pia inaunga mkono nafasi sawa na kutendewa sawa kwa watu wote haijalishi mapendeleo ya kingono. Mratibu wa Sehemu ya 504 ni Bi. Renesha Parks, Mkurugenzi wa Elimu ya Kipekee, 301 North 9th Street, Richmond, Virginia 23219, (804) 780-7911. Mratibu wa ADA ni Bw. Timothy Williams, Meneja wa Ombudsman, 301 North 9th Street, Richmond, Virginia 23219, (804) 780-7864. Maafisa wa The Title IX ni Bw. Timothy Williams na Bi. Regina Ellis, 301 North 9th Street, Richmond, Virginia 23219, (804) 780-7864 / (804) 780-7867. Ofisi ya Haki za Raia za Idara ya Elimu ya Marekani inaweza kufikiwa kwa 400 Maryland Avenue, SW, Washington, DC 20202, (202) 401-2000 au 1-800-872-5327.

**Jason Kamras, Msimamizi**